

KSh.3,000

**UCHANGANUZI WA METHALI ZA KISWAHILI: MTAZAMO WA  
KIUDENGUZI**

NA

**MURITHI MOSES MUREGA**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI  
ILI KUTOSHELEZA SEHEMU YA MAHITAJI YA SHAHADA YA  
UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA.**

2015

**KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na wala haijawahi kuwasilishwa kwa madhumuni ya shahada yoyote katika Chuo Kikuu kingine.

Sahihi: ..... 

Tarehe: ..... 14/10/2015

Murithi Moses Murega

C50/CE/21213/2012

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Sahihi: ..... 

Tarehe: ..... 15/10/2015

Dkt. Joseph N. Maitaria

Idara ya Kiswahili

Chuo kikuu cha Kenyatta

Sahihi: ..... 

Tarehe: ..... 15/10/15

Prof. Catherine Ndungo

Taasisi ya Masomo ya Kiafrika / Idara ya Kiswahili

Chuo kikuu cha Kenyatta

## **TABARUKU**

Kwa mamangu mpendwa Teresina kwa kujitolea kwa hali na mali ili nitimize ndoto yangu ya kupata elimu. Pia, kwa binti yangu Jamila; kua kwa kuienzi lugha ya Kiswahili mwanangu.

## SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu mwenye kuneemesha neema za kila namna kwa kunineemeshea neema hii ya kupata nafasi ya kufikia kiwango hiki cha elimu na hususan kuchangia ujuzi katika lugha ninayoienzi sana; Kiswahili.

Pia nawashukuru wasimamizi wangu Dkt. Joseph N. Maitaria na Prof. Catherine Ndungo kwa maelekezo na mawaidha yao ya busara nilipokuwa nikiishughulikia kazi hii. Asanteni kwa kujitolea kwenu katika kuhakikisha kuwa kazi hii imefanikiwa. Nawashukuru pia wahadhiri wengine walionipa mawaidha ya kunifaa kama vile Dkt. Edwin Masinde na Dkt. Pamela Ngugi walionifaa kitaalamu nilipokuwa nikiichagua mada yangu. Asanteni kwa kuchukua muda wenu mwingi kunielekeza na kunikosoa. Pasingekuwa msaada wenu kazi hii isingefanikiwa abadani. Mungu awashushie Baraka zake zisizo kifani.

Mamangu Teresina na kakangu Kabengi, asanteni sana kwa kujitolea kwenu kuhakikisha kuwa sikosi karo nilipokuwa shule ya upili na Chuo Kikuu. Kwa mke wangu mpenzi Irene Kananu (Kageni); asante sana kwa kunipa hamasa ya kuendeleza masomo yangu na kunipa imani kwamba ninaweza.

Nawashukuru pia rafiki zangu niliojenga nao urafiki wa dharti na wakaishia kuwa msaada mkubwa kwangu kielimu kama vile Joseph Kaberia, Kiponda (Sifa Sikubali), Annarita Masai Esther Nelima Mulumeti na Judy Onguka miongoni mwa wengine wengi.

Walimu wangu wote kutoka chekechea hadi chuo kikuu sina la kuwatosha ninyi ila kuwaombea Rabana awatunze kwa kazi yenu mufti. Shukrani spesheli zimwendee mwalimu wangu wa Kiswahili katika shule ya upili ya Karama (Meru) Bi. Sabina

Gitonga kwa kunifanya nikiambatie na kukienzi sana Kiswahili. Popote ulipo Mungu akubariki.

Nalishukuru pia shirika la HELB kwa kunipa ufadhili wa kulipia sehemu ya karo yangu kwa masomo ya shahada hii ya uzamili. Naomba Mwenyezi Mungu alidumishe shirika hili ili kuwahudumia wengine wengi wenye mahitaji kama mimi. Bwana Khalid, Mkurugenzi mkuu wa shirika la utafiti wa lugha na utamaduni wa Kiswahili, RISSEA, mjini Mombasa asante sana kwa ushauri wako na kwa kunipatanisha na Bwana Azwaj, Bi. Amira Msellem, Bi. Sharifa na Bwana Ahmad Nassir walionifaa zaidi.

Mwisho, sitawasahau wote walionisaidia katika safari yangu ya kiusomi hadi kufikia kilele. Asanteni sana; msaada wenu umenifikisha mbali.

## IKISIRI

Utafiti huu umezichanganua methali za Kiswahili kwa mtazamo wa kiudenguzi. Utafiti huu umefanywa ikizingatiwa kuwa maana za matini hujiahirisha kwa ambavyo hakuna matini iliyo na maana moja. Sababu kuu ya kuchagua mada hii ilikuwa kubainisha kuwa baadhi ya methali za Kiswahili zina dhima hasi kwa jamii kinyume na dhana ya kijumla kuwa methali zote zina dhima chanya ambayo ndiyo tu imekuwa ikiangaziwa. Kwa misingi hii, malengo ya utafiti huu yamekuwa kutambua miktadha ya matumizi ya methali za Kiswahili zenye dhima hasi, kuziainisha methali za Kiswahili zenye dhima hasi kutegemea uhasi wake na kutambua manufaa ya methali za Kiswahili zenye dhima hasi kwa jamii. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Udenguzi. Nadharia ya Udenguzi iliufaa utafiti huu kwa kuwa inawiana na lengo kuu la utafiti ambalo ni kuonyesha kuwa baadhi ya methali za Kiswahili zina maana hasi; maana hii inaweza kupatikana tu kwa kuzidengua. Data zilizotumika katika utafiti zilikusanywa maktabani ambapo kupitia usomaji methali za Kiswahili zinazopatikana katika kamusi mbalimbali za methali zilihakikiwa kwa makini na kubainisha dhima iliyomo; yaani uchanya au uhasi wake. Baada ya data (methali zenye dhima hasi) kukusanywa ziliainishwa kulingana na ujumbe uliomo kisha zilichanganuliwa kutegemea ujumbe husika na hususan kuzingatia dhima ya methali husika. Matokeo ya utafiti yamebainisha kuwa methali zenye dhima hasi kama kuchochea vita, kudharau wanyonge, kuvunja moyo, kudhihaki ulemavu na zenye ubaguzi wa kikabila, kiuana na kiumri zipo. Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti na nadharia teule. Utafiti huu umegawika katika sura tano ambazo ni utangulizi uliochukua sura ya kwanza huku muktadha wa matumizi ya methali zenye dhima hasi ikichukua sura ya pili. Sura ya tatu inahusisha uchanganuzi wa methali za Kiswahili zenye dhima hasi kwa misingi ya nadharia ya Udenguzi. Aidha, sura ya nne imejikita katika uchunguzi wa manufaa ya methali zenye dhima hasi zilizochanganuliwa katika sura ya tatu kwa jamii huku sura ya tano ikibeba hitimisho na mapendekezo kwa utafiti zaidi.

## UFAFANUZI WA ISTILAHU MUHIMU

**Uchanganuzi :** Utaratibu wa kutumia mbinu za kisayansi na miongozo ya kinadharia kukichambua kipengele cha lugha au cha fasihi.

**Kiswahili:** Lugha ya Kibantu yenye asili ya mwambao wa pwani ya Afrika Mashariki inayotumiwa na watu wengi Afrika Mashariki na Kati kwa lahaja zake mbalimbali katika mawasiliano.

**Methali:** Semi fupi ya kimapokeo yenye muundo mahsusi na iliyo na fumbo fupi ambalo linapofasiliwa hupata maana mbalimbali kutegemea muktadha na hali ya maisha ya mtumiaji.

**Dhima chanya:** Kazi yenye manufaa kwa jamii ifanywayo na kipengele cha fasihi au kipashio cha lugha katika jamii.

**Dhima hasi:** Kazi isiyo manufaa kwa jamii ambayo kipengele cha fasihi au kipashio cha lugha kinaweza kuelekezwa na wanajamii wenye nia mbaya kutekeleza.

## YALIYOMO

|                                   |      |
|-----------------------------------|------|
| UNGAMO .....                      | ii   |
| TABARUKU .....                    | iii  |
| SHUKRANI.....                     | iv   |
| IKISIRI .....                     | vi   |
| UFAFANUZI WA ISTILAHU MUHIMU..... | vii  |
| YALIYOMO .....                    | viii |

## SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

|  |    |
|--|----|
| 1.0 Utangulizi .....                           | 1  |
| 1.1 Swala la Utafiti .....                     | 3  |
| 1.2 Maswali ya Utafiti .....                   | 5  |
| 1.3 Malengo ya Utafiti.....                    | 5  |
| 1.4 Sababu za Kuchagua Mada.....               | 5  |
| 1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti .....            | 7  |
| 1.6 Misingi ya Nadharia .....                  | 9  |
| 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada .....            | 15 |
| 1.8 Mbinu za Utafiti.....                      | 30 |
| 1.8.1 Uteuzi wa Sampuli.....                   | 31 |
| 1.8.3 Ukusanyaji wa Data.....                  | 32 |
| 1.8.4 Uchanganuzi wa Data.....                 | 33 |
| 1.8.5 Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti ..... | 33 |

## SURA YA PILI: MIKTADHA YA MATUMIZI YA METHALI

|   |    |
|---|----|
| 2.0 Utangulizi .....  | 34 |
| 2.1 Umuhimu wa ufahamu wa miktadha ya matumizi ya methali .....             | 34 |
| 2.2 Uibukaji na udhihirikaji wa dhima hasi katika methali za Kiswahili..... | 39 |
| 2.3 Sifa za kimiktadha za methali za Kiswahili.....                         | 47 |

|                     |    |
|---------------------|----|
| 2.4 Kiishilio ..... | 50 |
|---------------------|----|

**SURA YA TATU: UCHANGANUZI WA METHALI ZA KISWAHILI ZENYE  
DHIMA HASI**

|  |     |
|--|-----|
| 3.0 Utangulizi .....                                     | 52  |
| 3.1 Kanuni ya Kwanza; Kanuni ya Uzungumzaji .....        | 54  |
| 3.2 Kanuni ya Pili; Kanuni ya Ushirikiano.....           | 55  |
| 3.3 Aina za Methali Hasi .....                           | 57  |
| 3.3.1 Methali Kandamizi .....                            | 57  |
| 3.3.2 Methali Zinazochochea Vita, Fitina na Uhasama..... | 68  |
| 3.3.3 Methali za Vitisho .....                           | 71  |
| 3.3.4 Methali Zenye Taathira za Uovu .....               | 79  |
| 3.3.5 Methali Zinazodhihaki Ulemavu .....                | 90  |
| 3.3.6 Methali Zinazohujumu Sifa Njema .....              | 92  |
| 3.3.7 Methali Za Kukatisha Tamaa .....                   | 94  |
| 3.3.8 Methali Zinazohimiza Unyonge .....                 | 99  |
| 3.3.9 Methali Zenye Ubaguzi wa Kinasaba.....             | 104 |
| 3.3.10 Methali Zenye Ubaguzi wa Kiumri .....             | 108 |
| 3.3.11 Methali Zenye Ubaguzi wa Kiuana .....             | 109 |
| 3.3.12 Methali Zinazohimiza Ukabila .....                | 119 |
| 3.3.13 Methali Zenye Ubaguzi wa Kidini .....             | 120 |
| 3.4 Kiishilio .....                                      | 122 |

**SURA YA NNE: MANUFAA YA METHALI ZA KISWAHILI ZENYE DHIMA  
HASI KWA JAMII**

|   |     |
|---|-----|
| 4.0 Utangulizi .....                              | 123 |
| 4.1 Uchanya wa Methali Hasi.....                  | 124 |
| 4.1.1 Kusawiri Ukweli wa Maisha ya Mwanadamu..... | 125 |

|                           |     |
|---------------------------|-----|
| 4.1.2 Kutahadhari .....   | 127 |
| 4.1.3 Kutoa Mawaidha..... | 131 |
| 4.2 Kiishilio .....       | 136 |

**SURA YA TANO:HITIMISHO, MATOKEO NA MAPENDEKEZO**

|   |     |
|---|-----|
| 5.0 Utangulizi .....                      | 138 |
| 5.1 Hitimisho na Matokeo ya Utafiti ..... | 138 |
| 5.2 Mapendekezo.....                      | 142 |
| Marejeleo .....                           | 146 |
| KIAMBATISHO A .....                       | 151 |

## **SURA YA KWANZA**

### **UTANGULIZI**

#### **1.0 UTANGULIZI**

Utafiti huu umezichanganua methali za Kiswahili kwa kutumia mtazamo wa kiudenguzi. Kwa kufanya hivyo, dhima hasi ya methali za Kiswahili imeangaziwa na kufafanuliwa huku methali ikichukuliwa kama kipera cha fasihi simulizi na pia kipengele cha lugha ya mazungumzo.

Lugha yoyote ile hutumia vipashio vyake kama malighafi ya kuumba fani au tamathali tofauti za kuipamba lugha iyo hiyo. Lugha haiwezi kutenganishwa na mwanadamu kwa kuwa ndiye muumba wake. Hivyo, chochote kinachoathiri lugha kinamwathiri binadamu na kuweza kuingizwa katika lugha kunatokana na tajriba za binadamu. Hii ndio sababu Njogu na Chimera (1999) wameieleza fasihi ambayo pia inatokana na lugha kama aina ya sanaa inayotumia lugha kueleza tajriba za binadamu. Tamathali zozote za lugha zinazotumiwa katika jamii zikiwemo methali zinafaa kueleza au kusawiri tajriba za binadamu kwa njia chanya na isiyoleta hisia zozote hasi miongoni mwa wanajamii. Jakobson (1988) ameeleza kwamba, fasihi ni matumizi ya nguvu dhidi ya lugha ya kawaida kimakusudi. Kwa mantiki hii, fasihi huichukua lugha ya kawaida na kuifinyanga kiasi kwamba kitakachosemwa kwa lugha hiyo kitaleta mchomo zaidi ya lugha ya kawaida kiwe kizuri au kibaya.

Kila kipengele cha lugha huonyesha uhalisia wa jamii na humpa mwanalugha nafasi ya kuhisi na kujua jamii hiyo ilivyokuwa, ilivyo na itakavyokuwa kando na kusawiri imani

zake kuhusu maswala tofauti ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kidini. Ikiwa kipengele chochote cha lugha, zikiwemo methali, kitawasilishwa kwa kutumia lugha inayoleta maana zaidi ya moja hasa maana hasi ikiwemo, basi wanajamii wataathirika kwa njia nyingi kwa kuwa kipengele chochote cha lugha huwasiliana na hadhira ambayo ni mwanajamii.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), methali ni mojawapo wa tanzu za sanaa-jadiiya ambazo hutambuliwa haraka kutokana na lugha yake, muundo na yaliyomo. Muundo wa methali unaweza kutumia mbinu maalumu za lugha au za kishairi zinazochangia katika kukumbukika kwake. Kwa kuwa methali za Kiswahili hutumika katika mawasiliano, basi husimamia ujumbe mahsusi ingawa ujumbe huo hutolewa kwa njia ya muhtasari. Kabira na Mutahi (1988) wakifanyia utafiti methali za jamii ya Agikuyu wametoa ufafanuzi kwamba, methali hutokana na tukio maalum katika jamii wala si usemi unaotumika tu. Wanaendelea kutoa maelezo kuwa kila methali katika jamii inaaminika kutokana na tukio ambalo lilitendwa na watu ambao baadhi hutajwa kwa majina katika methali zenyewe huku wakitoa mfano wa methali ya Kikuyu “Ciakorire Wacu Mugunda” (Zilimpata Wacu shambani) ambapo Wacu ni jina la mwanamke katika jamii ya Agikuyu, miongoni mwa methali zingine. Hivyo, katika kivuli cha methali ambayo huwa kauli moja fupi tu huwa na kisa kirefu kinachoweza kutusaidia kuelewa asili ya baadhi ya maana zinazopatikana katika methali.

Hali ya methali kurejelea tukio la kijamii pia inafafanua kwa nini Methali nyingi katika jamii za Kiafrika Kiswahili kikiwemo ni mafumbo au jazanda ambazo huelekea kuwa na maana mbili; maana ya juu na maana ya ndani au batini. Maana ya juu ni maana

ipatikanayo kwa kufahamu maana ya maneno yaliyotumika na maana ya ndani ni ile iliyofichika inayopatikana tu kwa kuzielewa tamathali zilizotumiwa. Katika uchunguzi wa maana batini, uhasi wa maana za baadhi ya methali hujitokeza. Hata hivyo, baadhi ya methali huwa na maana ya juu tu.

Utafiti huu umechunguza jinsi baadhi ya methali za Kiswahili zilivyofaraguliwa katika kipindi fulani cha kihistoria hivi kwamba zinabeba ujumbe hasi kwa wanajamii ilihali methali zinafaa kuonya, kuadili, kurekebisha, kukosoa na kunasihi jamii miongoni mwa dhima zingine chanya. Utafiti huu haukuwa na lengo la kuonyesha kuwa methali zote za Kiswahili hazina dhima yoyote chanya na zinafaa kutupiliwa mbali. Kinyume chake, utafiti unalenga kuonyesha kuwa baadhi ya methali hizo zinabeba ujumbe usioweza kuifaa jamii katika miktadha fulani na hasa kwa wanajamii wasioelewa utamaduni na muktadha wa matumizi yake katika jamii ya Waswahili. Aidha, uchanganuzi wa matini kidenguzi pia hutegemea itikadi, miktadha na mazingira ya kitamaduni ambamo matini husika hutumika wala utofauti wa kimaana hautoki katika ombwe tupu. Kwa mfano methali *'Mkata hendi Mkele na angenda Mkele na kupakia jahazi mtele tele hurudi na upele'* ina dhima hasi ya kuwavunja maskini moyo ila kupata dhima hiyo mtumiaji anahitaji kujua sifa za mahali paitwapo Mkele na mfumo wa kiuchumi wa jamii ya Waswahili kihistoria.

### **1.1 SWALA LA UTAFITI**

Methali zimetafitiwa sana katika jamii nyingi na kwa mitazamo tofauti huku watafiti wengi wakifaulu kuonyesha kuwa kijumla methali kama kipengele cha lugha ni kiungo muhimu sana katika jamii. Mwandishi maarufu Achebe (1962) katika kitabu chake

*Things Fall Apart* kilichotafsiriwa kwa Kiswahili kama *Shujaa Okonkwo*, anazinasibisha methali na mafuta maarufu ya mnazi ambayo jamii ya Igbo inayathamini sana kwa kusema kwamba '*methali ni mafuta ambayo wazee husindikiza nayo maneno wanapozungumza*'. Kwa kusema hivi, Achebe anachora taswira ya umuhimu wa methali ambazo hujitokeza pia katika takriban kila jamii ya Kiafrika pamoja na kuonyesha hadhi yake. Miongoni mwa jamii hizo, methali huthaminiwa sana na ndicho kiperu pekee ambacho kimetengewa watu waliopevuka kiumri na ambacho hutumiwa kila wakati panapo haja bila kutengewa wakati mahususi. Katika maongezi ya jamii za Kiafrika, anayetumia methali kwa wingi zaidi ndiye anayechukuliwa kuwa mlumbi. Kwa sababu ya umuhimu wa methali katika lugha, kila mwanajamii hujitahidi kufahamu maana ya methali za jamii yake na wakati mwingine hata maana ya methali za jamii zingine. Hivyo, matumizi na maana ya methali wakati mwingine husambaa katika jamii kiasi kwamba asilimia kubwa ya jamii inaifahamu maana ya methali inayohusika.

Watafiti wengi wametafiti methali kwa dhana ya kijumla kuwa methali zote za Kiswahili zina uchanya wa moja kwa moja na hivyo manufaa ya moja kwa moja kwa watumiaji wake. Utafiti huu kinyume na tafiti zingine kama vile Ndungo (1998), Maitaria (1991) na (2012), na Gitau (2008), umeleta uchanganuzi wa methali ambao unalenga kuonyesha sura fiche za baadhi ya methali za Kiswahili ambazo zina uhasi. Uhasi hapa una maana kuwa methali husika hazina manufaa kwa jamii katika muktadha fulani kwa kuwa ujumbe wake unalenga ama kuwavunja moyo baadhi ya wanajamii, kuwachochea kuzua fitina, kuwafanya kuridhika na hali zao duni, kuwagawa kitabaka na kadhalika. Hata hivyo, jambo hili haliwezi kuhalalisha kutupiliwa mbali kwa methali za Kiswahili kwa sababu, kuna methali zingine nyingi za Kiswahili ambazo zina dhima chanya na pia kwa

mtazamo tofauti methali zizi hizi zenye dhima hasi zinaweza kuonyesha uchanya wake. Umuhimu wa utafiti huu hauko tu katika kuonyesha dhima hasi katika methali za Kiswahili bali pia kuonyesha utelezi wa maana za kimatini hivi kwamba zinaonyesha dhima chanya kwa mtazamo au muktadha mmoja na dhima hasi katika muktadha mwingine.

## **1.2 MASWALI YA UTAFITI**

Utafiti huu umeongozwa na maswali yafuatayo:

- a) Methali hasi za Kiswahili hutumika katika miktadha gani?
- b) Methali hasi za Kiswahili hubainika kwa njia zipi?
- c) Methali hasi za Kiswahili zina manufaa gani kwa jamii?

## **1.3 MALENGO YA UTAFITI**

- (a) Kutambua miktadha ya matumizi ya methali hasi za Kiswahili.
- (b) Kuziainisha methali hasi za Kiswahili kutegemea uhasi wake.
- (c) Kutambua manufaa ya methali hasi za Kiswahili kwa jamii.

## **1.4 SABABU ZA KUCHAGUA MADA**

Methali ni kiungo muhimu sana cha lugha na mawasiliano katika jamii na tamathali ya lugha inayochukuliwa kwa umakini zaidi katika jamii. Umuhimu huu unatokana hasa na hali kuwa, methali zinatumiwa sana na watu waliopevuka kiumri katika maswala mazito yanayogusia maisha ya wanajamii kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kwa mujibu wa Miruka

(1994), jamii ndio mama wa utamaduni na utamaduni nao umegawika katika aina mbili ambapo utangamano wa kijamii ni mojawapo ya aina zake. Mojawapo ya vipengee vinavyounda utangamano wa kijamii ni lugha, na methali ni kipengee muhimu sana cha lugha kinachosaidia kuboresha mawasiliano au kuyafanikisha hasa zinapotumika kisanaa.

Nandwa na Bukenya (1983) nao wametaarifu kuwa methali ni uti wa mgongo wa tanzu zingine zote za fasihi simulizi ya Afrika kwa sababu takriban wasanii wote wakiwemo waimbaji, watambaji, walumbi, manju na hata malenga huzitumia katika kuufanikisha usanii wao pamoja na kuurembesha. Wahakiki wa awali kama vile Knappert (1979) kwa mfano wamedai kwamba kilichowapa washairi wa Kiswahili ari ya kutunga mashairi ilikuwa kuwepo kwa wingi wa methali katika fasihi simulizi ya jamii ya Waswahili.

Methali ni miongoni mwa tamathali za lugha zilizoachiwa watu wazima hasa wazee na zinazosibishwa na waanzilishi wa jamii husika. Hii ndio sababu kabla ya methali kutajwa, vitangulizi kama vile; *wazee wetu wa kale walisema kwamba... chambilecho wazee wetu... wahenga hawakukosea waliponena...* hutajwa. Methali ni kipengele chenye utajiri mkubwa wa busara, hekima na mawaidha.

Hata hivyo, imebainishwa na baadhi ya watafiti kama vile Ndungo (1998) kwamba baadhi ya methali zimebeba dhima hasi kwa jamii japo alijihusisha tu na methali zinazomdhalilisha mwanamke katika jamii za Agikuyu na Waswahili. Kwa hivyo, utafiti huu ulichaguliwa kwa sababu ya kuonyesha nyufa zaidi zilizoko katika dhima ya methali za Kiswahili kwa kuonyesha uhasi wake na kuufafanua kwa undani. Imebainika kwamba, baadhi ya methali hizi hupotosha, kudhalilisha, kuchochea uovu, fitina na vita na hata

kuwavunja moyo wanyonge kwa kuwaonyesha kwamba hawawezi kujikwamua kutoka hali zao duni.

Utafiti huu umetoa mchango katika taaluma ya lugha kwa kuizindua jamii ili iweze kutafakari ufaafu wa baadhi ya methali wanazotumia katika maongezi yao ya kila siku pamoja na kufahamu maana fiche zinazobebwa na methali hizo, katika miktadha fulani, ambazo hawakuzidhania. Pia, utafiti huu ni msingi wa kufanya utafiti zaidi na kuvidengua vipengele vingine vya lugha ya Kiswahili, ili kubaini ikiwa maana vinazosemekana kuwa nazo ndizo za pekee zinazopatikana katika vipengele hivyo au mtazamo tofauti unaweza kuzua maana zingine tofauti; chanya au hasi. Jambo hili linaegemea wazo la Mbaabu (1996) kuwa kwa sasa lugha ya Kiswahili si ya wanajamii wa pwani ya Afrika Mashariki pekee bali imesambaa na kushamiri katika eneo nzima la Afrika Mashariki na kati. Isitoshe, utafiti huu ulichaguliwa kwa kuwa, data za kutosha zipo katika kamusi nyingi za methali zilizoandikwa na wasomi mbalimbali na kuchapishwa. Kwa mujibu wa Norrick (1985) hiki ni kigezo muhimu sana cha kutiliwa maanani kabla ya kuzifanyia utafiti wa aina yoyote methali au matini zingine za aina yoyote katika jamii.

### **1.5 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI**

Methali zimekuwepo katika lugha ya jamii nyingi za Afrika na zimekuwa zikitumika katika uboreshaji wa mazungumzo na uwasilishaji wa hoja nzito katika jamii hususan na wazee. Asili ya methali hasa haiwezi kuwekewa kipindi au wakati maalum katika historia ya jamii kwa sababu zimekuwa zikitumika tangu miaka na mikaka na ni vigumu kutoa

uamuzi wa hasa zilianza kutumiwa na nani au nani alizitunga. Hili si swala la methali za Kiswahili pekee bali methali za lugha zote za Afrika.

Katika Kiswahili kuna methali za aina nyingi zikiwemo zile zinazotoa mawaidha, zinazoonya na zinazoadilisha jamii. Hata hivyo, utafiti huu umejikita tu katika methali ambazo zinabeba dhima hasi kwa wanajamii; inayoambatana na dhima nyingine ambayo inaweza kuwa chanya au ndiyo dhima ya pekee katika methali husika. Msokile (1993) amefafanua kwamba mojawapo ya madhumuni ya wahakiki, kufanya uhakiki, ni kuvichambua vipengele wanavyoshughulikia ili kujua misingi ya ubunifu wake na kutambua thamani pamoja na kuvihukumu kwa kuzingatia misingi maalumu ya uhakiki iliyokwisha wekwa. Hivyo, utafiti huu ulijikita hasa katika kuchunguza na kuamua ni methali zipi za Kiswahili zina dhima hasi na uhasi huo unajitokeza vipi jambo ambalo limefanywa kwa kutumia vigezo maalum vilivyowekwa katika nadharia ya Udenguzi iliyoteuliwa kuongoza utafiti.

Methali za Kiswahili tu ndizo zilizochanganuliwa katika utafiti huu na zilichaguliwa kwa sababu methali hizo zimeandikwa katika kamusi nyingi za methali zikiwemo ile ya Abudu na Baruwa (1981), Karama na Saidi (1983), Ndalú (1989), Wamitila (2001), Andambi na Muroño (2005), Waihiga na Kagwa (2007) na Kinge'i na Ndalú (2008).

Isitoshe, methali za Kiswahili ziliteuliwa kwa sababu zinajulikana na hutumika na watu wengi kote Afrika Mashariki na Kati na kwa sasa ambapo Kiswahili kinaenea kote ulimwenguni kupitia elimu na teknolojia ya mawasiliano (Lioba, 2006) methali hizi zitasambaa kote ulimwenguni na kutumika na hadhira pana zaidi. Hata hivyo, si methali

zote za Kiswahili zimeshughulikiwa bali tu zile zilizoambatishwa katika tasnifu hii (Kiambatisho A).

## 1.6 MISINGI YA NADHARIA

Utafiti huu ulitumia nadharia ya Udenguzi. Nadharia hii ilichaguliwa kwa kuzingatia kuwa methali ni kiungo muhimu sana katika lugha ya jamii, hivyo ni vyema kuchunguza maana zake mbalimbali zinazoweza kuibuka kufuatia miktadha ya matumizi badala ya kutegemea tu maana za kawaida zilizoandikwa katika kamusi za methali. Kutokana na kusoma tafiti zingine zilizotumia nadharia hii kwa mfano Ng'etich (2012) aliyetumia nadharia ya Udenguzi kuchambua lugha ya wahubiri, mtafiti aligundua kuwa nadharia hii ina uwezo wa kuendeleza kazi nzima kitaalamu.

Kimsingi, nadharia ya udenguzi ni mkabala wa kiuhakiki unaopinga mtazamo kwamba kazi ya kifasisihi ina kitovu kimoja cha kimaana (Goring, 2001). Mwasisi wa nadharia hii ni mwanafalsafa wa Kifaransa kwa jina Jacques Derrida. Derrida alichapisha vitabu vitatu katika mwaka wa 1967 ambavyo ni: *Writing and Difference*, *Speech and Phenomena na Of Grammatology* ambapo amesisitiza kuwa maandishi ni muhimu kuliko usemi, madai ambayo ni kinyume na yale ya mtangulizi wake Ferdinand de Saussure aliyesisitiza kwamba usemi ndio muhimu (Derrida, 1976).

Derrida alikuwa anaendeleza fikra za watangulizi wake Hegel, Freud, Heidegger na Husserl. Wanafalsafa hawa wameeleza kuwa lugha ikitazamwa kwa undani inaonekana kuwa na uwezo wa kujifafanua. Udenguzi hujishughulisha na kuangalia namna lugha na maana zinavyoingiliana na kufanya kazi kwa pamoja. Pia, udenguzi ni juhudi ya kuelewa

muundo wa ujuzi na maarifa ya kijamii. Kwa mujibu wa nadharia hii, ujuzi na maarifa si vitu vinavyoweza kueleweka moja kwa moja bali ujuzi ni kitu kisichoshikika, chenye utelezi na kinachodumu katika ukinzani wa lugha na unakidi. Utelezi wa nadharia hii ni kielelezo cha utelezi wa ujuzi na maarifa. Udenguzi huzama kwenye ufafanuzi wa matini na kuyatazama kwa jicho la ndani kwa kuyadengua na kuyabomoa. Nadharia hii inadai kuwa uelewaji wa matini unaweza kutupa mwanga kamili kuhusu jamii, na kwamba si muhimu tuangalie muktadha wake. Udenguzi unaweza kutajika kijumla kama unakidi wa lugha kama chombo cha mawasiliano chenye utata na uwezo wa kujifafanua hasa katika maandishi. Uchambuzi wa kiudenguzi husaidia katika kuweka wazi ukinzani wa matini mbalimbali.

Isitoshe, udenguzi unapinga ugawaji wa hali mbili au zaidi zinazokinzana (kama vile juu na chini, -nene na -embamba, -fupi na -refu) na kuonyesha kuwa kuna uwezekano wa hali hizo kuwa pamoja na kuchangiana kimaana. Udenguzi ni juhudi za kufikia nguvu na uwezo wa matini kama chombo kinachoweza kujifafanua. Kwa mujibu wa Derrida, kuna mvutano wa daima kati ya vinyume, ambao huacha kovu lisilofutika. Mvutano huu unaweza kuelezewa zaidi kama uliopo kati ya 'kuwepo' na 'kutokuwepo' na maana hujibainisha katika kijinafasa kidogo katika kovu hilo. Nadharia hii inachukulia kuwa matini huwa na maana mbalimbali zinazokinzana; inafundua kuwa lugha inaweza kufasiriwa kwa zaidi ya njia moja na kutoa maana tofauti katika kila njia maana zingine ambazo ni kinyume au zinazokinzana.

Wadenguzi huamini kwamba, kwenye vinyume ndiko kwenye maingiliano. Wao hujiuliza ikiwa vinyume vilivyoko kwenye matini vinaingiliana kwa njia gani, vinatianaje

nguvu na maingiliano yake yanajidhihirishaje katika lugha. Kwa njia hii, udenguzi huingilia matini kati na kuihakiki ndani kwa kuipeperusha, kuipindapinda na kuonyesha uwezekano wa kutokuwa na vidato vya kinyume. Kulingana na wadenguzi haiwezekani kuifasiri matini kwa maana moja tu. Matini huwa na maana mbalimbali ambazo hutofautiana. Udenguzi ni uhakiki wa matini ambao huonyesha kuwa lugha haina maana inayodumu na hatuwezi kubainisha wazi tunachomaanisha. Matini haiwezi kumpa msomaji maana moja kwa kuwa lugha yenyewe huwa na utata. Hata hivyo, lengo la wadenguzi ni kuvunja tofauti za kimaana. Wanafalsafa hawa hutumia sana mabano katika maandishi yao, wanapofafanua hoja zao, kuonyesha uwezekano wa vinyume kuingiliana. Kwa mfano, neno 'hakuna' linaweza kuendelezwa '(ha)kuna' kuonyesha kuwa dhana za 'hakuna' na 'kuna' ni dhana zinazoingiliana na ndani ya 'hakuna' kuna 'kuna' huku ndani ya 'kuna' kukiwa na 'hakuna' hali kadhalika.

Eagleton (1983) naye ametaarifu kuwa maana ya ishara huwa imesambazwa kwenye viashiria vingi. Maana haipatikani katika ishara moja pekee lakini huwa katika hali ya kuwepo na kutokuwepo. Yaani maana ya matini huwa imeahirishwa na kiashiria kimoja humwelekeza mhakiki kwa kiashiria kingine. Maana za awali huumbwa upya na maana za baadaye. Ingawa sentensi inaweza kufikia kikomo, hatua za lugha haziwezi kwa kuwa maana haipatikani tu katika uunganishaji wa maneno kuunda sentensi bali lazima vipashio vyake vihusiane katika kujenga maana ili sentensi husika ilete maana. Maana haipatikani moja kwa moja katika ishara kwa sababu maana ya ishara ni kile ambacho ishara hiyo siyo. Hivyo, maana ya ishara huwa haipo kwenye ishara husika. Maana ya matini huwa imetawanyika katika mfululizo wa viashiria wala haipatikani kwa ukamilifu katika ishara moja pekee. Kwa mujibu wa Cuddon (1991), Udenguzi unahusu njia

mahsusi ya usomaji na mbinu ya uhakiki na uchanganuzi chunguzi. Anafafanua kuwa kudengua si mambo na kubomoa bali unakaribiana sana na maana ya kietimolojia ya kuchanganua ambayo ni kutendua. Matini inapodenguliwa haiharibiwi bali dhana kwamba matini hiyo ina maana moja maalumu ndiyo huharibiwa.

Derrida (1976) anafafanua kuwa, mdenguzi huchunguza ni kwa njia gani maana moja inapendelewa katika matini au mjadala. Maana moja inaweza kupendelewa kwa kuchukuliwa kuwa ya kipekee, iliyojitenga, yenye ukweli, yenye thamani, yenye umuhimu au yenye ujumla zaidi ya vinyume vyake. Hata hivyo, kwa kuwa vitu vinaweza kuwa na zaidi ya kinyume kimoja maana nyingi zinaweza kupendelewa kwa wakati mmoja. Mdenguzi anaweza kuangalia maneno msingi yenye zaidi ya maana moja, etimolojia ya mahusiano ya maneno au kejeli na ucheshi kuonyesha ni vipi matini hiyo inavyotoa maana nyingi na kinzani (Balkin, 1990). Balkin ameendelea kutoa ufafanuzi kuwa udenguzi hauonyeshi kwamba matini hazina maana yoyote bali huonyesha kuwa matini zina maana nyingi ambazo wakati mwingine hata huwa kinzani. Kwa wakati uo huo, udenguzi hauonyeshi kuwa maana za matini hazina mipaka bali kwamba mipaka yake inaweza kusongezwa kwa njia kadha hasa matini hizo zinapowekwa katika miktadha mipya ya uchunguzi. Kwa mujibu wa Derrida (1976), matini zinapowekwa katika miktadha mipya huendelea kuzalisha maana mpya ambazo zinatofautiana lakini kwa wakati huo zinazowiana na maana za hapo awali. Hivyo, upinzani kati ya maana hizo hutokea. Wadenguzi wanaamini hakuna toleo la mwisho la matini hasa kazi ya fasihi. Hii ndio sababu inayowafanya wahakiki kutoa fasiri tofauti za jambo moja baadhi yazo zinazokinzana maadamu wana ushahidi wa kutosha (Wafula na Njogu, 2007). Wahakiki wengine waliosaidiana na Derrida katika kuikuza na kuijenga nadharia hii

wakiwemo Pual de Mann, Joseph Hilis Miller, Geoffrey Hartman na Harold Bloom wamedai kuwa kuna uwezekano wa fasiri mbili za kazi za matini zisizolingana kamwe kuingiliana. Hata hivyo, fasiri zote mbili zinaweza kukubalika kimaana.

Barthes (1977), ametoa maelezo zaidi kuhusu nadharia ya Udenguzi ambapo analenga Udenguzi katika matini andishi. Barthes ameeleza kuwa baada ya mwandishi kuandika kazi yake, wajibu wake na jukumu lake huishia papo hapo. Mwandishi huyo 'hufa' huku msomaji 'hufufuka' kwa kuwa ndiye muhimu katika uamuzi wa maana ya matini husika. Kazi yake huchukua uhai wake yenyewe usiohusiana na mtunzi. Hivyo, mtunzi hana mchango wowote katika kuelekeza mkondo au mtazamo wa uhakiki wala kubainisha maana zitokanazo na kazi yake. Kiini asilia cha mwandishi kuandika kazi husika nacho hakiathiri maana za msomaji wala mhakiki kwa vyovyote. Kilicho muhimu tokea hapo ni mhakiki na maandishi, pamoja na fasiri anazozipata kutokana na mantiki itokanayo na muktadha wa jamii na uelewa wake. Kazi inayohakikiwa basi ina maana yenyewe na kuna uwezekano wa fasiri nyingi kutolewa kwa kazi moja kutegemea wasomaji na wahakiki wa kazi hiyo.

Fauka ya hayo, Udenguzi ni uhakiki unaojikita katika matini kama chombo kinachojitosheleza na kinachoweza kufichua maana bila kurejelea muktadha kama alivyodai Derrida (1967), japo waitifaki wa baadaye kama Belsey (1983) waliongeza kuwa muktadha unapaswa kurejelewa ili matini iwe na maana kwa jamii.

Miongoni mwa mihimili mingi ya nadharia ya Udenguzi mihimili ifuatayo imezingatiwa katika kazi hii;

- i) Matini huwa na maana nyingi zinazokinzana – mhimili huu umesaidia kudengua methali ambazo kwa upande mmoja zinaonekana kuwa na dhima chanya lakini kwa mtazamo tofauti zinaonyesha dhima hasi.
- ii) Matini inaweza kufasiriwa kwa zaidi ya njia moja na kutoa maana tofauti katika kila ufasiri. Wahakiki huweza kutoa fasiri tofauti za matini moja baadhi zinazokinzana mradi wana ushahidi wa kutosha – mhimili huu umeshirikiana na mhimili wa kwanza kutoa ushahidi wa kuwepo kwa dhima hasi katika methali teule ambazo zinakinzana na dhima chanya zilizozoeleka.
- iii) Maana haipatikani katika ishara moja pekee bali huwa katika hali ya kuwepo na kutokuwepo – mhimili huu umetumika kuonyesha kuwa uhasi wa methali haupatikani tu katika inachotaja bali katika isichotaja pia.

Nadharia hii imefaa sana katika utafiti huu hususan katika kufafanua undani wa methali, baadhi ambazo hutumika kila siku katika maandishi na maongezi, na kuonyesha kuwa baadhi zina maana zingine fiche ambazo ni hasi. Pia, nadharia ya Udenguzi imeusaidia utafiti huu katika kuzidengua methali na kuonyesha baadhi ya vipengele jenzi ambavyo havikutiliwa maanani na wahakiki wa methali wa awali na ambavyo ndivyo hubeba dhima hasi iliyokuwa ikichunguzwa katika utafiti.

## 1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Waandishi wengi wamejishughulisha na utafiti pamoja na uandishi kuzihusu methali za Kiswahili na za lugha zingine za Kiafrika. Watafiti hao wametafiti kwa mikabala mbalimbali na kuibua dhana kadha kuzihusu methali za jamii fulani muhsusi na pia jamii za Kiafrika kwa jumla.

Chesaina (1997) akizitafiti methali za jamii za Embu na Mbeere amefafanua kuwa, methali ndicho kipera kinachokaribiana na nyimbo katika wingi wa hekima na busara. Upekee wa methali unapatikana katika uwezo wake wa kuwasilisha ujumbe kwa ukali huku zikitumia maneno machache iwezekanavyo. Kinyume na utafiti wa Chesaina uliochunguza methali kama kipengele cha fasihi simulizi, utafiti huu umeangalia methali kama kipengele cha lugha bila kuzihusisha na matini nyingine yoyote ile na umezitaftiti methali za Kiswahili pekee.

Lazima methali zifasiriwe kabla ya maana yake kufahamika kikamilifu. Mawazo haya ni kwa mujibu wa Odaga (1984) anayeendelea kuongeza kuwa kila kundi la watu lina methali zake wanazozitumia katika mawasiliano yao ya kila siku na kama zilivyo tungo zingine za fasihi simulizi methali hugusia kila dhana ya maisha ya watu kama vile siasa, elimu, dini, na uchumi. Kuna baadhi ya methali ambazo zimerithishwa kizazi baada ya kizazi tangu zamani na kuna zile ambazo zimeundwa kutokana na tajriba za jamii katika miaka ya hivi maajuzi. Methali husheheni falsafa ya wanajamii pamoja na busara yao na kutokana nazo tunaweza kujua mwonoulimwengu wa watu hao pamoja na historia yao. Kama ilivyo katika utafiti huu Odaga ana maoni kuwa methali hutokana na tajriba za

wanajamii hivyo kufanya maana na dhima za methali kuwa tegemezi kwa miktadha ya jamii husika.

Methali kama misemo ya hekima na busara hubuniwa na wanajamii ili kuwawezesha kuwasiliana vizuri na pia huwawezesha watu wanaozungumza au kuandika kufafanua ujumbe wanaozungumzia. Hali kadhalika, methali huwa na mafumbo fulani na huashiria ukweli fulani ambao wanajamii huwa wameuona katika maisha yao. Japo methali zinaweza kufasiriwa kwa njia mbili; maana ya juu na fiche, maana ya juu aghalabu huwa si muhimu bali fasiri muhimu zaidi ni maana ya ndani (Ngugi na Musau, 1999). Wataalamu hawa wamezichukulia methali kama kipengele cha lugha kama ilivyo katika utafiti huu.

Knappert (1979) akiangazia *Methali kama chanzo cha ushairi wa Kiswahili* anadai kuwa labda chanzo kikubwa cha washairi wa kale wa Kiswahili kupata ilhamu ya kuandika ni kuwepo kwa hazina kubwa ya methali za Kiswahili zilizokuwa hazina ya fasihi simulizi ya jamii iliyofichika bongoni mwa wazee. Methali za Kiswahili zinapatikana katika tenzi za karne ya kumi na nane na inaonekana kwamba waliozitunga methali zamani kabla ya tenzi za Kiswahili kuwepo walifanya hivyo kwa njia ya kishairi na yenye mahadhi. Hata hivyo, ni vigumu kutoa uamuzi wa ikiwa watunzi wa tenzi walijiundia methali walizotumia au walitumia methali ambazo zilikuwepo katika fasihi simulizi ya jamii tayari. Japo Knappert alitafiti methali za Kiswahili, alifanya hivyo kwa kuangalia mchango wake katika uandishi hasa wa mashairi kinyume na utafiti huu ambao uliziangalia kama kipengele cha lugha na fasihi simulizi kinachoweza kujisimamia kivyake.

Methali ni semi za kiistiari zinazorejelea muktadha wa kijamii, tukio au tajriba ya kijamii kwa kifupi. Methali hutumika hasa kuonya, kunasihi, kufahamisha na kufafanua miongoni mwa dhima zingine na hutumika katika maswala mazito kama majadiliano kuhusu ardhi, ndoa au kesi. Katika miktadha kama hii, methali zinazotolewa hazifasiriwi. Aidha, lazima mwanajamii awe na hazina kubwa ya methali za lugha yake ili aweze kuzitumia katika miktadha tofauti ya maisha ya kila siku kwa kuwa methali hutegemea uwezo wa mtumiaji kuzitumia ipasavyo. Pia, kwa kuwa methali zimefumana na utamaduni wa jamii lazima mtumiaji aelewe miktadha ya kitamaduni ili aweze kukumbatia maana na dhima ya methali ipasavyo. Mawazo haya ni kwa mujibu wa Kabira na Mutahi (1988) waliozitifiti methali za Wakikuyu. Japo utafiti huu umeshughulikia methali za Kiswahili pekee unashiriki maoni sawa na ya watafiti hawa katika kauli kuwa methali kama misemo ya kiistiari hurejelea tukio la kijamii kwa kifupi.

Madumulla (1995) akitafiti methali za Wahehe ametoa ufafanuzi kuwa, methali ni utanzu wa kisanaa ambao umekuwa ukitumiwa na jamii tangu kale kueleza uelewa wa watu kuhusu mazingira yao kwa njia wazi na dhahania. Kwa maoni ya Madumulla hata methali zinazopatikana katika Bibilia Takatifu na zinazodaiwa kuandikwa na mwanafalsafa Suleiman zinafaa kuangaliwa kama methali za kizazi cha wakati huo zilizokusanywa na Suleiman kutokana na busara yake na asili yake ya kifalme. Kwa mantiki hii, methali zinawakilisha sauti ya nafsi ya kijumla isiyojulikana, inayotokana na busara ya binadamu japo jambo hili halimaanishi kwa vyovyote kuwa wakati fulani katika historia ya jamii kulikuwa na kundi la watu waliokuwa wakitunga methali. Kinyume chake ni kuwa, wakati fulani, mahali fulani na katika muktadha fulani wa

kijamii mtu fulani alitoa usemi kwa njia ya mdomo au maandishi ambao ulikuja kukubalika na jamii na ukasambazwa kama methali.

Wescott (1981) naye amesherehi kuwa methali zilitungwa kabla ya tenzi lakini baada ya vitendawili. Ametaja kuwa vitendawili vilitungwa takriban miaka 15,000 iliyopita, methali zikatungwa miaka 10,000 iliyopita nazo tenzi zikaja miaka 5,000 iliyopita. Hata hivyo, amesema kuwa tarehe hizi ni dhahania tu na kuwapa watafiti wengine changamoto ya kufanya utafiti zaidi. Akitoa dhibitisho ya tarehe hizi dhahania, Madumulla anasema kuwa kutokana na ufupi na sifa za ushairi za methali inaweza kufahamika kwamba methali ziliibuka baada ya tanzu zingine kama nyimbo; kama masalio yake baada ya nyimbo hizo kupotea. Zinaweza kuwa zilitokana pia na mbazi, hekaya au ngano. Si methali zote ziliibuka kwa njia hii hata hivyo. Isitoshe, Culler (1975) ameeleza kuwa ni jambo la kibatili kujaribu kutafuta kisahih mwanzilishi wa methali yoyote ile. Utafiti huu haukujikita katika swala la historia ya methali kiwakati bali umechunguza tu dhima zake hasi katika miktadha mbalimbali.

Suala la umapokeo ni muhimu sana katika taaluma ya methali (Wamitila, 2003). Methali hupokezanwa katika jamii na mtu anayeitumia ama kuelekeza, kushauri, kuamua, kunasihi au kukosoa hutegemea uwezo wa methali wa kimapokeo. Ikiwa tukio la kijamii lililoibua methali hiyo lilikuwa hasi hata hivyo uwezo wake wa kimapokeo utakuwa hasi na dhima yake katika jamii itakuwa hasi. Wamitila ameziainisha methali kwa kutumia vigezo vya abjadi, muktadha, uamilifu, muundo, maana na sarufi. Ameendelea kueleza kuwa zipo methali zinazoweza kutajwa kama methali-bia; yaani methali ambazo haziwezi kufungwa katika jamii moja na zinazoonekana kama zilitafsiriwa kutoka jamii

moja hadi nyingine. Wamitila alikuwa akiziangalia methali za jamii kadha kwa pamoja na hakutaja kuwa methali inaweza kuwa na dhima hasi.

Kinoti (2008) amesema kuwa methali hupitisha ujumbe wake kwa kufumba na kupigia mfano jambo fulani na zinatajika kama maneno ya wahenga kwa sababu ni mali na amali ya jamii. Kwa mujibu wa utafiti huu methali hazipigii mfano jambo fulani tu bali ni kiwakilishi cha tukio la kweli lililoifaa au kuiumiza jamii.

Andambi na Muroso (2005) nao wametumia mpangilio wa methali za Kiswahili ambao ni tofauti kabisa na wa watangulizi wao ambao walizipanga kiabjadi. Mpangilio wa Andambi na Muroso umezingatia makundi ya methali. Makundi ya methali waliyo nayo ni kama methali zinazohusu sehemu za mwili, wanyama, wadudu, ndege, vifaa vya nyumbani, falaki na nyakati, mimea, vyombo vya majini na kadhalika. Hata hivyo, wataalamu hawa hawakuwatajia wasomaji kuwa baadhi ya methali zinaweza kuangukia zaidi ya kitengo kimoja. Nia ya utafiti huu haikuwa kuzikusanya methali na kuzipanga kwa mpangilio wowote bali kuchanganua chache zilizoteuliwa japo baadhi ya methali teule zimeteuliwa kutoka kwa kamusi ya Andambi na Muroso.

Waihiga na Kagwa (2007) wakieleza umuhimu wa methali wana maoni kuwa fasihi haikamiliki bila methali. Pia methali hazitumiki katika fasihi simulizi pekee bali na fasihi andishi kwa kuwa kwa mfano zinatumiwa na wanafunzi wanapoandika insha na pia waandishi katika uandishi wa riwaya, tamthilia, hadithi fupi na hata mashairi. Kitabu cha fasihi chenye uhaba wa methali huonekana chapwa na chenye upungufu wa mbinu za lugha. Kwa upande mwingine mwandishi yeyote anayetumia methali ipasavyo hudhihirisha busara na ujuzi wa lugha na hufanya kazi yake iwe ya kipekee na yenye

mvuto wa hali yake kwa hadhira. Athari sawa na hii huonekana kwa mzungumzaji anayetumia wingi wa methali kwa njia mwafaka katika mazungumzo yake. Katika kueleza muundo wa methali wataalamu hawa wanataja kuwa baadhi ya methali za Kiswahili hazitumii lugha sanifu ya Kiswahili jambo linaloonyesha kuwa zilitokana na lahaja mbalimbali za Kiswahili. Mfano wa methali hizi ni kama '*Mchama ago hanyeli huenda akauya papo*' na '*Mwendo kikuongonga mawe mtapike.*' Katika maelezo haya wataalamu hawa wamejikita zaidi katika methali kama kipera cha fasihi simulizi na kipengele cha fasihi andishi japo pia wamegusia swala la methali kama kipengele cha lugha (mazungumzo) ambao ndio mwelekeo wa utafiti huu.

Mazrui na Syambo (1992) nao wanatoa ufasili kuwa methali hudhihirisha mkusanyiko wa mafunzo waliyopata watu wa vizazi vingi vya jumuiya fulani katika maisha yao, na ni sehemu ya lugha inayobaini falsafa ya watu fulani kuhusu maisha kwa jumla. Ni muhimu kutaja hapa kuwa japo methali hutoa mafunzo kwa wanajamii si methali zote zilizotolewa kwa njia ya mafunzo bali nyingi zilitumika kabla ya kuamuliwa kwamba kuna mafunzo ndani yake na kuna baadhi ambazo hazibebi mafunzo yanayoweza kuifaa jamii hasa katika miktadha fulani.

Methali ni tamko lenye kueleza wazo la busara la binadamu kwa ufupi. Pia ni muhtasari wa wazo la busara kwa mkato. Methali nyingi zinatokana na kufungamana moja kwa moja na mashairi. Katika ufupi wake, mwaweza kupatikana takriri, vina, mizani, na tanakali za sauti mumo kwa mumo zikiwa katika idadi sawa na zile zipatikanazo katika mishororo ya mashairi Njogu na Chimerah (1999). Kwa mfano, methali yaweza kuwa na mizani kumi na sita iliyogawanyika katikati katika idadi sawa katika ukwapi na utao;

yaani nane nane katika kila kipande. Kwa mfano, *Pole pole, (mizani 8) ndio mwendo, (mizani 8)*. Sifa hii ya methali inaweza kutumiwa kudhibitisha mawazo ya Wescott yaliyotolewa awali kuwa methali zilitokana na vitanzu vingine kama nyimbo, mashairi simulizi, hekaya na ngano. Hata hivyo, si methali zote zenye mpangilio huu. Utafiti huu haukujikita katika sifa za nje za methali bali ujumbe ulio katika maana fiche.

Vansina (1985) ameeleza kuwa methali zinapatikana katika kundi la tungo za fasihi simulizi ambazo hazihitaji ama maneno mahsusi au muundo mahsusi wa kiisimu katika utunzi wake. Muundo wowote unaogonga hoja iliyokusudiwa kwa umakini zaidi huwa sawa. Kichocheo cha uundaji wa methali na misemo katika jamii hasa hakijulikani kwa kuwa zinaonekana kuibuka kwa njia sawa tu na istiari ambapo zinaanza kutumika kama semi za kawaida kisha kukubalika na kusambaa kama methali. Methali zaweza kuwa za kale au za kisasa. Hata hivyo ni vigumu kutoa kijelezi kitakachotosheleza uamuzi wa ni methali ipi ya kale na ni ipi ya kisasa. Akigusia swala la maana Vansina anatoa ufafanuzi kuwa kuna maana mbili za kazi yoyote ile; maana asili/ maana iliyokusudiwa na maana wasilishwa au maana inayojitokeza. Maana hizi mbili wakati mwingine huwa kinyume jambo linalosababishwa na matumizi ya istiari na jazanda. Maana hizi mbili anazotaja Vansina ndizo zinazosababisha methali nyingi kuwa na dhima hasi wala si kwamba nyingi za methali hizo ziliundwa kwa lengo la kuwasilisha dhima hiyo.

Nandwa na Bukenya (1983) nao wametoa ufafanuzi kuwa methali zina sifa ya matumizi mahsusi hivi kwamba zitaleta maana tu ikiwa zitatumika katika muktadha na hali fulani maalumu. Mawazo sawa na haya yametolewa na wasomi wengine kama Arewa na Dundes (1964), Anozie (1981) na Finnegan (1970). Japo methali zina falsafa ndani yake

hazina uwezo wa kuchunguza ukweli na kutoa uamuzi wa kudumu daima. Umuhimu wa methali umejikita katika matumizi yake katika tukio au hali moja maalumu; hivyo, ni jambo lisiloweza kuzaa matunda yoyote kujaribu kufasiri methali nje ya muktadha wake. Wakati mwingine baadhi ya methali huweza kufasiriwa kwa zaidi ya njia moja lakini katika miktadha tofauti. Vivyo hivyo, katika lugha za baadhi ya jamii kuna methali ambazo zikiangaliwa kijuujuu zinakinzana kimaana. Methali kama hizi zinaweza kutupiliwa mbali kama ambazo hazina maana yoyote ila tu zitumike katika miktadha yake tofauti. Kwa mfano, methali za Kiswahili *Haraka haraka haina baraka*, na *Pole pole ndio mwendo* haziwezi kuwa na maana yoyote kwa pamoja ila tu zitenganishwe na kutumika katika hali zake au miktadha yake tofauti na maalumu. Hata hivyo, Odaga na Akivaga (1982) wana maoni kuwa methali inaweza kutumika katika miktadha tofauti na kuiwekea mipaka ni kuiua methali hiyo.

Akilifafanua zaidi swala hili la muktadha Anozie (1981) ametoa maelezo kuwa ufafanuzi wa miktadha ya fasihi ya Kiafrika kama kigezo muhimu cha uelewaji wa miundo ya kijamii na kitamaduni ya kazi za fasihi umeachiwa wanafasihi ambao huishia kutumia miongozo ya nadharia zisizofaa. Inafaa ifahamike kuwa nadharia ya muktadha kwa fasihi ya Afrika inafaa kuwa kiungo muhimu cha maana. Kwa sababu, itasaidia katika kusaili anachojua mzungumzaji, mwandishi, msomaji, msikilizaji au hata mtafiti kuhusu muktadha, mazingira anamotolea madai yake pamoja na maana jumuishwa ya anachokisema. Utafiti huu ulitilia maanani maoni ya Anozie kwa kuchagua nadharia ya Udenguzi kwa kuwa dhima hasi ya methali inayokusudiwa kuchunguzwa inaweza kupatikana tu kwa kuzidengua methali husika.

Bambara (1998) amerejelea methali kama msemu wa kitamaduni ambao hasa huwa sentensi moja jumla na ambao huwakilisha ukweli kuhusu maisha. Methali zinapatikana katika jamii zote duniani, zimekuwepo tangu maelfu ya miaka iliyopita na mfano mzuri zaidi wa methali ni mkusanyiko wa methali zilizoandikwa na mfalme Suleiman katika Agano la Kale la Biblia Takatifu. Hata hivyo, japo Bambara alikuwa akiandika kuhusu utamaduni wa fasihi ya Afrika-Amerika hakutoa mifano kutoka jamii hizo. Zaidi ya hayo, utafiti huu haukujikita katika methali za jamii pana kama alivyofanya Bambara bali methali za Kiswahili pekee.

Tatizo la kijejezi mwafaka cha methali pamoja na mipaka ya miundo yake limeonekana katika tafiti za wataalamu wengi waliolivalia njuga swala la methali barani Afrika. Miongoni mwao ni Nyembezi (1954) aliyezifanyia utafiti methali za Kizulu na kugundua kuwa neno 'izaga' linatumika kurejelea 'methali' na pia 'nahau'. Finnegan (1970) pia aligundua tatizo lilo hilo katika utafiti wake wa methali za Wakamba, Fulani, Baganda, Nyamba, Limba and Mongo. Hata hivyo, hili si tatizo la lugha au fasihi simulizi ya jamii za Afrika tu kwa sababu kama inavyofahamika katika kamusi ya Kiingereza ya Hornby (2010) kando na neno la Kiingereza la methali '*proverb*' ambalo ndilo linafahamika zaidi kuna maneno mengine kama '*saw*', '*adage*', '*epigram*', '*apophthegym*', '*gnome*' na '*saying*' ambayo hutumiwa kurejelea dhana hiyo. Hata hivyo, tatizo hili linatofautiana katika muktadha wa Afrika na Ulaya. Katika lugha ya Kiingereza tatizo ni kuwa vipengele vingine vya lugha kama vile '*saw*', '*adage*', '*epigram*', '*apophthegym*', '*gnome*' na '*saying*' hutolewa kijejezi sawa na methali; yaani vyote huelezwa kama *kundi la maneno machache yanayobeba ujumbe wa busara*. Katika jamii za Afrika tatizo ni kuwa dhana methali huhusisha vipengele vingine vingi kando na methali vikiwemo

misemo, nahau na istiari. Utafiti huu haukujiingiza katika mjadala huu wa kijejezi cha methali bali ulichunguza kundi teule la methali za Kiswahili kubainisha kuwa dhima yake ni hasi na kuwa katika muktadha tofauti methali hizo hasi zinaweza kuwa na dhima chanya hivyo kuna utelezi wa maana.

Okpewho (1992) ameziweka methali, vitendawili, mafumbo na vitanza ndimi katika kundi moja aliloliita 'tungo za busara'. Pia, alivitaja vipera vyote hivi kama tungo fupi za fasihi simulizi zisizo na umuhimu mkubwa. Kuna uwezekano wa nahau pia kuwekwa katika kundi hili la Okpewho bila pingamizi kwa kuwa vipera vyote vinavyohusika ni vifupi na vinahitaji busara katika utunzi au uundaji wake. Swala la kutiliwa shaka hapa ni ikiwa vipera vyote hivi ni vyenye busara na zaidi ikiwa methali zinaweza kutajwa kama zisizo na umuhimu mkubwa katika jamii. Japo utafiti huu umeangalia baadhi ya methali za Kiswahili kama zenye dhima hasi, hauna maana kuwa methali zote si muhimu bali kuwa uhasi wa methali husika unatokana na ama tukio lililozalisha ambalo lilikuwa hasi au maana nasibishwa ambayo ni tofauti na maana asilia.

Miongoni mwa mengi ambayo ameyafafanua Schipper (1991), ni kuwa methali na misemo humpa mlumbi ujasiri wa kuongea kwa kuwa anaweza kuyazungumza maneno mazito na makali kwa njia dhahania na isiyo ya moja kwa moja bila yeye mwenyewe kuhusishwa na aliyoyasema wala kuyawajibikia. Kupitia methali mlumbi hujenga mpaka kati yake na maneno yake kwa kuyanasibisha na wahenga ambao ndio waanzilishi wa itikadi na maadili ya jamii. Anawahusisha wahenga na kuwafanya waseme kwa niaba yake maadamu maneno waliyoyasema wao hayapingiki. Hili ni jambo muhimu sana katika utafiti huu kwa kuwa methali zenye dhima hasi hutumika kwa njia iliyotajwa.

Ikiwa mzungumzaji kwa mfano, anataka kutumia methali yenye kuvunja moyo kama *Ngoma ya vijana haikeshi* kwa kupitisha ujumbe wa kuvunja moyo anainasibisha na wahenga na kuchukulia kuwa alilosema ni ukweli usiopingika na wala hafai kulaumiwa kwalo kwa kuwa si lake bali ameliomba kutoka kwa wahenga.

Kwa mujibu wa Mwikali na Coughlin (1990) katika utafiti wao wa methali za jamii ya Akamba, methali hutumiwa na wazee kumshauri mtu mmoja katika kundi bila kumtaja kwa jina. Mzee anaweza kutumia methali kumponda mtu mmoja katika kundi la wengi bila kundi nzima kujua anayepondwa ni nani ila tu mhusika. Utafiti huu kinyume na utafiti wa Mwikali na Coughlin umejikita katika methali za Kiswahili.

Odaga na Akivaga (1982) wana mawazo kuwa methali ni mkusanyiko wa tajriba za wanajamii ambazo hasa hazikuwa nzuri kwao au tajriba ambazo walijifundisha kwa uchungu mwingi. Zinafichua kile jamii inachohusudu na kile inachodharau na mwelekeo wa watu kuhusu maisha. Methali hupata malighafi ya kutumia katika kupitisha ujumbe wake kutoka kwa jamii na mazingira yake. Kwa mfano, methali za Wamaasai na Waswahili hutofautiana katika istiyari na jazanda zake japo zinawasilisha ujumbe mmoja. Maoni ya wataalamu hawa kuwa nyingi za tajriba zilizozalisha methali za jamii zilikuwa zenye uchungu mwingi yanaoana moja kwa moja na maoni ya utafiti huu kuwa methali zenye dhima hasi zipo na labda zilitokana na matukio yasiyopendeza yaliyoikumba jamii.

Akijibu swali la kwa nini alishughulikia utafiti wa methali tu bila kuzihusisha na fasihi Norick (1985) ametanzua kuwa ana sababu tatu muhimu; kwanza ni kwa kuwa methali ni kipashio kimojawapo cha lugha kinachobeba maana kama maneno na istiyari hivyo, ufafanuzi wa lugha yoyote hauwezi kukamilika bila kuzifafanua. Pili methali ni vipashio

huru na changamano vya lugha vinavyobeba maana na vinavyoweza kuchanganuliwa kipekee na tatu methali huwa na sifa za kipekee zinazoziwezesha kutumia maneno sahili tu katika kuunda kauli zilizosheheni maana changamano na nzito kiasi kuwa inarejelea kisa kizima. Kama ilivyo na utafiti wa Norick utafiti huu umezichanganua methali kama vipengele vya lugha vinavyojisimamia kivyake.

Isitoshe, methali hujisimamia kimaana na hujitokeza kivyake katika kauli mbiu za kampuni au makundi mbalimbali, matangazo, maandishi yanayoandamana na vibonzo katika magazeti, na hata maandiko yanayopatikana katika nyumba na ofisi za watu mbalimbali. Katika hali zote hizi methali huwa na dhima ya kiutangamano na kisiomitiki ya kimatini pamoja na picha au vitu vingine vinavyopatikana katika muktadha husika; hata hivyo maana ya methali hutawala. Maana muhimu kama hii inahitaji uchanganuzi wa kipekee. Zaidi ya hayo, jambo hili linauhalalisha usomaji wa methali kama matini. Hata inapotokea kama sehemu ya matini nyingine kubwa zaidi iwe andishi au simulizi maana huru ya methali huwa na mchango mkubwa wa kisemantiki kwa matini nzima.

Finnegan (1970) aliyejihusisha na utafiti wa fasihi simulizi ya jamii za Kiafrika kwa jumla ametaarifu kuwa methali zinajitokeza kwa wingi katika takriban kila jamii ya Kiafrika ikilinganishwa na jamii zingine ulimwenguni. Hata hivyo, ametaja kuwa jamii za Kibantu zina methali nyingi kuliko jamii za Kiniloti na Wanyika (Bushmen) wa Afrika Kusini. Katika utafiti wake pia amedhihirisha kuwa jamii nyingi za Kiafrika zina uhusiano wa karibu sana kati ya methali na vipera vingine vya fasihi simulizi ambapo zilihusishwa na vitendawili, ngano, misemo na mbazi katika jamii za Azande, Zulu, Ashanti, Nguni, Nyanja, Baganda, Fulani na Kamba miongoni mwa jamii zingine.

Isitoshe, methali za jamii za Kiafrika zimetawaliwa na mbinu nyingi za kisanaa zikiwemo taswira, istiari, kinaya, tashbihi, uradidi, chuku na ukinzano miongoni mwa zingine. Utafiti huu haukujikita katika sifa za juu za methali pamoja na mahusiano yake na vipengele vingine vya lugha au fasihi bali umejikita katika dhima zake ambazo zina mwelekeo hasi na chanya katika miktadha tofauti.

Ndungo (1998) naye ameshughulikia methali za Gikuyu na Kiswahili kama chombo cha kutubainishia taswira mbalimbali za mwanamke hasa taswira zinazoonyesha udhalilishaji wa mwanamke. Kijelezi chake cha methali ni kuwa; methali ni usemi wa kitamathali ambao husheheni utamaduni na matukio mbalimbali yanayohusu mielekeo, falsafa, na maono ya jamii. Ndungo amebaini kuwa methali zinapotumiwa katika mawasiliano ya watu, huwa ni kioo cha kudhihirisha utamaduni na uhalisia wa maisha ya watu hao. Mintarafu, taswira ya jamii hudhihirika kupitia matumizi ya methali ama katika mawasiliano ya kawaida au katika matini zingine hasa za kifasihi. Utafiti wa Ndungo umechukua mtazamo sawa kabisa na huu kwa kuwa umetaja baadhi ya methali za Kiswahili ambazo humdhalilisha mwanamke. Utafiti huu umepenya katika kina cha uhasi wa dhima ambao methali za Kiswahili zinaweza kuwa nao na kubainisha nyufa zaidi zinazopatikana katika dhima za methali hizo kwa kuonyesha kuwa kuna uhasi zaidi si tu ule wa kumdhalilisha mwanamke.

Methali za Kiswahili zimeainishwa na kuchambuliwa kwa kuzingatia uteuzi wa maneno katika methali hizo na Ngure (2003). Ngure amefasiri kuwa methali huwa na sura za kuvutia na methali nzuri hupita kinywani kwa ulaini wa aina yake, huku ikiwa na mahadhi ya kimuziki. Baadhi ya methali hata huwa na mapigo yenye urari na mpangilio

wa maneno usiokuwa wa kawaida. Utafiti huu kwa upande wake umejikita tu katika dhima ya methali wala si uzuri wake au sura yake ya juu.

Maitaria (1991) akishughulikia '*Methali za Kiswahili kama chombo cha mawasiliano: mtazamo wa kiisimu jamii*' ameeleza kuwa methali ni vyombo vya mawasiliano vinavyotawaliwa na misingi ya kijamii kama vile mahusiano ya watu, shughuli zao na kadhalika. Anahitimisha kuwa bali na kuwa methali ni mbinu inayotumiwa katika ubunifu wa kisanaa, ndani yake mna ujumbe fulani unaowasilishwa kwa mkato. Katika utafiti zaidi wa methali Maitaria (2012) aliyaaanisha mashairi ya Kiswahili kwa kutumia dhima ya methali huku akizingatia mashairi yanayotumia methali kwa wingi, yasiyotumia methali kabisa na yanayotumia methali chache. Kijumla Maitaria aliangalia dhima chanya ya methali kama kipengele cha lugha (1991) na kama kipengele cha fasihi (2012). Utafiti huu ni kinyume kabisa cha utafiti wake kwa kuwa umeangalia upande wa pili wa dhima ya methali za Kiswahili ambao ameepuka kuuangalia; yaani dhima hasi.

Baadhi ya watafiti waliotumia nadharia ya Udenguzi katika kazi zao ni pamoja na Ng'etich (2011). Ng'etich aliitumia nadharia ya Udenguzi kuichambua na kuibomoa lugha ya wahubiri kama ilivyotumiwa katika baadhi ya vitabu vya fasihi. Kwa kufanya hivyo Ng'etich anang'amua kuwa dini inatumiwa na wahubiri kama chombo cha kuwadhulumu na kuwanyanyasa waumini. Aidha, ameonyesha jinsi viongozi wa kidini hudhulumiana wao kwa wao, imani potovu za waumini kuhusu dini zinazowafanya wadhulumiwe kwa urahisi, ufaraguzi unaofanyiwa lugha ya dini ili iwe chombo cha dhuluma, aina mbalimbali za dhuluma na visababishi vyake pamoja na mbinu mbalimbali za sanaa zilizotumiwa na waandishi wa kazi za sanaa kupinga au kuunga mkono

udhalimu wa kidini. Kazi hii sawa na kazi ya Ng'etich itatumia nadharia ya Udenguzi lakini haitashughulikia swala la dini bali itajikita katika uchanganuzi wa methali za Kiswahili kutambua zile zenye uhasi.

Naye Mwamzandi (2013) ametumia nadharia ya Udenguzi kuichambua riwaya ya *Nyuso za Mwanamke na Dunia Yao* za Mohamed S.A. kwa kudhibitisha jinsi mwandishi alivyokuwa ametawaliwa na mawazo ya kidenguzi. Mwamzandi hasa amejikita katika mihimili miwili mikuu ya nadharia ya Udenguzi ambayo ni ukinzani wa jozi za maneno na hali ya Udenguzi kufutulia mbali mipaka ya kijoji na kuonyesha kuwa jozi za maneno ni mfano wa sarafu moja yenye pande mbili. Anauanisha hasa mhimili wa kwanza na mawazo ya mhusika mkuu wa *Nyuso za Mwanamke* kwa jina Nana anayesema;

Kwa kawaida nafsi yangu ilinifanya niamini kwamba hakuna utenganisho mkamilifu baina ya kuwepo na kutokuwepo. Sisi binadamu tupo kama hatupo au hatupo kumbe tupo. Basi, maisha ya siku hizi ni kama kuwepo ndani ya kutokuwepo au katika kuto-kuwepo na kuwepo. Ni hali ya kudinda ndani ya ukweli na uwongo (Mohamed 2010: 59)

Utafiti huu kinyume na utafiti wa Mwamzandi hautaichambua kazi yoyote ya fasihi kwa lengo la kuonyesha jinsi Udenguzi ulivyotumika bali itazichanganua methali za Kiswahili kidenguzi kwa lengo la kuonyesha kuwa baadhi yazo zina uhasi kwa upande mmoja na uchanya kwa upande mwingine.

Mung'athia (2011) pia aliitumia nadharia ya Udenguzi katika utafiti wake. Mtafiti huyu aliitumia nadharia hiyo kuyadengua baadhi ya mashairi ya Kiswahili ili kupata maana ya mtunzi. Anaanza kwa kusema kuwa, mashairi ni mafumbo na iwapo yatachanganuliwa kupitia vipengele vilivyoyajenga, maana itafafanuliwa na kuwekwa wazi kwa wasomaji. Aidha, utafiti wake unaongozwa hasa na mhimili wa Udenguzi unaosema kuwa kuna

uwezekano wa maingiliano ya fasiri mbili za kazi moja ya kifasihi zisizolingana kamwe kwa kuwa fasiri hizo mbili zina uwezekano wa kukubalika na wasomaji au wafasiri. Kuzingatia mhimili huo, Mung'athia anataja kuwa, lugha ya washairi ni changamano mno na inazua utata mwingi katika ufasiri wa maana na huenda maana tofauti zikatolewa na wasomaji tofauti wa shairi moja swala linaloweza kuangaziwa tu kwa kutumia nadharia ya Udenguzi. Japo utafiti wa Mung'athia unatumia nadharia ya Udenguzi kwa njia sawa na utafiti huu, tafiti hizi zinatofautiana kwa kuwa utafiti huu hautajikita katika mashairi ya Kiswahili bali methali za Kiswahili.

Tafiti za wataalamu mbalimbali walioangaziwa zimeziangalia methali kwa undani sana katika ama jamii moja mahususi, jamii lugha au jamii nyingi tofauti. Tafiti hizo hata hivyo zimeshughulikia upande mmoja tu wa dhima za methali ambapo zimegusia dhima chanya tu isipokuwa utafiti wa Ndungo (1998). Wengi wa wataalamu hawa pia wamezishughulikia methali kama zinavyojitokeza kimuundo, kimaana au kidhima ndani ya matini zingine. Aidha, baadhi ya tafiti hizo zimetaja kuwa methali zilitokana na miktadha na tajriba za jamii na kuwa baadhi ya tajriba hizo hazikuwa za kupendeza. Kwa mantiki hii, japo haikutajwa, tafiti hizo zinakubaliana na utafiti huu kuwa zipo methali zenye dhima hasi ambazo zilitokana na tajriba hizo zilizoiumiza jamii.

## **1.8 MBINU ZA UTAFITI**

Utafiti huu umefanywa maktabani. Mtafiti amekusanya data ya upili kulingana na malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia teule. Maandishi yanayohusiana na mada yamepitiwa kwa undani yakiwemo majarida, vitabu, magazeti na makala katika mtandao. Yote haya yamefanywa ili kupata data faafu kwa mada ya utafiti. Aidha, kamusi saba za

methali za Kiswahili zimepitiwa ili kufahamu methali nyingi zaidi zinazoweza kuufaa utafiti. Kigezo kikuu ambacho kimetumiwa kuchagua methali teule ni ujumbe wake; methali zenye ujumbe hasi zilipendelewa. Tafiti zingine zilizofanywa awali kuhusiana na mada ya utafiti pia zimepitiwa ili kujipatia ujuzi zaidi kuhusu mada kwa ujumla, ukusanyaji data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti.

Vitabu na maandishi mengine yanayohusu miktadha ya matumizi ya methali pamoja na uchambuzi wake pia yamepitiwa ili kuweza kupata ufahamu wa methali hasa za Kiswahili vyema zaidi. Isitoshe, vitabu vihusavyo nadharia teule vimesomwa kwa kina ili kuifahamu katika vipengele vyake vyote na kudhukuru jinsi mwafaka ya kuitumia. Data iliyopatikana hapa ni methali zenye dhima hasi ambazo zimechanganuliwa kwa mujibu wa nadharia ya Udenguzi na malengo ya utafiti.

### ***1.8.1 UTEUZI WA SAMPULI***

Katika utafiti huu sampuli lengwa imekuwa methali za Kiswahili zenye dhima hasi. Methali teule zimeteuliwa kwa mbinu kusudio. Methali hizo zimeteuliwa na mtafiti kutokana na utafiti wake wa maktabani ambapo amezipitia kamusi za methali zilizoandikwa na waandishi mbalimbali tokea miaka ya themanini hadi sasa. Kipindi hiki kilizingatiwa kwa kuwa ni hapa ambapo utafiti wa kina umefanyika kuhusu methali za Kiswahili hasa kwa lengo la kuzikusanya methali hizo na kupelekea kuchapishwa kwa kamusi nyingi za waandishi mbalimbali zenye orodha ndefu ya methali za Kiswahili. Baadhi ya kamusi zizotumika ni kama vile, ya Abudu na Baruwa (1981), Karama na Saidi (1983), Ndalul (1989), Wamitila (2001), Andambi na Muroho (2005), Waihiga na Kagwa (2007) na Kinge'i na Ndalul (2008). Utafiti umechunguza swala la uhasi katika

methali zinazopatikana katika kamusi zilizotajwa na kuchagua tu zile zilizopatikana kuwa na ujumbe usiofaa ama kwa jamii nzima au kundi mojawapo la wanajamii. Mtafiti ametumia kamusi nyingi katika uteuzi wa methali ili kuhakikisha kuwa amepata sampuli kubwa na faafu. Aidha, mtafiti alilenga pia kupata ufafanuzi uliotolewa na watafiti mbalimbali walioandika kamusi kuhusu methali teule ili kubainisha ikiwa wao wanauona uhasi katika dhima yake au la.

### **1.8.3 UKUSANYAJI WA DATA**

Data ilikusanywa kutoka kamusi saba za methali zilizoandikwa na waandishi tofauti. Kamusi hizi zilichaguliwa kwa sababu mbili kuu; kwanza kwa kuwa zinazitolea methali za Kiswahili maelezo kwa lugha ya Kiswahili na pili kwa kuwa zimekusanya methali nyingi (kamusi za hivi karibuni kama ya Wamitila (2001), Waihiga na Kagwa (2007) na Kinge'i na Ndal (2008) zikiwa na zaidi ya methali elfu mbili). Hivyo, ilimwia mtafiti rahisi kupata data faafu. Mtafiti alizisoma kamusi hizi ili kupata data ambayo inaufaa utafiti wake. Pia, alinukuu mambo yote muhimu katika pakatalishi ili kumwezesha kukamilisha utafiti kwa kupata data toshelevu kwa mahitaji ya utafiti. Ukusanyaji wa data ulihusisha uchunguzi wa mbinu zinazotumika katika methali hasa jazanda, itikadi za jamii, utamaduni, historia, miktadha rejelewa, uhamishaji muktadha, dini, taasubi za kiume na kike, uchumi wa jamii za kale pamoja na vipengele vinginevyo vinavyobebea uhasi katika methali za Kiswahili. Vipengele hivi vimechunguzwa ili kupata methali zinazotumia mbinu mbalimbali kupitisha ujumbe hasi kwa wanajamii.

#### **1.8.4 UCHANGANUZI WA DATA**

Baada ya data kukusanywa maktabani kwa kusoma na kunukuu, uchanganuzi umefanywa kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Methali teule zimechanganuliwa kubainisha jinsi zilivyo na dhima hasi. Uchanganuzi umefanywa pia kwa kuazinisha methali hizi kulingana na uhasi husika. Aidha, ufafanuzi wa manufaa ya methali hizo kwa jamii pia umefanywa kwa kuzingatia utofauti wa muktadha. Kulingana na Mugenda na Mugenda (2003) uchanganuzi wa kimaelezo unafaa zaidi katika kueleza maana za kauli wanazotumia watu katika mazungumzo yao. Kwa hivyo, uchanganuzi huu umefanywa kimaelezo kwa kuwa unahusisha maana zinazoambatana na baadhi ya methali zinazotumiwa na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili kila siku ama katika maongezi au maandishi yao. Mihimili changamano iliyotokana na nadharia teule pamoja na malengo ya utafiti imezingatiwa katika uchanganuzi. Hivyo, uchanganuzi umefanyika ikifahamika kuwa, methali ya Kiswahili inaweza kuwa na maana mbili kinzani; maana moja ikiwa chanya na nyingine hasi na baadhi ya matukio yaliyozalisha methali za Kiswahili hayakuwa ya kupendeza kwa jamii; ndio sababu yalizalisha methali zenye dhima hasi. Aidha, imetliwa maanani pia kuwa, methali za Kiswahili hupata maana kutegemea mtazamo wa mhakiki; kwa hivyo, zinaweza kuwa na fasiri tofauti katika kila mtazamo.

#### **1.8.5 UWASILISHAJI WA MATOKEO YA UTAFITI**

Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa njia ya maelezo kutegemea malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia teule. Matokeo hayo yamewekwa katika sura tano ambazo ni utangulizi, miktadha ya matumizi ya methali, uchanganuzi wa methali za Kiswahili kuonyesha dhima hasi, manufaa ya methali zenye dhima hasi kwa jamii na hitimisho.

## SURA YA PILI

### MIKTADHA YA MATUMIZI YA METHALI

#### 2.0 UTANGULIZI

Sura hii imeshughulikia ufafanuzi wa miktadha ya matumizi ya methali kwa kueleza miktadha bora ya matumizi yake pamoja na uibukaji wake huku ufafanuzi ukirejelea miktadha ya Uswahilini kwa kuwa nyingi za methali hizo zilitokana na mazingira, na tajriba za Waswahili kama wazungumzaji asilia wa lugha hiyo. Ufafanuzi unaorejelea methali za jamii zingine za Kiafrika umetajwa ikiwa unasaidia kutanzua hoja muhimu kuhusu miktadha ya matumizi ya methali kwa jumla. Baadhi ya methali hizi zinapatikana katika jamii nyingi Afrika na kote duniani, na ni vigumu kuamua ikiwa ziliombwa na Waswahili au watu wengine waliziomba kutoka kwao. Mbonde (2005) anazirejelea kama methali za kiutandawazi au za kimataifa. Aidha, sura hii imeeleza jinsi methali huishia kuwa na maana mbili au zaidi na wakati mwingine kinzani, na miktadha ya uibukaji na matumizi ya methali za Kiswahili zenye dhima hasi.

Katika kutoa ufafanuzi wa miktadha ya matumizi ya methali pia, baadhi ya tamaduni za Waswahili wa Pwani ya Kenya zimetajwa na mifano ya methali zinazoambatana na tamaduni hizo kutolewa kama njia ya kuonyesha uwiano uliopo kati ya miktadha zalishi ya methali za jamii na miktadha tumizi ya methali hizo.

#### 2.1 Umuhimu wa ufahamu wa miktadha ya matumizi ya methali

Japo ni vigumu kutoa kijejezi kamilifu cha methali tunaweza kusema kijumla kuwa methali ni msemu wenye muundo mahususi, unaotumia maneno machache kuwasilisha

ukweli fulani unaopatikana katika jamii. Kwa mujibu wa Waihiga na Kagwa (2007), methali ni semi fupi inayotumiwa kwa busara na iliyo na maana ya fumbo fupi ila lenye maana pana ambayo inapofasiliwa hupata mizizi katika jamii inayoitumia. Naye Durkheim (1933) ametoa maelezo kuwa methali ni kauli finyu inayohusu wazo la kijumla linalonasibishwa na vitu au hali kadha zilizokiliwa.

Yankah (1989) ameliendeleza wazo hilo la Durkheim kwa kusema kuwa haiwezekani watu kuamini kauli kama hizi bila kauli hizo kuwa na miundo maalum. Hii ni kwa sababu, dhana ikipata imani za watu na kusambazwa kwa wanajamii wengi inaishia kuwekwa katika muundo maalum ambao wameuzoea wao. Sifa kuu ya methali za Kiswahili ni ufupi na umaalum wake wa kimuundo aghalabu katika kiolezo hata kama maneno yanaweza kubadilika. Kando na sifa hizi zinazoweza kupatikana katika jamii nyingi zenye methali, methali za Kiswahili pia zina sifa ya ushairi ambayo huzitenga kabisa na tamathali zingine. Hata hivyo, methali hujumuishwa katika mkusanyiko wa methali za jamii fulani, ya Kiswahili ikiwemo, ikiwa inasemekana kuwa kauli inayokubalika na jamii nzima. Sifa hii huzua utata mwingi kwa kuwa ni vigumu kujua ikiwa mathalani baadhi ya methali zinazopatikana katika kamusi za wataalamu mbalimbali waliofanya utafiti wao katika lugha ya Kiswahili ni kauli zinazokubalika na jamii nzima au ni misemo tu inayotokana na mtu mmoja aliyeiibua kutokana na tajriba ya tukio moja tu lililomwathiri yeye na iliyochukuliwa na mtafiti na kujumuishwa kama methali kutokana na kupendezwa nayo kibinafsi. Ifahamike kuwa kamusi za methali hazionyeshi katika kila methali asilimia ya wanajamii wanaokubaliana na ukweli wa methali husika au wanaoifahamu. Jambo hili huleta utata zaidi kwa kuwa watafiti

hawaelezi muktadha wa uibukaji na matumizi ya methali hizi katika mtazamo wa wakati, utamaduni, jamii na mwanzilishi.

Ni muhimu kwa mtumiaji wa methali fulani katika jamii yoyote ile kujua methali hiyo iliibuliwa na nani, wakati gani, katika jamii gani ambayo ina utamaduni gani. Kwa kuwa ni vigumu kujua methali fulani ziliibuliwa na nani kutokana na mpito wa wakati, aghalabu watumiaji wanafaa kuambiwa utamaduni uliokuwepo katika jamii wakati wa kuibuliwa kwa methali hiyo kwa sababu utamaduni ni kichocheo kikuu cha falsafa ya jamii. Tatizo hasa hutokea katika methali zinazotaja miktadha ya kijumla bila watumiaji kujua muktadha mahsusi wa matumizi yake. Hivyo, methali “*Mgalla muue na haki yake umpe*” ingeeleweka vizuri zaidi ikiwa inafahamika iliibuliwa na nani, wakati gani, katika muktadha gani na uhusiano wa Wagalla na Waswahili, ambao ndio wana uwezekano mkubwa wa kuwa waliibua methali hii, wakati huo. Ni wazi kuwa aliyeibua methali hii hakuwa na mlahaka mwema na Wagalla kutokana na nasaha yake kuwa Mgalla auawe. Hata hivyo, haijulikani ikiwa huu ndio uliokuwa mtazamo au msimamo wa jamii nzima wakati huo na sasa au hizi ni hisia za mtu mmoja tu aliyekuwa na chuki ya kibinafsi kwa Wagalla. Uchambuzi wa miktadha ya uibukaji wa methali za jamii zote bali si Kiswahili pekee unaweza kuzisaidia jamii kufahamu ikiwa miktadha iliyoibua baadhi ya methali imepitwa na wakati na hivyo methali zinazonasibishwa na miktadha hiyo kupitwa na wakati pia. Ni kwa kufanya hivi tu ambapo baadhi ya methali zenye dhima hasi zinaweza kufahamika na labda kuondolewa kwa kuwa nyingi za methali hizo ni wazo la mtu mmoja au wachache tu na wala hazifai kuitwa methali bali maoni yao.

Kama ilivyotajwa awali, methali za Kiswahili zina sifa ya kishairi sifa ambayo zinashiriki na baadhi ya methali za jamii zingine za Kiafrika lakini isiyopatikana katika jamii za Kimagharibi. Kando na sifa hii kuna matumizi ya tashbihi, chuku, kweli kinzani na istiari katika kupitisha ukweli wa kijamii hasa kwa kuwa lugha inayotumika sana ni ya kitamathali. Hata hivyo, vidokezo vinavyopatikana katika methali za Kiswahili mara nyingi huwa havijulikani na kila mtu hasa kutokana na ukosefu wa ufahamu wa utamaduni wa jamii husika. Jambo hili hutokea hasa kwa methali ambazo zimetokana na ngano, tukio au watu maarufu. Ufahamu huu wa miktadha inayorejelewa katika methali ni muhimu kwa kuwa ni kupitia hilo ambapo tunafahamu maana ya methali. Methali moja inaweza kutumika kufafanua ukweli wa matukio tofauti, mitazamo mbalimbali ya ukweli mmoja au hata kutoa kauli ambayo ni kinyume cha ukweli unaofahamika ambayo hasa huwa na dhima hasi. Kinyume na nyimbo na hadithi methali hazina utendaji; hivyo, hazitegemei utendaji katika matumizi yake bali wepesi na uwezo wake wa kutumika katika miktadha tofauti tofauti. Wepesi huu ndio unaozifanya methali zilizoundwa kuwa na dhima chanya kuingizwa dhima hasi na vile vile kubakia na dhima chanya huku dhima hizi mbili zikitokea katika miktadha tofauti. Japo uelewa wa matukio ya uibukaji na matumizi ya methali ni muhimu kamusi za methali za Kiswahili zilizopo hazitaji lolote la muhimu kuhusu jambo hili ilhali mtumiaji hawezi kufahamu vidokezo vilivyo katika methali kikamilifu bila kufahamu matukio ya uibukaji wake.

Imetajwa awali kuwa methali za Kiswahili hutumia tamathali kama istiari na tashbihi. Tamathali hizi hasa hutumia vitu kama wanyama pori, samaki, miti na kadhalika. Jambo hili halitokei kwa sababu ya uhusiano wa aina nyingine yoyote ile kati ya Waswahili na wanyama au samaki bali kwa kuwa Waswahili waliishi karibu na pori kwa upande

mmoja na bahari kwa upande mwingine na ilikuwa lazima wao kutangamana na wanyama hawa kwa njia moja au nyingine. Hata hivyo, kwa kuwa huu sio muktadha pekee uliowazunguka methali zinazotaja miktadha mingine hujitokeza. Jambo la muhimu hapa ni kuwa bila uelewa wa si tu muktadha bali pia ufahamu wa umuhimu wa kinachotajwa kwa jamii ya wakati kilipotajwa, mtumiaji wa methali ataisema tu lakini hataweza kung'amua maana yake. Kwa mfano, ili kufahamu maana na dhima ya methali "*Dau la mnyonge haliendi joshi*" inabidi kuelewa maisha ya baharini na uvuvi kwa jumla, dau ni nini, joshi ni wapi, umuhimu wa uvuvi kwa jamii za kale za Pwani, na hata hatari ya dau kutoenda joshi. Vile vile, miti inayotajwa katika methali za Kiswahili ni ile inayopatikana katika mazingira yao tu kama mikoko, minazi, michongoma, mibono na kadhalika. Jambo hili si la Waswahili pekee hata hivyo, kwa kuwa jamii zote hutumia taswira zinazolengana na mazingira, tajriba na malengo yao katika methali zao.

Kimatumizi, methali huwasilishwa kitaswira. Taswira zinazotumika zinaweza kuwa zinazoonekana au fikirika; sahili au changamano. Vile vile, zinaweza kutokea katika umbo la tashbihi, istiari, tashhisi, ishara na kadhalika. Mathalani, methali zinaweza kutumia taswira kutoka nyanja za siasa, mazingira, maswala ya kijamii na uchumi miongoni mwa zingine. Hata hivyo, taswira husika zinapotolewa katika miktadha yake asilia na kuingizwa katika miktadha ya methali zinakuzwa na kukwezwa hivi kwamba hazirejelei hali moja tu bali zinakuwa viwakilishi vya hali nyingi tofauti. Methali nyingi hutaja majina ya watu na mahali. Kwa mfano, *Mungu si Athmani / Mzee Mkumba na Mwenda Pate harudi, kirudicho kilio* mtawalia. Methali hizi zina maana *Mungu si mwanadamu* na *Wapate ni watu wakali sana kivita hivyo wana uwezo wa kuwaua adui zao wote*, mtawalia. Ikiwa watu au mahali panapotajwa ni halisi, majina hayo humilikiwa

kuwili; katika ulimwengu halisi na katika ulimwengu wa ubunifu; yaani ulimwengu wa methali. Kufahamu ukweli wa kihistoria wa mahali au mtu anayetajwa katika methali husika kunamaanisha kujua pia historia ya methali husika. Hata hivyo, baadhi ya methali zimeundwa kutokana na majina ya kubuni tu wala hayahusiani na hali zinazotajwa kihistoria.

## **2.2 Uibukaji na udhihirikaji wa dhima hasi katika methali za Kiswahili**

### **kutegemea muktadha**

Methali kwa jumla hurejelea miktadha pana, na haiwezekani kamwe kutaja miktadha yote inayosheheni methali za Kiafrika na hasa Kiswahili. Miktadha hiyo huhusisha maswala yote ya maisha ya binadamu, huku baadhi ya vitu vinavyotajwa vikiwa mifugo, wanyama pori, ndege, wadudu, wageni, vita na zana zake, vifaa na kadhalika. Vitu hivi hutajwa katika miktadha ya mahusiano ya wanawake na wanaume, bidii ya wanadamu, kazi, maisha ya nyumbani, uhai na kifo, mpito wa wakati, maisha ya utawala na nguvu za kiutawala miongoni mwa mengine.

Swala la muktadha wa methali linaweza kueleweka vizuri hata zaidi tukihusisha hali ya mwingiliano wa wahusika, hali ya methali yenyewe, hali ya muktadha na uwiano. Hali ya mwingiliano wa wahusika inalenga muktadha wa kutumika kwa methali na uhusiano uliopo kati ya mtumiaji wa methali na msikilizaji kitabaka, kijinsia, kiumri na kadhalika. Kwa mfano methali “*Dua la kuku halimpati mwewe*” inaweza kusemwa na tajiri dhalimu kwa maskini mdhulumiwa. Uhusiano wao ni wa kiuchumi. Hali hii ya mwingiliano huchangia hali ya methali yenyewe ambapo uhusiano uliopo ni kati ya *kuku* na *mwewe*

ambapo kuku anamwomba mwewe dua (mbaya bila shaka kwa kuwanyakua vifaranga wake) naye mwewe analipuuza dua hilo kwa kuwa anaamini haliwezi kumdhuru kwa sababu ya uwezo wake mkubwa. Uhusiano huu umetumika kiistiari kwa hivyo unatuelekeza moja kwa moja kwa hali ya muktadha ambapo *tajiri* ndiye anayejipiga kifua kwa *maskini* kwa kuwa lalama zake kwa Mungu au kwa utawala kuhusu udhalimu aliomtendea ni bure tu kwa sababu hatofanywa lolote. Isitoshe, baadhi ya methali hazina wahusika wa moja kwa moja au zinadhihirisha mahusiano mengi. Mahusiano haya tofauti huibua maana na dhima tofauti kutegemea anayetumia methali husika, anayeelekezewa methali hiyo na nia ya msemaji. Ikiwa msemaji ana nia mbaya anaweza kutumia hata baadhi ya methali ambazo huonekana kuwa na dhima chanya kutoa maana hasi na hivyo kubadilisha dhima ya methali hiyo katika muktadha huo.

Methali ni kiungo muhimu sana cha lugha na fasihi ya jamii ambacho hudhaminiwa kiasi kuwa kinatumika baada ya sentensi chache katika kila mazungumzo hususan yanayohusisha wazee. Kinyume na tamathali zingine ni nadra kusikia methali zikitumika kufurahisha na kuchekesha tu bali hutumika katika miktadha hai ya maisha ya kila siku katika jamii. Umuhimu huu wa methali hata hivyo, si wa kipekee kwa methali za Kiswahili bali methali za jamii zote za Kiafrika. Kwa mfano, maelezo ya Nyembezi (1954) yanayotiliwa mkazo baadaye na Kanu (2014) ni kuwa, bila methali lugha ingekuwa kiunzi tu bila nyama; mwili bila roho. Anachosema Nyembezi hapa ni kuwa methali huchangia pakubwa sana katika uhai wa lugha ya jamii na zinapokosekana katika lugha, lugha hiyo hudhihirisha walakini. Ikiwa methali ni muhimu kiasi hiki basi, lazima zitumiwe ipasavyo na lazima tuhakikishe kuwa methali zinazosambazwa na kutumika na wanajamii zina dhima chanya kwao wala si methali za kuivuruga jamii.

Methali hazijatengewa msamiati wake wa kipekee, bali hutumia msamiati wa kawaida unaotumiwa na wanajamii kila siku. Kwa mantiki hiyo, upekee wa methali hautokani na miundo yake ya kipekee kwa kuwa haipo bali hutokana na imani ya kijumla ya jamii kuwa methali ni maneno ya busara, yanayovutia na yanayowakilisha ukweli. Methali hujipatia umuhimu kutokana na miktadha yake ya matumizi. Ikiwa methali fulani ina maana mbili au zaidi kinzani hili linatokana na uwezo wake wa kutumika katika zaidi ya muktadha mmoja na hasa kutokana na wanajamii kuwa na mitazamo tofauti ya kuliangalia jambo moja. Mitazamo hii ndiyo inayopelekea methali kuwa na dhima hasi kutokana na ama watu kuunda methali zenye dhima hasi ambazo huishia kusambazwa na kutumika na wanajamii wengi au kuziongezea methali zenye dhima chanya zilizopo dhima nyingine hasi. Evans-Pritchard (1956 na 1963) akizichambua methali za Zande ambayo ni jamii inayoishi Afrika ya Kati anasema kuwa neno “sanza” linalorejelea methali katika jamii hiyo linamaanisha methali na pia “*kijicho* au *wivu*.” Kando na hilo, anatoa maelezo yanayopewa ufafanuzi wa kina baadaye na Mieder (2004) kuwa methali huwa usemi mzunguko kimaana ambao huwa na maana ya ndani na nje ambapo hasa mojawapo ya maana hizo ni hasi. Jambo hili pia linapatikana katika methali za jamii zingine za Kiafrika zikiwemo methali za Kiswahili. Kwa mfano, maana ya juu ya methali *Asiye na mwana aeleke jiwe* haina maana mbaya kwa wanajamii na inaonekana tu kama yenye ujumbe usio wa kutiliwa maanani ila tunapochambua maana yake ya ndani dhima yake hasi inajitokeza kwa kuonyeshwa kwa mtazamo wake wa dharau kwa wanawake tasa.

Muktadha wa matumizi ya methali za Kiswahili huwa na athari kubwa kwa maana yake hivi kwamba takriban kila methali inaweza kumiliki zaidi ya maana moja chanya, hasi au

zote mbili. Mtumiaji ndiye anayechagua muktadha wa kuitumia methali kutegemea mahitaji au nia yake; nzuri au mbaya. Kijumla, methali hutumika kuonya, kumakinisha na kukejeli vitendo vya wengine. Katika kutekeleza jukumu hili la mwisho methali hasa huchukua uhasi wa hali ya juu hivi kwamba lugha fiche na kinzani kimaana hutumika kutoa hoja ya kejeli na dharau kumhusu mtu huku msemaji akibakia bila lawama kwa kuonekana kutoa usemi wa kawaida tu. Methali hapa hutumika kama ngao ya kujificha ili kuwasema watu vibaya au hata kuwatukana na kuwasengenywa bila kuwataja waziwazi. Japo mrejelewa anaweza kufahamu kuwa vijembe vilivyò katika methali vinaelekezwa kwake hawezi kulalamika kwa kuwa matusi anayotukanwa yamefichika ndani ya methali.

Ufiche huu wenye ufyongo wa kutumia lugha katika methali hutumika kuficha ufidhuli na unafiki pamoja na kukwepa kuwajibikia maneno anayosema mtu na hujitokeza sana katika ugomvi wa kijamii au hali zisizopendeza za mahusiano ya kijamii ambapo undani wa maana unajulikana tayari. Wakati mwingine hasa katika ugomvi methali hizi za kusuta na kudharau huelekezwa mlengwa kwa njia zisizo za moja kwa moja kama njia ya kujitenga na athari ya maneno hayo. Kwa mfano, Marie (2001b) akichunguza misemo na methali zinazopatikana katika kanga za Wanawake wa Kiswahili amefafanua kuwa misemo na methali hizo hutumika kupitisha ujumbe wenye mgogoro, fitina, wivu, kutoelewana, kutoridhika pamoja na jumbe zingine zisizoridhisha. Mbinu hii hutumika kwa sababu kwa 'kumvalia' mtu kanga yenye ujumbe fulani mlengwa ataupata ujumbe na ajue unaelekezwa kwake, ila hawezi kumuuzisha aliyevaa kanga na ujumbe husika moja kwa moja. Hata hivyo, Marie ameongeza kuwa mawasiliano ya aina hii hutokea kwa sababu ya kuwepo kwa vikwazo vya kimawasiliano katika jamii.

Aidha, kama ilivyotajwa awali kuna methali nyingi za Kiswahili zinazoweza kutumika katika miktadha mingi na kutoa maana nyingi tofauti katika kila muktadha hivyo kumlazimu mtumiaji kuelewa muktadha wa matumizi kabla ya kutafuta maana ya methali husika. Kimsingi, muktadha wa matumizi ya methali zozote zile hujitokeza katika sura na dhamira mbalimbali ikiwemo hali ya msemaji kujitenga na mjadala husika kisha kutoa methali inayobeba ujumbe jumla lakini mzito katika mada husika. Walumbi (wanasiasa wakiwemo) hutumia mbinu hii kukabiliana na wapinzani wao kwa kuwatukana na kuwasimanga hadharani bila wao kuwataja moja kwa moja. Katika hali hii usemi ambao huunda methali huoanishwa na mtu ambaye anaweza kuwa wa kweli au wa kubuni ambaye huhalalisha ukweli wa kauli husika. Msemaji huwa kama anayesema “Haya si maneno yangu lakini ukweli ni kuwa...” Jambo hili ni la kawaida katika methali zote za Kiswahili wala si katika methali zenye dhima hasi tu na linazua nafasi kubwa ya watu kutumia methali visivyo kwa kuwa hawawajibikii wasemacho. Katika utatuaji wa migogoro ya wanajamii vijijini pia mbinu hii hutumika kutoa maoni kumhusu mshukiwa au kujitetea bila kutaja swala husika moja kwa moja. Isitoshe, methali za aina hii hujitokeza katika hali ambapo kuna ugomvi lakini wahusika wanalazimika kutouanika ugomvi huo moja kwa moja kutokana na athari zake au aibu kwa watu wengine au kwa kutoufanya wa kibinafsi

Kando na muktadha, swala lingine muhimu katika methali ni mwanzilishi na mtumiaji wake. Methali za Kiswahili zinajulikana na takriban kila mwanajamii na ziko huru kutumika na kila mwanajamii. Watu hutumia sana methali zinazohusiana na miktadha yao ya kila siku. Aidha, wazee hutumia methali hususan za kutoa nasaha kwa wingi zaidi ya watu wengine kwa kuwa wao ndio wenye wajibu wa kutatua matatizo ya kijamii na

kutoa maamuzi. Kijumla, methali zote zinafaa kuwa zimebeba kauli zinazokubalika na kila mwanajamii. Hivyo, nafasi ya mwanajamii mmoja kuchangia methali yake yenye maoni yake yanayompendeza au yanayomfaa yeye binafsi huwa finyu sana. Hata hivyo, wepesi wa methali kujitokeza katika miundo mbalimbali na kutumika katika miktadha tofauti huibua upenyu wa mchango wa watu binafsi. Japo kila tunapotaja methali tunaanza kwa kudai kuwa ni maneno ya wahenga, wahenguzi na wazee wa kale, upenyu uliotajwa umetumika na watu kuunda methali mpya ambazo zimesambaa na kuingia katika orodha ya methali za jamii. Ni katika upenyu huu hasa ambapo watu wenye nia mbaya tangu kale walipata nafasi ya kutunga na kuingiza methali zenye dhima hasi kwa jamii katika lugha ya Kiswahili.

Kwa upande mwingine, methali hutokea katika kila muktadha ambapo lugha inatumika kuwasiliana ama kama kiungo cha sanaa au kama tamathali ya lugha; methali hujitokeza katika nyanja zote za maisha ya binadamu. Baadhi ya watu hasa kutegemea umri wanaweza kuzitumia kwa njia changamano zaidi huku wengine wakizitumia kwa njia wazi ila kwa kawaida methali hutumika sana panapo swala tata linalohitaji suluhisho. Hata hivyo, kama ilivyo kawaida ya watu kutatua shida kwa kutumia mbinu chanya na hasi, wengine hutatua utata uliotajwa kwa kutoa methali zinazolenga kuwavunja moyo wenzao, kuwadharau, kuwasimanga, kuwatabiria maovu miongoni mwa maovu mengine.

Methali pia hutumia ucheshi japo ucheshi wake umefungamana na utamaduni wa jamii kiasi kwamba unaeleweka vyema zaidi na watu wa jamii husika na wakati mwingine watu ambao si wa jamii husika wanaweza kushindwa kutambua ucheshi ndani ya methali. Hata hivyo, kama tujuavyo ucheshi ni chombo mwafaka cha kubebea tashtiti na

dhihaka. Tunapocheka mara nyingi tunasahau kugundua dhihaka, tashtiti au uhasi ulio ndani ya usemi. Ucheshi unakuwa kama kifunga macho cha kuzuia kupata uhasi uliofichika katika methali husika. Kwa mfano methali *Akunyimaye mbaazi akupunguzia mashuzi* na *Amnyimaye punda adesi ampunguzia mashuzi* zinachekesha kiasi kuwa mwishowe wengi hawapati kughamua kuwa zinabeba ujumbe hasi wa ubinafsi na kukata tamaa.

Kwa mujibu wa Yankah (1989) ukusanyaji na utafiti wa methali za lugha au jamii yoyote ile na kuzipa maana bila kuhusisha muktadha wake hakupuuzi upekee wake kati ya tamathali zingine tu bali kunazikosesha mvuto unaotokana na kutafiti nguvu za kipekee zilizo katika maneno ya hekima yanayotumiwa na badala yake kuendeleza chukulizi kuwa methali kama sanaa ya jadi zinatokana na masalio ya jamii ya kale takatifu. Kinyume chake ni kuwa miundo na maana za methali hubadilika kutegemea matumizi na wala si mahususi. Yankah ametoa mfano wa msomi Captain G. Merrick aliyetafiti methali za jamii ya Hausa na kuishia kulalamika kuwa wahojiwa hawakuweza kutoa maana moja mahususi ya methali. Alichokosa kuelewa Merrick ni kuwa methali za Kiafrika haziwekewi mipaka ya maana na matumizi bali hubadilika kutegemea muktadha. Yankah mwenyewe pia anasema kuwa alipokuwa akifanya utafiti wake mhojiwa mmoja alimpa maana mbili za methali moja kisha alipomwomba achague maana moja mhojiwa akamwambia kuwa “methali haibakii mahali pamoja bali hupaa.” Kupaa huku kwa methali kunaweza kuilekeza mahali panapoipatia maana tofauti kabisa na ile ya awali. Kwa mfano, methali yenye dhima chanya inaweza kupata dhima hasi, hali kadhalika kinyume chake kutegemea muktadha wa matumizi.

Aidha, ni vyema kuelewa tunachoita muktadha ni nini ili muktadha wa methali unaosababisha kubadilika kwa maana uweze kueleweka. Kimsingi, muktadha ni dhana ya kiisimu. Katika maana yake asilia muktadha unarejelea asili ya matini; ni hali inayotokea kabla ya kuibuka kwa matini. Hata hivyo, maana hii inaweza kupanuliwa kwa kuingiza hali ya kutamkwa kwa kauli, utamaduni wa jamii husika na historia ya msemaji na msemewa kama vipengele mojawapo katika muktadha. Gellner (1973) anafafanua kuwa japo muktadha hauepukiki, ni vyema kutumika, na ni muhimu sana, kwa wakati uo huo ni hatari kwa kuwa kuna uwezekano wa kutumiwa visivyo. Kutokana na mawazo ya Gellner ni vyema kutaja kuwa japo maana ya methali inaweza kutokana na makubaliano ya kimuktadha si kumaanisha kuwa maana yoyote inaweza kuwa sawa au kuwa mtumiaji wa methali hawekewi vikwazo vyovyote vya maana anayohusisha na methali fulani. Kinyume chake ni kuwa mtumiaji wa methali anaongozwa katika uchaguzi wake wa methali (na vivyo hivyo maana yake) na msimamo au mwelekeo wake katika mjadala husika, aliyosema kabla ya kuitaja methali na yanayofuatia methali tajwa. Mielekeo na mitazamo husika lazima iambatane na maana ya methali.

Katika upataji wa maana sadifu ya methali, sharti miktadha ambamo methali hutumika kuzingatiwa (Maitaria, 1991). Hivyo, ujumbe katika methali za Kiswahili hutegemea matumizi yake katika miktadha ya kijamii. Lengo la msemaji ndilo mhusika mkuu katika matumizi ya lugha. Mzungumzaji anapotumia methali fulani huwa na lengo la kuisitiza maoni yake. Hata hivyo, hakuna methali za aina maalum ambazo husisitiza lengo moja tu. Mtumiaji anaweza kuitumia methali mahali popote katika mazungumzo na katika miktadha tofauti ya kijamii anapoona inafaa ili kutekeleza lengo analodhamiria

mwenyewe hivyo methali hazijawekewa mipaka ya matumizi bali zimeachwa kupepea kutoka muktadha mmoja hadi mwingine.

### 2.3 Sifa za kimktadha za methali za Kiswahili

Katika jamii za Kiafrika, ambamo lugha muhimu zaidi ni lugha ya mazungumzo, methali zina nafasi kubwa sana. Zinatumiwa katika mazungumzo ya kawaida ya kila siku ama katika muktadha wa kutoa nasaha, siasa, mahubiri au zikifanya kazi ya kusisitiza jambo nzuri au baya linalofanyika. Baadhi ya watumiaji wa methali huzitaja kamili na wengine hutaja sehemu ya methali kwa kuwa vyovyote vile watu wanazijua mianzo na miisho yake maana ni sehemu ya hazina ya lugha kwa wazungumzaji lugha na wamezirithi moja kwa moja kutoka vinywa vya vizazi vilivyopita.

Kwa namna nyingine, kwa vile jamii ambayo methali huchota maneno na picha zake ni mazingira ya kimaumbile, dhana na fikra za wanajamii wa jamii fulani, methali ndizo hazina kubwa ya kutalii mazingira, utamaduni na maisha ya watu katika jamii. Kupitia methali tunaweza kufahamu aina za mimea na wanyama wa jamii fulani, hali ya hewa, vyakula, mavazi, dini, hali ya kimaendeleo, mifumo ya kiuchumi inayopendelewa, shughuli za kiuchumi, matambiko, sherehe, ushirikina na kadhalika. Mathalani, methali za Kiswahili kama *Asiyefunzwa na mama hufunzwa na ulimwengu, Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo, Mchelea mwana kulia mwisho hulia yeye na Jogoo halei mwana zinaweza kutufahamisha maswala ya uzazi na ulezi, huku Kukopa harusi kulipa matanga ikitufahamisha kuhusu masuala ya ndoa na arusi. Isitoshe, methali Siri ya kaburi aijuaye mwosha, Mchimba kaburi huingia mwenyewe, Adhabu ya kaburi aijuaye maiti hugusia maswala ya kifo na uzikaji. Tunaweza pia kufahamu kazi walizofanya Waswahili kukimu*

mahitaji yao ya kiuchumi kupitia methali kama; *Ukiona vyaelea vimeundwa, Dau la mnyonge haliendi joshi, Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani, Kumla nguru si kazi kazi ni kumwosha, Avumaye baharini papa kumbe wengi wapo, Hasira za mkizi furaha ya mvuvi, Maji yakijaa hupwa, Mfa maji haachi kutapa, Manahodha wengi chombo huenda mrama, Usisahau ubaharia kwa sababu ya unahodha, Akiba si mbi ingawa ya kumbi siku ya kivumbi hutiwa motoni, Aliyekupa wewe kiti ndiye aliyenipa mimi kumbi, Mke ni nguo mgomba hupaliliwa, Mchagua nazi hupata koroma, Mchele mmoja wapishi wengi, Mkagua jembe si mkulima, na Nazi mbovu harabu ya nzima* (Maitaria, 1991). Methali *Mungu si mzee Mfaki na Kafiri akufaaye si islamu asiyekufaa* zinasawiri mtawalia kuwa jamii ya Kiswahili ni watu wenye imani ya Uungu na wengi wao ni Waislamu.

Ni muhimu kutaja pia kuwa, tunapochunguza methali mbalimbali za Kiswahili tunatambua kuwa zina sifa mbalimbali za kipekee. Mathalani, kuna methali zenye msamiati mkongwe ambao hudhihirisha sifa za kilahaja. Methali hizo ni kama vile *Mchama ago hanyele huenda akauya papo* (Kipate), *Afadhali dooteni kama ambari kutanda* (Kiamu), *Msi kucha kwambwa nyamba* (Kipate), *Kuva mva na mvuvi* (Kiamu) na *Nguwe huagana wakenenda* (Kiamu na Kipate). Methali zingine hususan *Hindi ndiko kwenye nguo na wenda tupu wako* na *Usione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi*, zimehusishwa na mshairi mtajika wa karne ya kumi na tisa kwa jina Muyaka bin Haji huku zingine zikionyesha sifa za kuwa na chuku au balagha sifa ambayo hasa hudhihirika tunapochunguza sifa ya kijuujuu ya methali wala sio sifa ya kitamathali. Methali hizi ni kama *Ndovu akitamba ni masika, Hakuna kubwa lisiloshindwa, na Papo kwa papo kamba hukata jiwe*. Japo chuku hii haielekei kuonekana methali hizi zinapotafsiliwa kwa

fasiri ya kisanifu ya methali, ni vyema kufahamu kuwa maana ya juu ambayo ndiyo hubeba chuku ni muhimu pia kwa kuwa ndiyo watumiaji lugha wanayokumbana nayo kwanza na baadhi wanaweza kukosa kufanya ufasiri wa kisanifu.

Sifa nyingine muhimu ya kiisimu iliyo katika methali ni hali ya kuweza kugawika katika vipashio viwili japo si methali zote za Kiswahili zenye sifa hii. Methali zinazoweza kugawika ni kama; (*Aliye juu*) (*mngoje chini*), (*Aliyeshiba*) (*hamkumbuki mwenye njaa*), (*Asiyefunzwa na mamaye*) (*hufunzwa na ulimwengu*) na (*zimwi likujualo*) (*halikuli likakwisha*) miongoni mwa zingine nyingi. Fauka ya hili, baadhi ya methali zinabeba ujumbe wenye ukinzani au ukwelikinzani katika vipashio viwili vilivyotajwa. Hizi ni methali ambazo hupingana kati ya sehemu ya kwanza na sehemu ya pili. Mifano ya methali hizo ni kama (*Kuinamako*) (*ndiko kuinukako*), (*Embe dodo*) (*sawa na kisukari*), (*Mgeni pofu*) (*ingawa ana macho yake*), (*Naije baa*) (*iondoe baa*) na (*Amani haiji*) (*ila kwa ncha ya upanga*). Kando na ukinzani ambao huleta utata, baadhi ya methali za Kiswahili hupata utata kutokana na urefu wake ambao huzifanya kufupishwa zinapotumiwa katika mazungumzo ya kawaida. Mathalani, methali *Mwana mtukana nina kuzimu enda kiona, enda pigwa mikatale na pingu za mikono nyuma, na silisili za chuma za moto wa jehanamu hurejelewa kifupi Mwana mtukana nina kuzimu enda kiona* na huenda watu wanaojifundisha lugha wakaishia kuitumia kifupi pekee bila kuwahi kuufahamu ukamilifu wake. Aidha, kuna methali ambazo pia huonyesha matumizi ya sitiari kama *Ujana ni moshi ukienda haurudi na Usilolijua ni usiku wa kiza* miongoni mwa mbinu zingine nyingi kama tabaini, usambamba na tashibihi.

Swala la mwisho la kuangazia katika sura hii ni kuwa, japo utafiti huu umelenga kuzichanganua methali zinazodhihirisha mazingira na miktadha ya Uswahilini kwa kuwa ndizo methali asilia za Kiswahili, umetilia maanani pia wazo la Senkoro (1988) katika kuwekea mipaka fasihi ya Kiswahili. Senkoro anatoa ufafanuzi kuwa;

‘Tutaamua kuwa kazi fulani ni ya fasihi ya Kiswahili au la kutokana na jinsi ilivyojitambulisha na ilivyojikusisha na utamaduni wa Kiswahili. Hapa neno Waswahili halimaanishi kabila la Waswahili kwani kabila la namna hiyo halipo leo. Waswahili hapa ni wananchi wa Afrika Mashariki na Kati kwa jumla na wala si wale tu wanaoishi katika pwani ya nchi hizi.’ (uk.11).

Wazo hili la Senkoro lina maana kuwa lugha, utamaduni, itikadi, fasihi na hali ya maisha ya Waswahili kwa jumla imesambaa na kuwa hata kitambulisho cha takriban watu wote wa Afrika Mashariki na Kati kwa watu wa maeneo mengine ya dunia. Hata hivyo, si utamaduni wa Waswahili ulioadhiri maeneo mengine tu bali utamaduni wa Waswahili pia umeathiriwa na utamaduni wa kwingine. Kwa mantiki hii, inawezekana kupata methali ya jamii nyingine iliyoingiliana na mazingira na miktadha wa Waswahili hivi kwamba inadhaniwa kuwa ya kiasili.

## **2.4 KIISHILIO**

Sura hii imeshughulikia miktadha ya matumizi ya methali kwa ujumla na pia kwa kujikita katika upekee wa methali za Kiswahili. Tumefanya hivi kwa kuzingatia kuwa methali za jamii nyingi, za Kiswahili zikiwemo, zina uhusiano mkubwa na mazingira pamoja na utamaduni wa jamii japo kwa wakati uo huo zimepewa uwezo mkubwa wa kuweza kupaa na kutua katika miktadha mingine tofauti kabisa. Kwa jinsi hii, uchanganuzi wa miktadha ya matumizi ya methali za Kiswahili umebainisha jinsi methali

zinavyohamishwa kutoka muktadha mmoja hadi mwingine na kuishia kupata maana na dhima mpya kwa wanajamii huku dhima ya awali ikidumishwa au ikisahaulika kabisa. Aidha, sifa za kijumla za methali, dhima zake chanya pamoja na mbinu za uainishaji zimetajwa na kufafanuliwa. Sura ijayo itashughulikia methali za Kiswahili zenye dhima hasi kategoria na kwa kutoa ufafanuzi wa kina.

## SURA YA TATU

### UCHANGANUZI WA METHALI ZA KISWAHILI ZENYE DHIMA HASI

#### 3.0 UTANGULIZI

Sura hii imefafanua dhima hasi kama inavyopatikana katika methali teule. Methali zote zimechanganuliwa na kudenguliwa hivi kwamba dhima hasi imejitokeza wazi katika kila mojawapo. Methali zinazowiana kimaana na kidhima zimechanganuliwa pamoja. Sura hii pia, imeanza kwa kufafanua baadhi ya kanuni za matumizi ya lugha kama zilivyowekwa na Grice na Leech kama thibitisho mojawapo kuwa kwa kweli methali teule hazina dhima yoyote chanya katika miktadha inayolengwa katika uchanganuzi au katika baadhi ya methali katika miktadha yoyote iwayo.

Methali nyingi za Kiswahili zina dhima chanya na huasa au kuelekeza jamii kwa upole na hekima kuu. Hata hivyo, baadhi ya methali hizo zina dhima hasi ambapo maana zake huwa tu za kuelekeza jamii kusikofaa au kutoa maneno makali yenye kuziümiza nyoyo za wanajamii. Mohamed S.A. katika utangulizi wa kamusi ya methali ya Wamitila, (2001) anafafanua:

“Kazi nyingine ya methali inasemekana kuwa kama mafuta, kulainisha usemi. Hii ina maana kwamba kuna njia mbalimbali za matamko na matumizi ya lugha. Matamko mengine ni makali na ya kukasirisha, mengine laini na ya kupoza na kuburudisha. Inavyoonekana kuna methali chache ambazo hazina ulaini kiasi hicho; kwa mfano, *Akutendaye mtende, mche asiyekutenda* ikilinganishwa na *Adui mpende* au *Amani haiji ila kwa ncha ya upanga* ikilinganishwa na *Subira yavuta heri.*”

Mohamed (keshatajwa) anatilia mkazo hapa kuwa si methali zote za Kiswahili zina uchanya wa dhima bali kuna baadhi ambazo dhima zake haziiridhishi jamii zinapoangaliwa kijuujuu na hata kindani. Hili analotaja Mohamed kwa ufupi ndilo utafiti

huu umezamia kwa undani katika sura hii kwa kuzichambua methali za aina husika kidhima na kikategoria kwa lengo la kuibua dhima hasi inayopatikana katika methali hizo.

Ligami na Barasa (2006) wamegusia methali chache zenye dhima hasi na wanatamatisha kwa kusema kuwa swala la kujiuliza kuhusiana na methali za aina hii ni ikiwa ujumbe wake unafaa katika kuubadilisha mwenendo wa binadamu. Wameendelea kusema kuwa hili ni swala la kisemantiki na kipragmatiki. Ni swala la pragmatiki kwa sababu, maana huelezwa kulingana na msemaji au mtu anayetumia lugha hiyo. Katika muktadha huu, watumiaji lugha ni wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili na hasa wahenga walioibua methali. Kwa upande mwingine, ni swala la kisemantiki kwa kuwa maana huelezwa kama umiliki wa kujieleza katika lugha fulani kidhahania bila kuzingatia wasemaji au wasikilizaji.

Utafiti huu ulizingatia mtazamo wa kipragmatiki kwa kuzingatia kuwa methali za lugha yoyote ile Kiswahili kikiwemo hazikuibuka katika ombwe tupu bali zilitokana na matukio maalum katika jamii yaliyotendwa na wanajamii au mwanajamii fulani, mahali fulani na katika muktadha fulani mahsusi. Isitoshe, Mey (2001) anafafanua kuwa, watu hutumia lugha kwa lengo la kuwasilisha ujumbe fulani kwa mtu fulani. Katika pragmatiki, swala kuu katika mawasiliano au matumizi ya lugha ni kupitisha ujumbe. Katika kutanguliza kanuni zake Grice (1975) anatoa kanuni kuu isemayo;

‘Fanya mchango wako katika uzungumzaji uwe kama unavyohitajika kuwa katika muktadha husika, kwenye lengo husika na mkondo wa uzungumzaji ulio kwao.’

Kanuni hiyo ya Grice inamaanisha kwa ufupi kuwa muktadha wenye majonzi kwa mfano, unahitaji lugha ya kutia moyo wala si kuponda na kuvunja moyo huku muktadha wa safari na juhudi za kutarazaki ukihitaji kupewa hamasa wala si kuzima ari kama ilivyo katika methali *Dau la mnyonge haliendi joshi*. Kwa upande mwingine, vitendo viovu au vinavyotendwa bila makini huku vikielekea kusababisha hasara vinafaa kukashifiwa wala si kujificha chini ya methali kama *Ajali haina kinga*.

Grice (1975) na baadaye Leech (1983) katika kazi zao tofauti wametoa kanuni ambazo zinafaa kuongoza matumizi ya lugha katika jamii japo wahakiki wa baadaye kama Sperber (1995) na Mey (2001) wamepinga baadhi ya yale waliyosema. Grice na Leech wametoa kanuni mbili kuu za matumizi ya lugha. Kanuni hizi zinafaa sana katika uchambuzi wa maana na matumizi ya methali kwa kuwa methali ni mojawapo wa vipengele vinavyotawala mazungumzo ya wanajamii na zinapotumiwa katika sentensi, sentensi nzima au hata aya hutawaliwa na maana ya methali husika.

### **3.1 Kanuni ya kwanza; Kanuni ya uzungumzaji**

Kanuni ya uzungumzaji imeangaziwa sana na Leech (1983) anayesema kuwa msingi wa isimu (sayansi ya lugha) ni watu kutumia lugha kwa lengo la kuwasilisha ujumbe kwa wenzao katika jamii. Kila watu wanapotumia lugha hufanya hivyo kwa nia ya kuwasiliana ikiwa wanatumia kaida za kisarufi au la. Kuwasiliana nako hutegemea uwezo wa mtumiaji lugha kuweza kuwasiliana kutegemea muktadha na anacholazimika kuwasilisha kutegemea hali ya msikilizaji. Mawasiliano katika matumizi ya lugha hayategemei mantiki wala ukweli bali hali kuwa mawasiliano yamefanyika; yaani kilichosemwa kimesemwa. Vivyo hivyo, methali hutumika si kwa lengo la kupamba

lugha tu bali sababu kubwa ya kupatikana kwake katika maongezi ni kupitisha ujumbe. Methali yenye ujumbe hasi hupitisha athari yake kwa hadhira moja kwa moja iwe inarejelea tukio la kweli au la.

### **3.2 Kanuni ya pili; Kanuni ya ushirikiano**

Kwa mujibu wa Grice (1975) kanuni hii ina sheria nne ndani yake ambazo ni; Sheria ya kiwango, inayoangazia vipengele kama; mchango wa mzungumzaji katika uzungumzaji (uwe na ujumbe kiasi kinachohitajika na asiongezee kiasi cha ujumbe usiohitajika), sheria ya ubora inayotoa amri kuwa mzungumzaji asiyaseme mambo ayaaminiyo kuwa ni uwongo wala mambo ambayo hayana ithibati, sheria ya maelezo inayomtaka mzungumzaji afanye maelezo yake yaambatane na mjadala husika na sheria ya namna inayohitaji maelezo ya mzungumzaji yaeleweke, aepukane na mafumbo na utata, aseme kwa ufupi na afuate mpangilio.

Sheria zingine ni kama sheria ya mbinu inayomtaka mzungumzaji apunguze hasara kwa mwenzake huku akiongeza faida, sheria ya ukarimu inayomnasihi mzungumzaji kupunguza faida kwake, sheria ya sifa inayotaka apunguze sifa zake huku akiongeza kutojisifu na sheria ya makubaliano inayowataka wazungumzaji wapunguze kutokubaliana baina yao na wenzao na badala yake kuongeza makubaliano. Isitoshe, kuna sheria ya huruma inayoshauri mzungumzaji apunguze chuki kati yake na wengine na badala yake kuongeza huruma.

Kwa mujibu wa kanuni na sheria zilizotajwa, wanadamu wameumbwa hivi kwamba wanapendelea kusikia mambo mazuri wala sio mabaya kama ya kuvunja moyo, kutisha,

kukemea na kadhalika. Kwa upande mwingine, ni kawaida ya mwanadamu kupendelea kuonyeshwa upande mzuri wa mambo wala si mbaya hata katika mambo ambayo yanadhihirisha uhasi wa moja kwa moja.

Katika sura ya pili, mengi yamesemwa kuhusu miktadha mbalimbali ya matumizi ya methali na hivyo uwezekano wa methali kubeba maana nyingi. Mintarafu, uainishaji wa methali katika misingi ya kidhamira na kimaudhui umekashifiwa kama usio kamilifu na badala yake uainishaji unaoegemea mkabala wa kiisimu, kimuundo na kipragmatiki kupendelewa. Hata hivyo, wanaochukua mikabala ya kiisimu, kimuundo na kipragmatiki wamesahau kushughulikia dhima fiche ya baadhi ya methali za Kiswahili ambayo huwa hasi. Dhima hii ndiyo inayoangaziwa na sura hii. Utofauti huu unajitokeza hata katika kijejezi cha methali ambacho huwa kigumu kutolewa moja kwa moja kwa kuwa hutegemea mtazamo gani wa methali tunaochukua. Katika mtazamo wa kazi ya methali mara nyingi, methali hufafanuliwa kuwa misemo ya kimapokeo yenye kunata hekima na busara na kwa hivyo matumizi yake ni ya mafunzo, maaso na mwongozo katika maisha. Katika hali hii methali ni vifaa vinavyobebea uzoefu na maadili ya jamii yanayotumiwa na wanadamu kuweka uwiano mwema kati ya mtu na mwingine. Hii ndio sababu methali za tamaduni nyingi hufanana. Kufanana hutokea kwa sababu lengo na kazi ya methali kwa kila utamaduni ni moja; yaani kuweka mapatano na umoja baina ya watu (Kropacek, 1997).

Kwa mujibu wa Wamitila (2008), swala linalojitokeza hapa ni je methali zote zinanata busara? Na jibu linakuwa, methali nyingi za Kiswahili zina sifa iliyotajwa lakini si zote. Utafiti huu umejikita katika kundi hili la methali lisilonata busara ama kikamilifu au

zinapotumika katika muktadha fulani jambo linalofanyika kwa kuzingatia malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia ya Udenguzi pamoja na kanuni zingine zilizotajwa.

### 3.3 AINA ZA METHALI HASI

#### 3.3.1 Methali kandamizi

Kukandamiza ni hali ya kutumia uonevu, dhuluma, nguvu na vitisho kuhakikisha kuwa mtu au kundi fulani la watu limetawalika au limebakia katika hali yake ya unyonge. Methali zinazoangukia katika kundi hili hasa hutawala maskini kisaikolojia kwa kuwakumbusha kila mara kuwa wao ni wanyonge na hawawezi kujikwamua unyongeni. Methali hizi zinaweza kutumiwa na wenye nguvu kuwanyamazisha wanyonge au wanyonge wenyewe kujihalalishia hali zao duni. Mifano ya methali hizo ni kama;

- a) *Mkata hendi Mkele, angenda Mkele na kujaza mtele jahazi tele hurudi na upele*

Maneno 'hendi' na 'mtele' yana maana ya 'haendi' na 'mchele' katika Kiswahili sanifu mtawalia. Mkele ni mji wa zamani uliokuwa Pwani Kaskazini (King'ei na Ndal, 2008). Methali hii ina uhasi katika hali kuwa inaamua hatima ya mkata moja kwa moja kuwa hataweza kufika Mkele. Licha ya hayo, inamtabiria mawi kuwa hata akifaulu kwenda huko mtaji wake utashia hasarani kwa kuwa kando na kutorudi na mchele atarudi na upele (ugonjwa wa mtu kupata vituruturu mwili mzima ambavyo huwasha sana na kutunga usaha). Ifahamike kuwa, mkata ni maskini wa kupindukia. Huyu ni maskini *asiyekuwa na mbele wala nyuma; asiyeweza kukimu hata mahitaji yake ya kimsingi* kabisa kama chakula na nguo. Mkata huwa katika hali mbaya zaidi ya maskini wa

kawaida. Ikiwa Mkele huwa na mchele mwingi unaoweza kujazwa jahazi tele inamaanisha kuwa mavuno huko yanapatikana kwa wingi na ni rahisi kwa mwanadamu yeyote kufanikiwa kupata kipato chake huko. Hivyo, methali hii ina maana kuwa mkata hawezi kufanikiwa hata penye mavuno tele. Methali hii imesheheni maonevu kwa maskini na inamvunja moyo huku ikimwonyesha kuwa hana haja ya kutia bidii maishani kwa kuwa majaaliwa yake ni kutofanikiwa tu. Isitoshe, inambagua na kuzididimiza juhudi zake za kujipatia riziki. Methali hii ina maana sawa na methali “*La mkata halikiti na likikita ni mavumvuwele.*”

b) *Asiye na mwana, aeleke jiwe*

Uhasi wa methali hii unatokana moja kwa moja na kupitwa na wakati kwa muktadha wake zalishi. Mukstadha huo umedidimia kwa kuwa unafahamika na watu wachache sana hasa wazee katika jamii ya Waswahili. Methali hii inatokana na karamu zilizokuwa zikiandaliwa na wafalme wa zamani ili kusherehekea na watu wa janibu zote za utawala wao. Wafalme mbalimbali wa Uswahilini walikuwa wakiandaa karamu mara kwa mara hususan panapotokea jambo la kusherehekea na kuwaita watu waje karamuni. Kwa kuwa teknolojia ya mawasiliano haikuwa imerahisishwa kama ilivyo sasa wafalme wangewatuma wajumbe ambao walipita vijijini wakipiga ngoma na kupuliza siwa huku wakiwafahamisha watu kuwa walihitajika kwenda kusherehekea karamu kwa mfalme. Katika juhudi zao za kuwahimiza watu na kuusisitiza ujumbe wao wajumbe walisema maneno yaliyofuata mkondo kama “jamani mnaalikwa katika karamu ya mfalme hii leo alasiri. Asiye mwana aeleke jiwe, aliye chongo aweke gololi tukutane karamuni kwa mfalme hii leo alasiri.”

Kueleka ni hali ya kubeba kitu mgongoni. Kwa kawaida wanaoeleka wana au watoto katika jamii za Kiafrika ni wanawake. Enzi hizo, wanawake kubeba watoto mgongoni wanapoelekea shambani, shereheni na kadhalika lilikuwa jambo la kawaida na mwanamke kumweleka mtoto katika harakati za kuondoka nyumbani ilikuwa ishara tosha kuwa alikuwa tayari. Isitoshe, wanawake wenye watoto migongoni wangeshughulikiwa kwa dharura zaidi jambo ambalo linatendeka Pwani ya Kenya hadi sasa. Kwa kuwa sasa hamna mfumo wa utawala wa kifalme miongoni mwa Waswahili hamna sherehe tena na hata zingekuwepo teknolojia ya habari na mawasiliano isingeruhusu mbinu zilizotumiwa kupitisha habari wakati huo kutumika. Katika jamii nyingi mwanamke ambaye hana uwezo wa kupata mtoto alikuwa anaonekana kuwa na upungufu wa hali ya juu kwa kuwa ingekuwa vigumu kuidumisha ndoa yake na mapenzi ya mumewe. Katika nyingi za jamii hizi mume husika alilazimika kumwoa mke wa pili huku yule tasa akibakia tu au kurejeshwa kwa wazazi wake. Hali inayoleta majonzi kwa mwanajamii kama hii si hali ya kufanyia stihizai na mizaha. Kwa kuwa hali hii inamuumiza mhusika moyo tayari si vyema kumtia msumari moto kidondani kwa kumwambia kuwa alibebe jiwe kama mtoto. Kwa mujibu wa kanuni za Grice tunafaa kuongeza huruma kati yetu na wenzetu.

*c) Aliye na nguvu hula, dhaifu hulipa.*

Methali hii inataja kitendo cha mwenye uwezo kula au kutumia kitu fulani na mnyonge kulazimika kulipa kama kitendo cha kawaida kabisa na ambacho hakina ubaya wowote. Kwa kufanya hivi inawavunja moyo maskini na kuusawiri unyanyasaji wa wanyonge kama majaaliwa jambo ambalo si la kweli. Methali hii ina mwelekeo hasi kwa watu

dhaiifu na haiwezi kutumika kwa njia ya kuwapendelea au kuwafaa wao katika muktadha wowote.

*d) Cha mfupi huliwa na mrefu*

Katika muktadha wa methali hii mfupi ina maana ya mnyonge huku mrefu ikiwa na maana ya mwenye nguvu. Jazanda hii imetokana na hali kuwa jamii nyingi duniani zilichukulia urefu kama ishara ya nguvu na mashujaa wote walio katika simulizi za jamii kama vile Fumo Liyongo wa Waswahili walielezwa kuwa warefu wa kimo. Badala ya kumtetea 'mfupi' au kumwonyesha mbinu za kujitetea, methali hii inataja uovu unaotendeka kwa njia ya kuuhalalisha na kuonyesha ukawaida wake hivyo kumzidishia majonzi anayedhulumiwa.

*e) Mapenzi ya maskini hayaonekani*

Maskini ni mtu ambaye hana pato la kutosha kukimu mahitaji yake. Hata hivyo, kuwa maskini hana pato la kutosha hakumaanishi hana chochote kabisa; ana kipato ila ni kidogo sana kiasi cha kuwa hawezi kukitumia kutekeleza mambo ya haja. Mapenzi nayo ni hali ya kumthamini mtu. Aghalabu wanaume, hususan Waswahili wa kale na sasa hutumia zawadi za vito vya fedha, almasi, shaba na dhahabu pamoja na nguo, vitambaa na tunu nyinginezo kuwadhihirishia wanawake wao mapenzi yao. Hata hivyo, mapenzi hayako katika tunu hizi bali kwa watu wote mapenzi huchipukia moyoni kwa hivyo kimsingi hayaonekani yawe ya tajiri au maskini. Kwa upande mwingine, maskini anaweza kuonyesha mapenzi yake kwa matendo au vifaa vilivyo katika upeo wa uwezo wake wa kifedha. Methali hii inambagua maskini na kumkandamiza kijamii kando na

kumwekea mipaka ya matangamano yake ya kimapenzi katika ujirani wa kimaskini kwa hofu ya mapenzi yake kutoonekana kwingineko.

*f) Cha mfupi huliwa kichwani*

Methali hii kama ilivyo katika methali ya *Cha mfupi huliwa na mrefu*, ufupi ni jazanda ya unyonge na inamaanisha kuwa mwenye nguvu hufaidi mali au jasho la mnyonge. Kufaidi huku ni haramu kwa kuwa jasho la mnyonge linafaa kumfaidi mwenyewe. Methali hii inalitaja jambo hili kwa urahisi unaoonyesha mwelekeo wa kutojali au zaidi kusherehekea hali yenyewe. Kwa misingi hii, methali hii ina dhima hasi katika hali kuwa haiwezi kulifaa kundi nyanyaswa katika muktadha wowote ule ila inalikejeli na kulivunja moyo.

*g) Dau la mnyonge haliendi joshi, likienda ni Mwenyezi Mungu kupenda / jahazi la mkata haliendi joshi/ la mnyonge haliendi joshi, likienda litazama/ Mtumbwi wa maskini huzama / Mashua ya mnyonge huzama mtoni / La mnyonge halina mashiko*

Dau ni aina ya chombo cha majini kama jahazi dogo kilichochongwa mbele na nyuma na ambacho hakina mirengu huku jahazi likiwa chombo cha majini kikubwa zaidi ya dau kilichotengenezwa kwa mbao ambacho hasa hutumika kuchukulia abiria. Kwenda joshi ni kwenda kwa kasi, joshi ikiwa na maana ya mwendo wa chombo wa kufuata upepo wa katikati. Chombo cha baharini kisipoenda joshi basi huenda demani yaani upande wa chombo usioelekea upepo ambao hufanya chombo kwenda mwendo wa polepole sana (kudema). Methali hizi zinaonyesha kuwa mtu maskini hana mwelekeo wala mafanikio ya haja katika mambo yake ya kimaisha kwa sababu ya uwezo wake mdogo. Akifanikiwa

huwa ni kwa kuhurumiwa na mwenyezi Mungu tu wala si kwa juhudi au uwezo wake mwenyewe. Zinamsawiri maskini kama kiumbe aliyechukiwa hata na Mwenyezi Mungu na ambaye hupata mabaki ya rehema za Mungu baada ya Mungu kuzigawa kwa tajiri. Hata hivyo, methali hizi hazitumiwi na matajiri pekee kuwadhalilisha maskini bali pia hutumiwa na maskini kutoa lalama zao wanapodhulumiwa kudhihirisha hali zao duni.

Aidha, methali hizi zinaonyesha chuki ya tajiri kwa maskini anayetapatapa kutafuta chake kwa kujaribu kumkandamiza kwa hali na mali. Kwanza, mnyonge hatarajiwi kuwa na dau au jahazi; anapolipata linasemekana kuwa halitaenda joshi na likienda joshi linasemekana litazama. Mnyonge anaposhinda kwa dau lake kutozama mwenye nguvu tena anamnyima sifa kwa kudai kuwa dau au jahazi hilo limeenda joshi kwa msaada wa Mwenyezi Mungu wala si juhudi za mnyonge. Kauli hii haifai kuchukuliwa kumaanisha kuwa maskini hautegemei msaada wa Mungu ila kuonyesha uonevu anaofanyiwa mnyonge hasa inapokumbukwa kuwa kwenda joshi kwa jahazi la tajiri (kwenda joshi kukiwa na maana ya kufanikiwa kwa lolote lile) hakunasibishwi na nguvu za Mungu ila uwezo wake mwenyewe. Mwelekeo na dhima ya methali hizi kwa maskini katika jamii ni hasi na haziwezi kutumika kwa njia ya kuwafaa wao katika muktadha wowote.

*h) Dua la kuku halimpati mwewe / Kuku akemea mnyakuzi anyakua*

Dua ni ombi. Katika dini zote dua zote huelekezwa kwa miungu au Mungu ambaye anaaminika kuwa anazijibu dua hizo kwa uwezo wake usiokadirika. Mwewe ni ndege mkubwa wa jamii ya tai ambaye hukamata na kula vifaranga wa kuku. Katika hali hii, mwewe ni mwenye nguvu, mkosa na muuaji kama wenye nguvu wengine katika jamii wanaowakilishwa naye wanadamu wakiwemo. Kuku hapa ni mnyonge anayewakilisha

wanyonge wengine wa kila nui. Kwa kawaida, wanyonge humwendea Mwenyezi Mungu kutatuliwa matatizo yao kwa kukosa njia mbadala. Ni udhalimu na uonevu uliokita mizizi kumwambia mnyonge kuwa licha ya kudhulumiwa kilio chake kwa Mungu nacho hakitasikika bila sababu ya kilio hicho cha haki kutosikika. Hapa wenye nguvu wanajisawiri kama wenye mamlaka katika nyanja zote za maisha, uungu ukiwemo, huku methali nzima ikionyesha matajiri au wenye nguvu za kifedha na kimamlaka katika jamii kama wenye kinga dhidi ya adhabu zozote duniani na ahera licha ya maovu wayatendayo. Methali hii inalimaliza tumaini la mwisho la kidini wanaloshikilia maskini kuwa japo duniani kuna uonevu ahera kutakuwa na haki kwa kuwaonyesha kuwa mwenye nguvu ana uwezo kila mahali jambo ambalo si kweli.

*i) Funika kombe mwanaharamu apite.*

Methali hii inaenda kinyume kabisa na methali isemayo *Kitanda hakizai haramu* na inatokana na itikadi hasi ya jamii ya kuwachukia wanaharamu. Mwanaharamu ina maana ya mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa au aliyezaliwa na mwanamke ambaye hajaolewa huku kufunika kombe ikiwa jazanda ya kuficha siri. Jamii ya Waswahili hasa ilikuwa na utamaduni wa kuhakikisha kuwa kila binti anaolewa akiwa bikira na ingefahamika kuwa mwanamwali yeyote ameharibu ubikira wake kabla ya kuolewa alikuwa anasitiriwa (kutafutiwa mume) kabla ya kupata mwanaharamu aliyechukuliwa na jamii kama aibu.

Kwa mujibu wa Abudu na Baruwa (1981:6), kwa mila za Kiswahili ni tusi kubwa na aibu mwanamke kuzaa bila kuwa na mume. Mtoto anayezaliwa hivyo huitwa ‘mwanaharamu’ na anapofanya lolote la ukosefu wa adabu au la aibu watu wanamkumbusha kuwa yeye ni mwanaharamu. Hakuna mwanajamii anayeamua atazaliwa na wazazi wa aina gani au

atazaliwa wazazi wake wakiwa katika hali gani ya kimahusiano. Isitoshe, si mtoto haramu bali kitendo kilichopelekea kuzaliwa kwake. Methali hii inaendeleza chuki ya jamii kwa watoto wasio hatia waliozaliwa katika hali hii kwa kuwanyima nafasi ya kujua siri za jamii na kuwabagua. Methali hii pia hutajwa kama *Fumba lako jicho mwanaharamu apite* au *Funika kaa mwanaharamu apite*.

*j) Jicho la mkata halioni, likiona haliongozi*

Methali hii ni mojawapo ya methali zinazomdhalilisha maskini na kuonyesha jinsi asivyoweza kufanikiwa kisha anapofanikiwa zinatafuta njia ya kumnyima sifa. Kwanza, methali hii inamnyima maskini uwezo wa kuona kwa kudai kuwa jicho lake halioni. Na badala ya kumpa sifa zake jicho hilo linapoon, linatafutiwa doa lingine kwa kuambiwa kuwa halioni dhahiri, haliongozi au haliangazi. Kuona kwa jicho hapa kuna maana ya kufanikiwa katika shughuli yoyote maishani. Methali hii ina mwelekeo hasi na dhima hasi kwa maskini kwa kuwadhulumu kwa kila juhudi watiazo maishani.

*k) Kuku wa mkata hatagi na akitaga hufa / Ya mkiwa haita na ikita hupapata.*

Methali sawa na hii kimaana husema *Kuku wa mkata hatagi, akitaga haangui na akiangua vifaranga hutwaliwa na mwewe*. Kati ya mengi waliyofanya wanajamii wa jamii za Kiafrika kujikimu kiuchumi, ilikuwa ni ufugaji wa kuku na mifugo wengine. Faida ya kuku huwa ni mayai yake ambayo yanaweza kuliwa na wanadamu au kuatamiwa na kuku ili kuangua vifaranga. Methali hii inahakikisha kuwa imefunga kila upenyu wa kuku wa maskini kuweza kuongezeka kwa njia ya kuangua vifaranga au kijumla bidii ya mnyonge kumzolea faida yoyote. Maonevu, ukandamizaji na chuki vinajidhihirisha kwa jinsi kila ufanisi wa maskini unavyotafutiwa mkasa wa kuuzima.

Kwa mfano, kuku wa mnyonge anasemekana hana uwezo wa kutaga, anapotaga anasemekana atalipiga yai (livunjike) na asipolipiga anaambiwa kuwa mwenyewe atakufa. Anaposhinda yote haya, inasemekana kuwa hataangua vifaranga na anapoangua inatabiriwa kuwa watatwaliwa na mwewe. Hivyo, methali hii imejaa chuki iliyo wazi kwa maskini na kwa sababu hiyo dhima yake ni hasi. Methali hizi huenda kinyume kabisa na methali zisemazo *Kuku havunji yayile, Teke la kuku halimwumizi mwanawe na Simba hamli mwanawe.*

*l) Maskini haokoti, akiokota kaiba*

Kando na kuwa methali hii inamwonea maskini pia imesheheni sifa za ubinafsi wa matajiri ambao wanaamini kuwa ndio pekee waliojaaliwa bahati njema na ufanisi maishani. Ubinafsi huo unawapelekea kumsingizia maskini wizi hata katika vitu ambavyo amejaaliwa na Molawe kihalali. Isitoshe, inausawiri umaskini kama laana kutoka kwa Mungu hivi kwamba hawezi kukubali bahati njema kumwendea maskini.

*m) Mkata hampendi mwana*

Hakuna asiyetaka kuwa na mtoto hata awe maskini kiasi gani kwa kuwa kupata mtoto si swala la kiuchumi bali la kijamii. Methali hii basi haimtendei haki maskini kwa kumkatia shauri kuwa hampendi mwana bila idhibati ya kusema hivyo. Kwa upande mwingine, 'penda' ina maana ya 'ingiwa na hisia za kuenzi au kuthamini mtu.' Ikiwa hii ndio maana ya kupenda, kila mtu anaweza kupenda, maskini wakiwemo, kwa kuwa kupenda hakujafungika katika uwezo wa kiuchumi.

n) *Mnyonge kupata haki ni mwenye nguvu kupenda*

Methali hii inaendeleza dhana potofu kuwa nafasi na haki zote duniani ni za matajiri na ikiwa maskini atapata haki yoyote atakuwa amepishwa na tajiri, mwenye nguvu. Kama binadamu aliyekamilika maskini japo hana pesa ana haki zake ambazo ametunukiwa kimaumbile na kisheria asizohitaji kuomba apewe na tajiri. Kwa misingi hii, methali hii inaonyesha mashauo ya matajiri katika kuringia uwezo wao ambao hasa huwa umetiwa chuku sana. Kwa sababu hiyo dhima yake hasa kwa maskini katika jamii ni hasi.

o) *Mnyonge msonge*

Kusonga ina maana ya kubana, kutaabisha au kulimbikizia matatizo mengi kwa wakati mmoja. Methali hii inachofanya hasa ni kumhimiza mwenye nguvu azitumie nguvu zake kumzidishia udhia mnyonge hivyo kumkosesha raha maishani bila kutaja sababu ya kufanya hivyo. Methali sawa na hii husema *Mnyonge mnyongeni*. Inatoa idhini ya mnyonge kunyongwa kwa kuwa tu ni mnyonge wala si kwa sababu ametenda uovu wowote. Methali hii ni chochezi na kandamizi kwa maskini na haiwezi kumfaa yeye kwa lolote. Haina huruma kwake ilhali kanuni za Grice zinataja kuwa matumizi ya lugha *yanafaa kuzingatia huruma kwa wengine*.

p) *Mtashi hana haya au kinyongo / Nisimbulie unipe mnyonge hana kinyongo.*

Kusimbua ni kuudhi au kuaibisha mtu. Kwa upande mwingine, kinyongo ni hali ya kuchukizwa na kitu, mtu au jambo. Methali hii inampa aliye na uwezo wa kifedha au kirasilimali uhuru wa kumkera maskini kwa vyovyote vile ili amkidhie haja yake eti kwa kuwa maskini hana kinyongo. Kwa kusema hivi, methali hii inamnyima maskini utu

wake na kumsawiri kwa sifa zisizoweza kuitwa hata za hayawani kwa kuwa hata hayawani wana kinyongo na kuna viwango vya dhalala ambavyo hawawezi kuvivumilia. Fauka ya hilo, methali hii inachochea chuki na kujenga viwango katika jamii ya binadamu kwa kuonyesha kuwa kuna wasiohimili kusimbuliwa na kuna waliozaliwa kuelekezewa simbulio. Methali sawa na hii husema *Mkata hana miiko*.

q) *Ng'ombe wa maskini hazai pacha*

Methali hii pia inaonyesha kuwa maskini ni mtu asiyeangukiwa na nyota ya jaha kwa kuwa ng'ombe wake huzaa ndama mmoja mmoja kwa hivyo mifugo hao huongezeka polepole sana. Ikiwa ng'ombe wa maskini hazai mapacha na mapacha huzaliwa hilo linaweza tu kumaanisha kuwa mapacha hao huzaliwa upande wa pili; kwa matajiri. Hivyo, methali hii ina uwezekano mkubwa wa kutokea kunakozaliwa mapacha. Ikiwa hili ni kweli, basi hii ni methali inayoonyesha mashauo ya matajiri kuringia utajiri wao. Jambo hili ni hasi kwa kuwa tunapotumia lugha kwa mujibu wa Grice tunafaa kupunguza sifa kwetu na kwa wengine lakini kwa wakati uo huo tuepuke kutowasifu wengine.

r) *Ya mkiwa haizai nyike/ jike*.

Methali hii inaweza kulinganishwa na methali kama '*Kuku wa maskini hatagi na akitaga haangui*.' Mifugo wote wa mkata wanatabiriwa kuwa hawawezi kuzaa jike. Methali hii ina shida na kuzaa jike kwa sababu jambo hili litamaanisha maskini atafanikiwa kwa urahisi kwa kuwa jike hao watazaa tena na tena na maskini ajikwamue umaskinini. Kwa kuwa tajiri hataki jambo kama hili kutendeka, anaomba ikiwa kitendo cha kuzaa kitatendeka kamwe miongoni mwa mifugo wa maskini basi wazae dume ambao hawawezi kuzaa tena ila tu kuchinjwa. Methali hii pia ni onevu kwa maskini.

### 3.3.2 Methali zinazochoea vita, fitina na uhasama

Hizi ni methali zinazofarakanisha jamii kwa kuleta ugomvi, utesi na uadui kati ya wanajamii hasa palipo na kutoelewana. Zinatekeleza jambo hili kwa kutoa maneno yenye chuki, uchongezi na uchochezi huku zikidai kuwa vita ndio suluhu ya pekee kwa matatizo yanayohusiana na kutoelewana kati ya wanajamii. Aidha, baadhi ya methali hizi humwasa mwanadamu kuwa asikubali kulipa uovu kwa wema au aghalabu kusamehe bali zinamhimiza aliyetendwa asisahau na ahakikishe kuwa amelipiza uovu aliotendewa kwa uovu zaidi. Nasaha za kijamii na kidini huhimiza kuwa wanadamu wanafaa kusameheana kwa kuwa ikiwa kila mmoja atalipiza kisasi tukio husika litajirudia milele na kuishia kuwahumiza watu wengi zaidi. Kwa mtu mmoja au kundi moja husika kusamehe hata hivyo, msururu mzima wa uovu hukatika. Baadhi ya methali hizi ni kama;

*a) Amani haiji ila kwa ncha ya upanga/ Suluhu haiji ila kwa ncha ya upanga.*

Methali hii inajidhihirisha kuwa inarejelea muktadha wa kale kutokana na matumizi yake ya silaha ya vita (upanga) ambayo haitumiki sana vitani katika enzi hizi ambapo teknolojia ya kivita imefikia kiwango cha kutumia bunduki, mabomu na silaha zingine kubwa na haribifu. Kuna uwezekano kuwa methali hii imetokana na dini. Katika dini ya kiislamu Muhammad (SAW) kulingana na maagizo aliyopokea kutoka kwa *Allah* aliwaruhusu waumini kupigana iwapo adui atawaletea fitina hadi pale amani itakapopatikana (Quran 2:191-193). Vivyo hivyo, Quran (4:95) anawamiminia sifa wanaoenda vitani na kujitolea kuumia kwa kusema kuwa wao wana tunu kwa Mwenyezi Mungu huku ikiwabeza wanaofanya uamuzi wa kutoingia vitani.

Siku za hivi karibuni kumekuwa na uhasama kati ya mataifa na makabila tofauti kote ulimwenguni kwa sababu mbalimbali. Uhasama huo umeishia katika mapigano na kusababisha mali nyingi kuharibiwa na watu wengi kupoteza maisha kwa sababu ya makundi husika kuamini kuwa wanaweza tu kupata haki kupitia kuwapiga na kuwashinda wenzao. Katika kutoa matumizi ya methali hii King'ei na Ndaluu wanaibua ukinzano wake mkubwa unaoifanya kupoteza dhima yake katika jamii au kuwa na dhima hasi. Wanasema '*Methali hii inapigiwa mtu anayestaajabu ni kwa nini watu au mataifa hupigana na kupata hasara kubwa. Mtu kama huyo huwa amesahau kuwa mapatano hutokea pia. Vile vile, huambiwa mtu anayetegemea maneno kuleta suluhu katika jambo.*'

Japo wataalamu hawa wana ukweli katika kusema kuwa ndani ya vita huja suluhu, jambo linaloungwa mkono na nadharia ya Udenguzi ambapo inaamini kuwa hali mbili kinzani huwa katika hali ya kuwepo na ku(to)kuwepo, jambo la muhimu zaidi ni kuwa hata vita viwe vikali vipi suluhu hupatikana katika maneno wala si ncha ya upanga. Haiwezekani kwa makundi mawili hasimu kupigana na kupata suluhu ya ugomvi wao kuko huko vitani bali suluhu hupatikana kupitia viongozi wao ambao hukutana na kujiingiza katika vita vya maneno ambayo huleta suluhisho. Methali hii inawapotosha watu kumalizana katika juhudi za kutafuta amani jambo ambalo haliwezekani asilani. Japo wengi wa waumini wameitetea methali hii kwa kusema kuwa 'ncha ya upanga' haimaanishi vita vya moja kwa moja bali jambo lolote linaloweza kuleta suluhu, uhasi wa methali hii hauupi uchanya nafasi ya kushamiri kwa kuwa inachochea vita moja kwa moja.

b) *Asiye mali hasidi wa mwenye mali*

Hasidi ni adui. Kwa hivyo methali hii inamaanisha kuwa maskini na tajiri ni maadui hasa kwa maskini kumchukia tajiri. Japo maskini na tajiri hawahusiani kwa karibu kutokana na hali zao za kiuchumi kuwa tofauti, haimaanishi kuwa wana uhasama kwa kuwa wao hufaana hasa kikazi ambapo maskini humfanyia tajiri kazi naye akalipwa malipo yanayomsaidia maishani. Bila tajiri maskini hana kazi na bila maskini kazi ya tajiri haifanyiki. Uhusiano wao huu haufai kutiwa nyufa na methali kama hii inayomwonyesha tajiri kuwa maskini ni adui yake. Methali hii basi inahatarisha uhusiano kati ya tajiri na maskini na kujenga uhasama kati yao jambo linaloifanya dhima yake kuwa hasi. Aidha, methali hii pia inajenga utabaka katika jamii.

c) *Anayenyolewa kwa chupa hasahau*

Kigae cha chupa kinapotumiwa kunyolea nywele huwa ni kifaa butu sana hivyo husababisha anayenyolewa kuhisi uchungu sana. Kunyolewa kwa chupa katika muktadha huu kunarejelea kutendwa ubaya kwa hivyo methali hii inasema aliyetendewa ubaya hasahau. Maadili ya kijamii hutufunza kusamehe na kuwa si vizuri kupoteza wakati katika ulipizaji kisasi kwa kuwa *yaliyopita si ndwele tunafaa tugange yajayo*. Hakuna uhakika pia kuwa hatutaumizwa zaidi katika juhudi zetu za kulipiza kisasi kando na kuwa hakutakuwa na kikomo cha kutenda uovu kwa kuwa kila anayetendwa hatasahau bali atalipiza kisasi.

d) *Akutendaye mtende, usimche akutendaye.*

Methali hii inatumia lugha kali isiyo na hata chembe ya huruma wala utu. King'ei na Ndalu (keshatajwa) wanaeleza matumizi ya methali hii kama *tusiogope kuwalipa maadui zetu kwa ubaya kiasi walichotutendea*. Naye Wamitila (keshatajwa) anaeleza matumizi yake kama *tusichelee kuwalipa ubaya waliotutendea ubaya*. Ikiwa walivyoeleza wataalamu hawa ndivyo methali hii inavyofaa kutumiwa, dhima yake ni hasi kwa kuwa inawachochea watu wapigane na kuumizana bila nafasi yoyote ya kusameheana. Wanadamu kote duniani wakifuata nasaha hii potofu ulimwengu mzima unaweza kuangamizwa kwa muda mfupi sana kwa kuwa wanaotutenda uovu ni wengi. Vivyo hivyo, hakutakuwa na maana ya methali kama *Adui mpende.*'

### 3.3.3 Methali za vitisho

Uhasi mkubwa wa methali za aina hii ni kuwafanya watu wawe na wasiwasi wa usalama wa maisha yao na shughuli zao kwa hatari isiyo halisi bali ya kukisia tu. Wasiwasi huu huwafanya watu kuishi kwa kutotulia na kufanya kazi zao kwa hangaiko la moyo huku wakitazamia hatari kila wakati. Baadhi ya methali katika kategoria hii aidha, hutoa vitisho kwa kutumia utabiri. Kutabiri ni sawa na kutoa habari au kueleza mambo yatakayotokea baadaye kwa kutumia uwezo wa aina fulani hasa wa kiganga na kichawi. Uganga wa kutabiri na unajimu ulikuwa jambo la kawaida kwa Waswahili. Aghalabu Waswahili walienda kwa waganga kutafuta habari njema za usoni za maisha yao au ya jamaa zao au kutafuta ikiwa kuna baya linaelekea kuwakumba ili wajiepushe nalo. Kwa kujiegemeza katika dhana hiyo ya utabiri, methali hizi hutumia maisha ya usoni ambayo jamii haina uhakika wa jinsi yatakavyokuwa kuwatisha wengine na kuwavunja moyo

kwa sababu hasi. Fauka ya hayo, baadhi zinatumia ubaya wa wazazi kuwatabiria wana mabaya. Ni vyema kujua kuwa kila mtu ana maisha yake na nyota yake na haiwezekani kutumia maisha ya mtu mmoja kutabiri maisha ya mwenzake kwa kuwa mikondo ya maisha hayo ni tofauti. Methali hizi ni kama;

a) *Adhaniaye amesimama aangalie asianguke.*

Kabla ya kutoa kitisho, sehemu ya kwanza ya methali hii inautilia shaka ufanisi wa mrejelewa. Haielekei kuamini kweli amesimama japo amesimama. Inaanza kwa kumvunja moyo mhusika na kumfanya kuzishuku juhudi na ufanisi wake hivyo kurudi nyuma. Fauka ya hayo, sehemu ya pili inasema *aangalie asianguke* ikiwa na maana kuwa kuna uwezekano wa juu sana wa mhusika kuanguka. Japo sehemu hii ya pili inatoa tahadhari nzuri, inaielekeza makini na nguvu za mhusika katika kujizuia kuanguka badala ya kujiendeleza zaidi. Inatabiri kushushwa na kuporomoka badala ya kuhimiza ufanisi zaidi. Kutokana na jambo hili dhima ya methali hii ni hasi.

b) *Adui ukimtahadhari mara moja rafiki utamtahadhari mara mia.*

Katika saikolojia kuna ugonjwa wa '*paranoia*' ambao ni 'wazimu usiotibika wa kujiona unaonewa kila wakati.' Japo ni kweli maadui zetu wanaweza kutuumiza bila kuwashuku, ni jambo la kutilia chuku kuwatahadhari mara mia zaidi ya maadui zetu kwa kuwa makini yote tutakayotumia katika kutia tahadhari itatugeza kuwa watumwa wa uoga kwa marafiki hao na hivyo wagonjwa wa kuogopa kutendwa. Methali hii ni chochezi na imejaa kasumba inayotokana na athari za kisaikolojia kutokana na matukio machache maovu yaliyowahi kuwakumba baadhi ya wanajamii. Hii ni methali inayowaelekeza wanajamii katika adui mkubwa zaidi wa maisha ambaye ni woga. Inajitokeza popote

penye urafiki na kuleta kushukiana hivi kwamba urafiki huo hauwezi kudumu au unaendelea katika hali ya tashwishi. Ni vyema kufahamu kuwa shughuli nyingi katika maisha ya mwanadamu huendeshwa kupitia ushirikiano na hali ya kuaminiana na kwa kiwango kikubwa maisha ya mwanadamu huwa mikononi mwa mwanadamu mwenzake hasa rafiki. Kwa mantiki hii, nia ya methali hii ni kuleta kufarakana katika jamii kwa kuzua jakamoyo kati ya marafiki kwa sababu ya kuogopana na kushukiana. Inajenga mpaka wa kutoaminiana na kuutia urafiki wao doa. Hivyo, ina mwelekeo hasi kwa urafiki katika jamii na dhima hasi kwa jamii kwa jumla.

*c) Utajiri ni raha ya leo, mateso ya kesho ahera.*

Ahera ni makazi ya roho za wanadamu baada ya kufa kwao hadi siku ya kiama. Hii ni mojawapo ya methali zinazotumiwa na watu wenye nia ya kuwanyanyasa maskini hasa wahubiri kuwafanya maskini waridhike na umaskini wao kwa tumaini la maisha mema ahera huku wakingojea kwa udi na uvumba siku watakyowaona matajiri wakiteseka ahera. Maskini wanafanywa kuamini kuwa utajiri wao wa ahera ni bora zaidi ya wa duniani wanaoukosa kwa kuwa utajiri wa ahera ni wa milele.

Katika dini ya Kiyahudi, Kiislamu na Kikristo maskini wamesifiwa sana kuwa watu wema na kuwa itawawia rahisi sana kuingia peponi huku matajiri wakisawiriwa kama watu ambao hawataingia peponi au wakiingia itakuwa kwa shida sana. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuwa ni rahisi kwa ngamia kupenya katika tundu la sindano zaidi ya tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu (Mathayo 19:24). Kwa upande mwingine, hadith za Mtume Muhammad (SAW) zinasema kuwa maskini wataingia peponi miaka arobaini kabla ya matajiri huku *Mujahideen* maskini wakiingia peponi miaka elfu tano kabla ya

matajiri (Mishkaat Masaabeeh nambari 5235). Bila kutoa kufuru, ahera ni dhana ambayo inadumu katika imani ya kidini wala si mahali mahsusi panapojulikana na kudhibitika kuwa ni pa raha kwa maskini na karaha kwa tajiri. Kando na hilo, vitabu vitakatifu vinataja uongovu na utakatifu kama sharti la kuingia peponi wala si utajiri au umaskini. Hivyo, kando na kuwapa maskini matumaini ya uongo na kuwafanya kubakia katika hali duni methali hii inawabagua na kuwatisha matajiri kwa mateso ya ahera kwa sababu tu ya utajiri wao wala si makosa yoyote waliyotenda.

*d) Wakimbia kufiwako wenda kuliwako nyama.*

Hulka moja bora zaidi ya binadamu ni kuwa na utu na kuoneana huruma. Si jambo la kusherehekea kuona binadamu mwenza anakumbwa na tatizo moja baada ya lingine. Hata hivyo, methali hii inatolewa kwa njia inayoonyesha kusherehekea hali kuwa mhusika amekimbia kufiwako lakini anaelekea kuliwako nyama kwa hivyo atakumbwa na mauti liwe liwalo. Kifo ni hali inayohitimisha maisha ya mja na inayoogopwa na kila kiumbe kwa kuwa matokeo yake hayarekebishiki. Kutishia mtu kwa jambo kama hilo basi ni kuumumiza moyo na hakufai kwa lolote.

*e) Mahaba ya wanadamu si mambo ya dawamu.*

Mahaba ni mapenzi au hisia za kuthamini mtu au kitu. Aghalabu kati ya viumbe wote binadamu ndiye aliyeumbwa na hisia za mapenzi kwa mwenzake au wenzake. Mapenzi ndiyo msingi wa jamii kwa kuwa ni kupitia kwayo ambapo ndoa huwa, na ni katika ndoa ambapo watoto huzaliwa na kukiendeleza kizazi. Pia, ni katika kuwa na mapenzi kwa binadamu wenza ambapo mtu huweza kutoa msaada kwa wenzake. Watu kupendana na baadaye kukosana basi, hakuna maana kuwa haiwezekani kwa binadamu kupendana

mpaka kifo kiwatenganishe kama wanavyoapa harusini na pia hakuwezi kuchukuliwa kumaanisha kuwa hakuna wanadamu wawili wamewahi kuwa na mapenzi ya aina hiyo. Kudumisha mapenzi kunahitaji kujitolea kwingi pamoja na kuwa na matumaini ya kuweza kuyanawirisha mapenzi hayo hata zaidi siku za usoni. Kando na kutabiri maovu, methali hii inawavunja moyo wapenzi wanaofanya juhudi kuyadumisha na kuyanawirisha mapenzi yao kwa kuwaambia kuwa juhudi hizo ni za bure kwa kuwa hakuna mapenzi yanayoweza kudumu.

*f) Aliye juu mngoje chini*

Uhasi wa methali hii unategemea matumizi yake. Kwa kawaida methali hii inatumiwa kumaanisha kuwa aliye mahali juu ngazini ama mtini lazima wakati mmoja atashuka. Kuzingatia maana hii, methali hii inawanasihi wenye vyeo au waliofanikiwa kiuchumi kuwa wasiringe kwa kuwa wanaweza kushuka chini kwa vyeo au mali kuisha jambo ambalo ni la kweli na muhimu sana. Hata hivyo, methali hii inaweza na inatumiwa na watu wenye nia mbaya kuwavunja moyo waliofanikiwa katika maisha ambao wana wivu nao kwa kuwatisha na utabiri kuwa aliye juu atashuka tu. Vitisho hivi huwafanya baadhi ya 'walio juu' kupoteza mwelekeo wao na kuishia kweli kushuka chini. Visipofikia kiwango hiki vitisho hivyo vinaweza kuwafanya watu hawa kuishi kwa woga wa kufilisika au kupoteza vyeo, hivyo kupungua kwa utendakazi wao kwa kukosa makini inayohitajika.

*g) Mwenda Pate harudi kirudicho kilio*

Pate ni mji ulio kaskazini mwa pwani ya Kenya karibu na mji wa Lamu. Miji ya Pate, Mombasa na Lamu ilikuwa ikipigana sana na kuvamiana kwa silaha kali kuanzia miaka

ya nyuma hadi mwanzoni mwa karne ya ishirini (Biersteker na Shariff, 1995). Methali hii ilitajwa kwanza kabisa kama *Mwenda Pate kauya kiuyacho kiriro*, matamshi yanayoendana moja kwa moja na sarufi ya lugha za Kimijikenda hasa lugha ya Kigiriama. Inasemekana methali hii ilitokana na kisa cha kweli ambapo watu wa Mombasa walipanga kwenda Pate kupigana na watu wa huko zama hizo Mombasa ikijulikana kama ‘Kisiwa cha Mvita’ kutokana na vita vingi kupiganwa humo. Walitayarisha silaha kama bunduki, risasi, nyuta, mishale na mikuki na kuwachukua Wagiriama wengi kwenda kuwasaidia vitani. Walipofika Pate, walipata Wapate wamejihami kuwaliko na wakashindwa vitani huku wapiganaji wao wakifa kwa wingi sana hasa Wagiriama. Baada ya vita hivi pakawa na matanga katika takriban kila familia Kisiwani na zaidi miongoni mwa Wagiriama walio karibu na kisiwa. Kisa hiki kikawa chanzo cha methali hii baadaye. Hata hivyo, ni wachache wanaofahamu kisa hiki japo methali iliyozalishwa nacho inajulikana. Hii ni methali inayosifia uhodari na uwezo wa kivita wa Wapate kwa kusema kuwa anayethubutu kuivamia Pate hawezi kurudi bali kirudicho ni kilio tu kinachoashiria kifo chake. Kwanza, methali hii inataja habari za vita na vifo vya watu kama jambo ambalo ni la kujivunia sana na linalofaa kuupa mji wa Pate sifa. Kinyume cha matarajio ya jamii, methali hii inasherehekea vifo vya watu. Jambo hili linachochea hisia za kivita hasa kwa Wapate dhidi ya miji mingine ili kudumisha sifa yao ya kuwa bora kivita na kwa miji mingine dhidi ya Pate ili kuwanyanganya nafasi hiyo. Vita vyote hivi vinasababisha vifo vya wanadamu jambo ambalo ni hasi. Kwa upande mwingine methali hii inaleta vitisho na kujenga woga kwa wasafiri wanaoelekea Pate kwa kuwatabiria kuwa hawatarudi wao bali habari za vifo vyao tu. Mwisho, inaitenga Pate na miji mingine kimahusiano hivyo ni hasi kidhima.

*h) Bendera ipepeayo sana mwishowe huchanika.*

Kazi ya bendera au beramu ni kupepea. Ikiwa bendera inapepea haraka au polepole haiwezi kudumu milele bali lazima ichanike wakati mmoja. Vivyo hivyo, wanadamu wanapofanya kazi ikiwa wanafanya polepole kwa kuogopa kuchosha miili yao au kuogopa kuzeeka haraka ukweli ni kuwa kwa vyovyote vile uzee na kuchoka vitatufika sote. Ni vyema kujitolea kabisa kufanya kazi aliyotengewa mtu bila kuzembea. Methali hii inatabiri uovu kwa kudai kuchanika kwa bendera na wakati uo huo kutishia wanadamu kutoachia nguvu zao zote kazini kwa hofu ya kuzeesha miili yao haraka. Methali hii ina uhasi sawa na *Ngoma ikilia sana mwisho hupasuka kiwambo.*

*i) Kilichomla baba na mwana kitamla*

Wamitila na King'ei wakishirikiana na Ndalul katika kamusi zao tofauti wanaeleza maana ya methali hii kifupi kuwa “kilichoweza kumdhuru baba lazima kitamdhuru mtoto.” Aghalabu mtu hudhuriwa kukiwa na sababu ya kufanywa hivyo japo hata katika hali hii kumdhuru mtu hakufai. Ikiwa baba alidhuriwa lazima kulikuwa na sababu ya kufanywa hivyo. Isitoshe, hali kuwa baba amedhuriwa; yaani ameuawa ni uchungu mkubwa kwa mtoto ambaye ama ameachwa na mama pekee au ni yatima. Hivyo, kupoteza baba ni adhabu tosha kwa mtoto huyu anayeteseka kwa kosa asilolijua. Kutabiri kuwa kicho hicho kilichomdhuru baba kitamdhuru na huyu mtoto ni uhayawani uliokita mipaka kwa kuwa kunampotezea matumaini ya kuishi kando na kumfanya kuishi kwa wasiwasi na woga wa kuvamiwa. Vile vile, si haki kwa methali hii kuchukulia hali ya mtoto kulipia makosa ya baba au kutumiwa kulipiza kisasi kwa baba kama jambo ambalo halina kizuizi kwa kuwa ni la kawaida.

*j) Mtenda mema kinyuki jazaye hulipwa moto.*

Jaza ni zawadi, fadhili au thawabu hasa inayohusisha malipo mema kutoka kwa Mungu sababu ya kutenda wema. Mtu anapotenda wema aghalabu hutarajia kulipwa kwa wema unaohusisha shukrani za maneno au vifaa wala si uovu. Methali hii hata hivyo inadai kuwa anayetenda wema huishia kulipwa kwa uovu kama nyuki anavyolipwa kitendo chake cha kutengeneza asali kwa uovu wa kuchomwa moto na binadamu anapoirina asali yake. Kwa kusema hivi, methali hii inawavunja moyo wanajamii katika vitendo vyao vya utendaji wema kwa kuwa hawatarajii chochote kizuri kutokana na wema wao bali uovu tu. Jamii nzima ikifuatia mwelekeo huu wa maisha hapatakuwa na yeyote aliye tayari kumfaa mwenzake kwa kuwa tayari wamejazwa kasumba kuwa malipo hayatapendeza. Kwa upande mwingine, la mno ni kutenda wema wala si kulipwa kwa wema, mantiki inayoungwa mkono na msembo wa Kiswahili '*Tenda wema wende zako.*' Jambo hili limaanisha kuwa umuhimu wa utendaji wema hauko katika malipo bali katika utendaji wenyewe.

*k) Anayepandisha wengine hupigwa teke menoni.*

Kupandisha hapa kuna maana ya kuwasaidia wengine kukwea ngazi ya ufanisi katika maisha. Kufanikiwa kunanasibishwa na kupanda ngazini ambapo anayepandisha analazimika kuwa chini ya anayepandishwa pindi anayepandishwa anapofika juu. Ikiwa anayepandisha wengine huishia tu kulipwa kwa hila ya kupigwa teke menoni inalotuambia methali hii ni kuwa tusiwapandishe wenzetu; yaani tusiwasaidie. Methali hii inawahimiza wanajamii wasiwasaidie wenzao asilani kwa kuwatisha na uchungu wa kutendwa pindi wanayemsaidia anapofanikiwa. Japo watu kweli husaidiwa wakaishia

kuwaumiza waliowasaidia hatufai kuwa na kasumba kama hii kwa kuwa itatufanya tusiwasaidie hata wale waliokuwa waifae jamii halafuye.

*1) Fadhila ni utumwa.*

Fadhila ni wema, ukarimu, hisani au jamala huku utumwa ukiwa hali ya kummiliki mtu kama mali. Kwa hivyo, inalosema methali hii ni kuwa kutenda au kutendewa wema ni mamoja na kumilikiwa. Hakuna mwanajamii anayefurahia kitendo cha kumilikiwa na mwenzake kwa kuwa jambo hilo linamaanisha anayemiliki ana uhuru wa kumfanya lolote. Methali hii inawahimiza wanajamii kutowatendea wenzao fadhila wala kukubali kutendewa fadhila kwa kutoa vitisho kuwa watakuwa watumwa. Ikiwa kutakuwa na jamii ya watu wasiotendeanan hisani basi, watu hao bila shaka watakuwa wanatendeanan kinyume ambacho ni uovu na jamii hiyo itaumizana wala haitaendelea.

### **3.3.4 Methali zenye taathira za uovu**

Sifa au hulka zinazohusisha uovu huigwa wala hazipiti kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kama vilivyo virusi vya ugonjwa. Kuna nafasi ya kufanya uchaguzi wa ama kuiga au kuacha kwa kuwa ni vigumu mtu kulazimishiwa tabia. Hivyo, ujumuishaji wa kuwa tabia ya mtu mmoja katika kundi nzima la watu inawakilisha tabia ya kundi nzima haina ukweli wowote ila tu upotoshi. Baadhi ya methali katika kundi hili pia huwaonyesha watumiaji lugha kuwa kutenda uovu si neno mradi kunawaletea manufaa huku zingine zikiweka pesa mbele ya wema na utu kwa kusawiri kuwa pesa zikiwemo haina haja ya kutafuta uungwana.

Isitoshe, hulka mojawapo hasi ya binadamu ni kujaribu kuepuka lawama na adhabu hata katika hali ambapo ni wazi kuwa ndiye mkosa. Takriban binadamu wote wakipata nafasi ya kutorokea au kuelea adhabu baada ya kufanya uovu watachukua fursa hiyo. Wanadamu hivyo hutumia methali za aina hii kujaribu kuficha maovu waliyoyatenda ama kwa kuyarahisisha au kulaumu majaaliwa ambayo hayawezi kuulizwa kujitetea. Methali hizi ni kama;

a) *Samaki mmoja akioza huoza wote / Pono mmoja akioza huoza shazile*

Shazi ni mtungo wa samaki wengi waliofungwa pamoja hasa kwa kamba baada ya kuvuliwa. Katika methali hii, samaki ni kiwakilishi cha watu huku harufu ikiwakilisha tabia zisizopendeza. Methali hii ina maana kuwa mtu mmoja akiwa na tabia isiyofaa katika kundi la watu kundi nzima litakuwa na tabia hiyo. Kama ilivyotajwa awali, tabia haipiti kama virusi kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine bali huhusisha uamuzi wa mwigaji. Maelezo haya hayana maana kuwa tabia ya mtu mmoja haiwezi kuliharibu kundi bali kupinga ujumuishaji hakika unaofanywa na methali hizi bila kuacha upenyu wa hata mtu mmoja kutoathirika kwa kuwa hata katika hali ya kawaida ya uvuvi mitungo huweza kuwa na samaki mmoja au wachache walioza huku wengine wakiwa wazima kabisa. Maitaria (1991) akiishughulikia methali *Samaki mmoja akioza huoza wote* kwa mtazamo wa kiisimujamii anasema kuwa:

“Hii ni methali ambayo haionyeshi ukweli wowote hasa hali halisi ya maisha inapozingatiwa. Kwa mfano, Waswahili au watu wenye kuishi kandokando ya bahari, ziwa au mto hufahamu kwamba samaki wachache wanaweza kuoza lakini pia wanafahamu kuwa kuna wengine wangali hai, wengine wanazidi kuvuliwa na kuuzwa sokoni.”

Japo Maitaria anaitetea methali hii baadaye yaliyosemwa awali yanaonyesha kuwa methali hii haina ukweli wa kuaminika kwa wanajamii.

*b) Mtoto wa nyoka ni nyoka.*

Wamitila (keshatajwa) katika kamusi yake ya methali anaeleza matumizi ya methali hii kwa kusema kuwa mtoto wa mtu mwenye sifa mbaya huishia kuwa na sifa mbaya. Mwelekeo huu kwa wanajamii si tu potoshi na usio na idhibati bali pia unaobeba uongo na unaoweza kupelekea watu wasio hatia kuadhibiwa na hata kuuawa. Kumekuwa na visa vingi hivi karibuni ambapo mwanafamilia mmoja anaikosea jamii nayo jamii inalipiza kisasi kwa kuiangamiza familia nzima au wanadoa wanakosana kisha mmoja wao anamuua mwenzake pamoja na watoto kwa imani kuwa watachukua hulka za marehemu anazochukia. Ni vyema kufahamu kuwa japo wana hurithi baadhi ya hulka za wazazi, kila mtu ameumbwa kipekee na anafaa kuhukumiwa kwa vitendo vyake wala si vitendo vya wazazi au jamaa zake wengineo. Kwa kutoa dai hili methali hii inaielekeza jamii visivyo.

*c) Hakuna mchele usiokuwa na ndume*

Kama ilivyotajwa awali jamii nyingi za Pwani zilikuwa na utamaduni wa kulima mpunga na chakula chao hasa kilikuwa wali. Kwa hivyo, katika uvunaji wao wa mchele pamoja na kuutayarisha ili upikwe walikumbana sana na ndume. Ndume ni chembe za mchele zenye maganda ambazo hazikutwangika. Pia huitwa chuya. Katika maana yake ya ndani methali hii inamaanisha kuwa katika kila kundi la watu wema lazima pawe na mbaya. Japo kweli chuya hupatikana sana katika mchele si jambo lisilowezezana kutoa chuya zote na kubaki na mchele safi kabisa. Vivyo hivyo, japo makundi mengi ya watu huwa na

watu wachache wabaya inawezekana kuwarekebisha wabaya wote na kuwaondoa wengine hivyo kubaki na jamii safi au kundi safi la watu wema tu. Si haki kwa methali hii kudai haiwezekani kupata kundi la watu lisilo mbaya kwa kuwa ukweli ni kuwa inawezekana. Methali hii inaijumlisha jamii nzima au makundi yake katika kapu moja la kuwepo wabaya ilhali kuna makundi yaliyoasilika na yaliyo safi kabisa.

*d) Ukila pamwe na namiri igiza zake desturi*

Namiri ni chui jike ambaye huwa mkali sana hasa katika uwindaji. Chui hasa huwinda wanyama dhaifu kama swara na paa na ulaji wake huhusisha uuaji. Uhasi wa methali hii unatokana na hali kuwa inatushauri tuige tabia za chui anayewaangamiza wenzake. Kwa kuiga hulka zake inamaanisha chui hufanya jambo la kujivunia. Swali la kujiuliza hapa ni je, lazima tuige kila linalofanywa na wenzetu liwe nzuri au baya? Kwa kutumia mfano huu pia methali hii inahalalisha kitendo cha namiri cha uuaji pamoja na viumbe wengine wanaowakilishwa naye wanadamu wakiwemo. Huku ni kuipotosha jamii.

*e) Ungwana haufai bora ni ndarama.*

Ndarama au darahima ni pesa / fulusi. Methali hii inadai kuwa uungwana yaani kuwa na tabia njema zinazokubalika katika jamii hakuna thamani yoyote mbele ya umiliki wa pesa. Kwa kutoa dai hili methali hii inaonyesha uroho na umero wa wenye pesa wa kutaka kujinyakulia zaidi na zaidi hata kwa kutumia njia zisizolengana na maadili ya kijamii. Inahalalisha mbinu za kihuni za kuzalisha mali nyingi huku binadamu akipoteza utu na maadili ya kijamii. Hii ni methali yenye dhima hasi kwa jamii, na haiwezi kuifaa jamii inayotaka kukikuza kizazi chake kimaadili.

*f) Waovu wana maisha marefu.*

Methali hii inasifu uovu kwa kudai kuwa waovu ndio hujaaliwa kuishi miaka mingi duniani. Jambo hili linaweza kufasirika kwa kifupi kwa upande mwingine kuwa watu wema hufa mapema. Kufuatia ufasiri huu methali hii inatuhimiza tuwe waovu kwa kuwa hulka moja inayowaunganisha wanadamu wote ni hofu kwa kifo na mapenzi kwa maisha marefu. Licha ya kasumba potofu za methali hii, dini huitetea kwa madai kuwa kauli kama hizi zinapatikana katika vitabu vitakatifu. Katika Biblia Takatifu (Isaya 57:1-2) nabii Isaya anasema kuwa mtu mtakatifu hufa haraka kama njia ya kumwepusha na majanga na kumwingiza katika utakatifu. Quran Takatifu pia inataja jambo linalokaribiana na hili (Quran 46: 15 na 16). Dhana hii ni potofu kwa kuwa ikizingatiwa na wanadamu katika juhudi za kutafuta maisha marefu dunia itajaa zogo na vurumai.

*g) Mwana mtukutu hali ugali mtupu.*

Neno mtukutu katika methali hii limefafanuliwa na Wamitila (2001) kuwa halikutumiwa kwa maana mbaya bali maana nzuri katika juhudi za kuipa methali hii dhima chanya. Visawe vya neno hilo vinavyopeanwa na Mohamed na Mohamed (1998) hata hivyo ni msumbi, mtundu, mnumanuma, mgobo, mshari, mtiriri, mtesi, mgomvi, harabu, matata, nunda, habithi, gwagu na harashi. Kati ya maneno yote haya hakuna hata neno moja ambalo lina maana nzuri. Hivyo, methali hii inawanasihi wana kipotofu kwa kuwaonyesha kuwa utukutu unaweza kuwaletea faida ilhali ukweli ni kuwa utukutu huleta hasara na kilio kwa mhusika na jamaa yake.

*h) Ajali haina kinga / Ajali haikingiki / Cha kuzama hakina rubani / Cha kuzama hakina usukani*

Kama ilivyotajwa awali Waswahili waliamini sana katika maajaliwa na kudura ya Mwenyezi Mungu kama inayoendesha na kuamua hatima ya maisha ya mja. Karama na Saidi (1983) wakieleza maana ya methali *Ajali haina kinga* wanatoa madai kuwa Mungu akitaka ufikwe na ajali au jambo hakuna la kukukinga; utafikwa tu na jambo hilo. Vivyo hivyo, wakieleza maana ya methali "*Cha kuzama hakina rubani*" wanadai kuwa chombo kilichojaaliwa kuvunjika na pengine kuzama kitavunjika tu na hata rubani afanye nini hataweza kukisaidia kisivunjike. Waumini wa dini mbalimbali japo humwomba Mungu kwa njia tofauti wote huamini kuwa wanamwomba Mungu mwema ambaye hawaelekezi maovuni bali wemani; Mungu anayewawazia wema. Kwa kuwa vitendo vinavyotajwa kuwa havizuiliki katika methali hizi vyote ni vibaya tena vinavyoweza kusababisha vifo vingi haibainiki wala kumkinika ni vipi waumini wanamtarajia yule yule Mungu mwema kuwajalia maovu. Japo hatukusudii kumsawiri Mungu kama asiye na nguvu za kutenda chochote kimpendezacho, haielekei kueleweka kutoka katika methali hizi linalosababisha Mungu awajaalie wanadamu hawa mawi bila kutenda ubaya wowote. Inaelekea kuwa, methali hizi zinatumia jina la Mungu asiyekuwepo kujitetea bila shaka kuhalalisha kutowajika na kutojali kwa wanadamu ambako hatimaye husababisha ajali za vyombo vya usafiri au zingine zozote zitokee. Zinatumika kuficha makosa ya mwanadamu yaliyosababisha ajali kutendeka kwa kuzinasibisha na kudura ya Mwenyezi Mungu. Kando na hayo, zinawakatisha tamaa wanadamu katika juhudi zao za kuzuia ajali zinazowakumba kila uchao. Zinawahitimishia kwa njia hasi kwa kuwaambia kuwa juhudi zao hizo wanazofanya ni za bure kwa kuwa bado ajali zitatokea kwa kuwa hayo ndiyo

mapenzi ya Mungu. Swali la kujiuliza hapa ni je, waumini wanamwamini Mungu anayewalipa kwa uovu na machungu?

*i) Bibi wa ovyo hupata mume mzuri.*

Waswahili walikuwa na utamaduni wa kuwaasa na kuwafundisha wana wao wa kike jinsi ya kuwa wake wazuri wanaopendeka na waume na kuheshimiwa na jamii. Jambo hili lilikuwa muhimu katika jamii kiasi kuwa wanawali waliwekwa chini ya kungwi wakiwa wadogo na hata kutawishwa ili “wasiharibike”; wasiwe wanawake wa ovyo. Methali hii ina maana kuwa mwanamke mwenye sifa mbaya huishia kupata mume mzuri. Tukizingatia utamaduni uliotajwa kuwahusu Waswahili na jinsi walivyowatunza wanawali, utamaduni ambao ulikuwepo katika baadhi ya jamii zingine za kiasia pia, methali hii ni potoshi kwa jamii na hasa kwa wanawake. Jamii inachukulia makosa ya kitabia kwa wanawake kwa uzito zaidi ya wanaume na kuna uwezekano mkubwa wa mwanamke anayejulikana kuwa na tabia mbaya kukosa wa kumwoa kabisa au kuishia kuolewa na mtu aliyekosa mwanamke wa kuoia kutokana na uduni wake wa kiuchumi au kiafya. Swali la kujiuliza hapa ni je, ikiwa bibi wa ovyo hupata mume mzuri, kwa nini jamii inatia juhudi sana kuhakikisha kuwa binti zao wana tabia njema? Kwa upande mwingine, binti aliyetambulika kuwa alikuwa ameupoteza ubikira wake Uswahilini alitafutiwa mtu wa kumwoa (kumsitiri) haraka iwezekanavyo. Mbona jambo hili lilitendeka badala ya kungoja tabia yake mbaya impe mume mzuri? Hali zote hizi zinaonyesha kuwa methali hii haina ukweli wowote bali upotoshi na dhima yake katika jamii ni hasi.

*j) Kiingiacho mjini si haramu*

Methali hii imetokana na utofauti wa uwezo wa kiushawishi katika jamii kati ya watu wa mijini na mashambani kwa sababu za kiuchumi na kiutawala. Mijini ndiko huishi watawala na wenye mali hivyo watu wenye ushawishi katika jamii tangu enzi za kale pwani na hata bara. Hivyo, jambo likikubalika na watu wa mjini watu wa mashambani hawana budi bali kulikubali kwa kuwa limeshahalalishwa na wenye uwezo wa kuishawishi jamii. Methali hii ina maana kuwa kitu au tabia inayoanza mjini huweza kusambaa kwa watu wote kwa haraka na hata kilichoonekana kibaya hubadilika na kukubalika na kitu kinapofanywa na watu wengi huwa vigumu kupingika na kuharamishwa. Jambo la kutilia maanani hapa ni kuwa wingi wa watu wanaofanya jambo fulani mbaya pamoja na usuli wao havibadilishi hali ya kitu; ikiwa ni kibaya kinabakia vivyo hivyo. Madhara ya ubaya wa kitu pia hayabadiliki hata kitu hicho au tabia ikikubalika kwa watu wote duniani. Athari zake zinabakia kuwa zile zile. Kwa mfano, kilugha cha sheng kimekuwa kikipingwa sana nchini Kenya kwa kuwa kinahitilafiana na sarufi ya Kiswahili. Japo kilugha hiki kinatumika sana mijini na mashambani kwa sasa hakiwezi kukubalika kama sehemu ya Kiswahili sanifu kutokana na idadi ya wazungumzaji kwa kuwa idadi hiyo haibadilishi ukweli wa uduni wa kilugha hicho. Methali hii ni potoshi hasa kwa vijana ambao mara nyingi hukimbilia kitu kwa kuwa wengi wanajihusisha nacho hususan watokao mjini. Ni vyema kuwalea vijana na wanajamii wote wakiwa na uhuru wa mawazo na uchaguzi kiasi kuwa wanajihusisha na tabia fulani kwa misingi ya manufaa yake kwao wala si kwa kuangalia tabia hiyo inafanywa na nani.

*k) Kufa kwa wengi ni harusi*

Kama ilivyosemwa awali kifo si jambo mojawapo linalofanyiwa mzaha na jamii kwa kuwa kinapoinyanganya wapendwa wao hakiwarudishii tena wala hawana uwezo wa kujua linalowatendekea huko waendako. Hawana uhakika hata kama watawahi kuonana tena; kuonana tena ni swala la imani tu wala halijadhibitishwa. Isitoshe, haiwezekani kwa wanadamu kuzoea kifo kiasi kuwa hakiwaumizi mioyoni mwao. Jambo hili ni sawa na matatizo mengine yote yanayomkumba mwanadamu kando na kifo. Binadamu hakuumbwa katika ukamilifu wa kuzoea shida bali kila tukio jipya la shida humuumiza upya. Haimkiniki ni vipi methali hii inadai kuwa kifo cha wengi ni harusi. Hakuna jamii ya watu ambayo inaweza kusawasisha kifo na harusi kiwe cha mtoto malaika, mtu mzee zaidi, au hata mwenda wazimu. Ikiwa kifo cha mtu mmoja tu kinaleta huzuni katika jamii haiwezekani kwa vifo vingi kuleta raha kwa kuwa kila msiba una huzuni wake. Methali hii ni hasi katika hali kuwa inalifanyia mzaha swala la kifo ambalo huleta majonzi sana kwa wanajamii kiasi kuwa hawalijadili ila tu katika muktadha unaolazimu.

Methali hizi huwahimiza wanajamii kujijali wao bila kumfikiria mtu mwingine yeyote yule. Zinaonyesha kuwa kila mtu anafaa kuujali ufanisi wake akichukua nafasi yoyote atakayopata kuwadhulumu wengine na kujipatia zaidi. Aidha methali hizi huonyesha kuwa wanaowasaidia wenzao wanafanya kitendo cha kijinga na watakuja kupata hasara kubwa kutokana na jambo hilo. Methali hizi ni kama:

*l) Kila mwamba ngoma huvuta kwake.*

Methali hii inaonyesha ukawaida wa kila mtu anayefanya jambo fulani kutaka kujifaa yeye kwanza. Japo baadhi ya watu kweli hujifaa wao kwanza wanapopata nafasi ya

kufanya jambo, si vizuri kulipigia jambo hilo mifano kama linalofaa. Aidha, methali hii inatukumbusha kuwa tujinufaishe vya kutosha kibinafsi kabla ya kuwafikiria wenzetu kila tunapopata nafasi ya kufanya hivyo. Huu ni ushauri potoshi ambao hauwezi kuifaa jamii kwa vyovyote vile kwa kuwa walio na nafasi kama vile za uongozi wataishia kujitajirisha kwa mali ya umma na kuwaacha walio wengi wakiangaika. Inapendekeza kuwa watu wawe na mapendeleo katika ugawaji wa raslimali na huduma kwa wanadamu wenzao pindi wapatapo nafasi ya kuongoza au kushikilia wadhifa wowote unaowaweka katika kitovu cha ugawaji wa mali ya umma. Hii ni njia hasi ya kuikuza na kuijenga jamii hasa katika karne hii ambapo takriban kila nchi duniani inapigana na ufiisadi na ukabila na wakati mwingine uchumi wa nchi nyingi kulemazwa na viongozi ambao wanawajali jamaa zao na makabila yao tu.

*m) Aliyeshiba hamkumbuki mwenye njaa.*

Japo methali hii inatunasihi tusiwategeme wengine ambao ni matajiri bali tujitegeme wenyewe nasaha ambayo ni nzuri, pia inamhalalishia 'aliyeshiba' ubinafsi wake wa kutomkumbuka 'mwenye njaa' jambo ambalo ni hasi.

*n) Asiyejua maana haambiwi maana.*

Miongoni mwa mengi waliyofaana nayo wanajamii ilikuwa ni kuelimishana kuhusu maswala mbalimbali ya kijamii. Wazee hasa walikuwa na jukumu kubwa la kukielimisha kizazi cha baadaye maswala ya kijamii ambayo hawakuyajua lakini yalikuwa na umuhimu katika kuiendeleza jamii. Takriban kila tambiko katika jamii huambatana na mafunzo ya aina fulani ambayo yote ni muhimu kwa jamii. Aidha, haijalishi ikiwa anayefahamishwa anajua maana au hajui ila kwa kuwa ni mwanajamii lazima

afahamishwe maana husika kwa kuwa bila hivyo ataachwa nyuma na jamii na kwa njia hiyo ataivuta jamii nzima nyuma. Kutomjuza mwanajamii mmoja asichojua na kinachofaa kujulikana na jamii nzima si tu kumbagua na kuwa mbinafsi bali kuichongea jamii nzima kwa kuwa maangamizi yanaweza kutokea kupitia kutojua kwake.

*o) Asiyekuwapo na lake halipo / Asiyekuwapo machoni na moyoni hayupo*

Ni kawaida ya wanajamii hasa Wapwani hadi sasa kufanya kazi kwa pamoja kisha kugawa mapato yao baadaye. Kwa mfano, ni nadra sana kupatikana mvuvi anayevua samaki peke yake ila wavuvi wengi huvua pamoja kisha kugawa samaki watakaopata au pesa zitakazotokana na uuzaji wa samaki hao baadaye. Hii ndio sababu Waswahili wana methali kama *Kuvua numbi si kazi, kazi ni magawioni*. Ikiwa methali hii inashauri kuwa *Asiyekuwapo machoni lake lisiwepo* basi inawahimiza wanajamii kuwa dhalimu kwa wenzao ambao watafanya kazi lakini wasiwepo magawioni kwa sababu moja au nyingine. Jambo hili si haki kamwe na likizingatiwa na jamii linaweza kuleta kutoelewana kwa hali ya juu pamoja na kuvunja utendakazi wa pamoja unaowasaidia wanajamii kutekeleza kazi zao kwa urahisi. Aidha, uhasi mkubwa wa methali hii ni kuwahimiza wanajamii kuwa wabinafsi nafasi inapojitokeza.

*p) Alalaye usimwamshe, ukimwamsha utalala wewe.*

Wanajamii hutegemeana katika kufaana kwa jambo moja hadi lingine kwa kuwa kila mmoja ametunukiwa uwezo wa aina yake na hakuna mwanajamii ambaye anaweza kujitosheleza kwa kila hali. Katika kusaidiana huku wanajamii hulazimika kusaidia hata pasipo kuitishwa msaada kwa kuwa tatizo la mwanajamii mmoja ni tatizo la jamii nzima kutokana na kuwa mwanajamii huyo ni sehemu ya jamii na akiumia jamii nzima inaumia.

Pia, athari za tatizo lake zinaweza kuishia kuikumba jamii nzima. Wamitila (keshatajwa) akieleza maana ya methali hii anatoa ufafanuzi ‘*usijishughulishe na mtu aliye katika ujinga au hali fulani usije ukalaumiwa wewe.*’ Mwelekeo kama huu kwa jamii yoyote ile ni hatari sana kwa kuwa kila mwanajamii akiufuatilia dhana ya jamii itakufa hatimaye. Haiwezekani kwa dhana ya jamii kuwa hai ikiwa wanajamii hawajishughulishi na maswala yanayowakumba wenzao; yaani ikiwa wao ni wabinafsi. Hivyo, methali hii ni hasi kidhima kwa kuwa inahimiza ubinafsi na uchoyo.

### **3.3.5 Methali zinazodhihaki ulemavu**

Lugha ya Kiswahili imekashifiwa sana kwa maonevu yake kwa walemavu katika matumizi ya msamiati kama kipofu, kiziwi, kiwete, kiguu n.k ambao ni wanajamii wenye maumbile ya kipekee na mahitaji maalum lakini wanaonekana kama wenye udhaifu. Kulemaa ni kuwa na upungufu hasa katika kiwiliwili cha mtu kwa kuzaliwa, ugonjwa au ajali. Hakuna aina ya ulemavu isiyokuwa na changamoto na aghalau jamaa wenye mlemavu huona aibu na ugumu wa kumshughulikia. Swala hili si la kupigiwa mifano ovyo bali la kuonewa imani na kupewa moyo. Methali zilizo katika kategoria hii ni:

*a) Bibi mzuri hakosi kilema / Kizuri hakikosi ila*

Methali hii kwanza inajipinga yenyewe; ina sehemu mbili kinzani. Sehemu ya kwanza inadai kuwa bibi mhusika ni mzuri kisha sehemu ya pili inasema ana kilema. Ikiwa vipimo vya uzuri vilizingatiwa kabla ya uamuzi wa uzuri wake kutolewa bibi huyu hana kilema na ikiwa bibi huyu ana kilema asingepita vipimo vya uzuri kwa kuwa kilema chake kingeonekana. Tukizingatia kuwa imetajwa kwanza kuwa ni mzuri tunaweza

kuhitimisha kuwa anayemlimbikiza ulemavu uwe ni wa kisura au kitabia anafanya hivyo kumwaribia sifa zake za awali. Hata hivyo, uhasi wa methali hii unatokana hasa na hali ya kutumia ulemavu kupigia mfano jambo linaloonyesha ubaguzi na dhalala kwa walemavu.

*b) Akipenda chongo huita kengeza*

Chongo ni mtu aliyelemaa jicho hivi kwamba halioni na kengeza ni jicho lenye mboni iliyokwenda kombo / upande. Methali hii inachoonyesha moja kwa moja ni kuwa watu wenye matatizo haya ni muhali kupendwa. Inaona ajabu kwa mtu kumpenda chongo na hivyo inadai kuwa anaita kengeza ambaye kwa mujibu wake ana afadhali. Kando na kuwadhalilisha walemavu, methali hii inawabagua kwa kuwasawiri kama watu wa kitengo tofauti na binadamu wa kawaida jambo ambalo si kweli. Mwelekeo wake kwa watu wa aina hii ni hasi, kwa hivyo dhima yake ni hasi.

*c) Mke kipofu ni mwaminifu.*

Kipofu ni mtu asiye na uwezo wa kuona. Methali hii pia inaweza kupigiwa upato kama iliyo na mwelekeo chanya na inayompa sifa nzuri kipofu lakini inamdhalilisha zaidi ya kumpa sifa. Ni unafiki na matusi kudai kuwa upofu humpa mke uaminifu unaosakwa na kila mume kwa mkewe ilhali ni nadra kupata mume anayetaka kumwoa mke kipofu au kumpofusha aliye naye ili awe mwaminifu. Kwa upande mwingine, japo ni kweli mke kipofu anaweza kuwa mwaminifu kwa kuwa hawezi kwenda mbali peke yake na hawaoni wanaume, kumkumbusha kuwa uaminifu wake umeletwa na upofu kunaleta fasiri mbili hasi. Kwanza, kunamaanisha kuwa mke huyu si mwaminifu ila tu kwa sababu ya upofu wake na kupoteza upofu wake kunaenda sambamba na kupoteza uaminifu, na pili wake

wote ambao si vipofu si waaminifu kwa kuwa upofu ndio huleta uaminifu kwa wake. Mwelekeo huu ni wa kuipotosha jamii wala hauifai kwa lolote.

### 3.3.6 Methali zinazohujumu sifa njema

Hizi ni methali zenye uchoyo wa sifa. Methali hizi hujaribu iwezekanavyo kutafuta ila hata isipokuwa na zinapoikosa zinahitimisha kwa kudai tu kuwa vyema hivyo havitadumu bila kutoa sababu maalum. Kando na kuwa madai yanayotolewa na methali hizo si ya kweli, hazitoi suluhu za kufanya vyema hivyo visikumbwe na maovu zinayotaja. Methali zilizo katika kategoria hii ni kama;

#### *a) Chema hakidumu / hakikai/ hakina maisha*

Methali hii inachomaanisha ni kuwa kitu au mtu ambaye ni mzuri wa sura, tabia au matendo hakai kwa muda mrefu. Kitu au mtu kama huyo hufa na kuwaacha wabaya. Ikiwa kifo chake kinasababishwa na hao wabaya au kinatokea tu si swala la kutilia maanani bali swala kuwa amekufa na ni kawaida kwa mtu kama huyo kufa. Ni wazi kwa mujibu wa methali hii kuwa, kuwa mwema ni sawasawa na kujitakia kifo kwa kuwa kifo huendea wema kwanza tena mapema. Kila mwanadamu ameumbwa na woga mwingi kwa kifo. Hakuna hata mwanadamu mmoja awe mtoto, kijana au mzee anayeweza kuifuata njia anayojua fika kuwa itamletea kifo kwa kuwa uchu wa mwanadamu kwa uhai ni mkubwa mno. Kifo ndicho adui mkubwa wa mwanadamu kwa kuwa kinapomchukua mmoja wao akimrejeshi tena daima wala hakuna njia ya kujua anayopitia alikoelekea. Kwa methali hii kudai kuwa wema hawakai inatunasihi moja kwa moja tuwe na hulka zisizovuta kifo; yaani tuwe waovu au wabaya. Dai hili likizingatiwa basi jamii

itaoza na kuharibika kwa maovu yasiyokoma kwa juhudi za mwanadamu kuepuka kifo cha mapema. Kwa mintarafu ya jambo hili, methali hii ina dhima hasi kwa jamii.

*b) Ivumayo haidumu*

Wamitila (keshatajwa) akieleza matumizi ya methali hii anasema;

“Aghalabu mtu anayependwa huwa haishi kwa muda mrefu kama ilivyo kitu kinachopendwa sana.”

Yasichotaja maelezo haya ni kinachofanya mtu au kitu hiki kisidumu. Je, sifa njema huleta kifo? Bila shaka hapana. Kwa hivyo, methali hii inaeneza tu propaganda kando na kuwatishia kwa hofu ya kifo watenda mazuri wanaopendwa na jamii hivyo kuwanyima nafasi ya kuwahudumia wanajamii zaidi na kuendelea kuwa maarufu na kupendwa zaidi. Isitoshe, methali hii inaonyesha chembe za wivu kwa huyo au hicho kivumacho kutoka kwa walioshindwa kuvuma. Ni kutokana na hasira na kuvunjika moyo kwa kushindwa ndipo washinde wanakuja na msemu kama huu kama njia ya kupunguza ari ya mshindi. Methali hii imechochewa na wivu na haiwezi kuifaa jamii kwa vyovyote.

*c) Akusameheaye deni amekunyima mkopo.*

Deni ni kitu anachodaiwa mtu kinachoweza kuwa pesa au mali. Kwa upande mwingine, kusamehe deni ni hali ya mtu kuacha kwa hiari kudai deni kutoka kwa mdeni wake. Ni muhimu kusisitiza hapa kuwa kusamehe hakulazimishwi bali hutokea kwa mapenzi ya mtu mwenyewe. Mtu kama huyu (anayesamehe) anafaa kushukuriwa na sifa zake za wema kusambazwa kote katika jamii kwa kuwa yeye ni mfano bora kwa wanajamii wote. Ieleweke pia kuwa, ikiwa anayedaiwa amesamehewa deni alikuwa ameshindwa kulilipa na kwa kuwa hali yake ya uchochole haijabadilika anaweza kulazimika kumwendea yuyu

huyu aliyemsamehe ili ampe deni lingine. Ni kitendo cha utovu wa shukrani na juhudi za kuwakosanisha mdeni na mkopeshaji kudai kuwa kusamehe deni ni sawa na kunyima deni. Kusema hivi ni kujaribu tu kumnyima mkopeshaji mwema sifa zake za kuwa karimu na mwenye huruma kwa wenzake. Kando na hilo, methali hii inamvunja moyo katika utenda wema wake na inaweza kumfanya kutowafaa wenzake maadamu hata wanapopewa hawashukuru.

### 3.3.7 Methali za kukatisha tamaa

Baadhi ya methali hizi huonyesha wazi kuwa kuzembea na kutia juhudi au bidii maishani ni mamoja kwa kuwa ufanisi hautegemei juhudi. Ikiwa ujumbe unaopitishwa na methali hizi ni kweli basi i wapi sababu ya kufanya kazi au kutia juhudi kazini? Methali hizi huchukulia ufanisi kama mchezo wa bahati nasibu ambapo yeyote anaweza kuwa mshindi jambo ambalo halitendeki kimantiki. Mifano ya methali hizi ni kama;

a) *Bahati humwacha wa mbele na kumfuata wa nyuma.*

Bahati ni jambo jema, nasibu, neema au jaha. Kwa kawaida wanadamu hunga'ang'ana ili kupata bahati. Hii ndio sababu katika Kiswahili kuna methali kama *Mgaagaa na upwa hali wali mkavu, Mtembea bure si mkaa bure huenda akaokota*, na *Achanikaye na mpini hafi njaa* miongoni mwa zingine. Hivyo, kila mtu hujitahidi kuwa wa mbele ili bahati iwe yake hasa katika ulimwengu wa sasa uliojaa mashindano. Kudai kuwa hiyo bahati inayosakwa kwa juhudi zote hizi itamwacha wa mbele na kumwendea wa nyuma basi ni kumvunja moyo na kumkatisha tamaa mwanajamii anayefanya kila juhudi kupata ufanisi maishani. Kwa upande mwingine, methali hii inaweza kuhalalisha ufisadi na mapendeleo

kwa waliotumia mbinu hizi kuuiba ufanisi kwa kuitaja katika kujitetea kwao. Methali hii ni hasi kidhima.

*b) Bidii ya mja haikidhi haja.*

Kila mwanadamu anapokua tangu akiwa na umri mdogo, wakubwa humnasihi kuwa anafaa kuweka jitihada maishani ili afanikiwe. Wanaoonekana kuwa na jitihada zaidi hupewa hongera kwa kuwa hayo ndiyo matarajio ya jamii na ndiyo njia pekee ya kuiimarisha jamii. Kila linaloonekana sawa na la kupendeza katika jamii limetokana na bidii ya mwanajamii mmoja au kundi la wanajamii. Kutokana na jambo hili kumwambia mwanajamii yuyo huyo kuwa bidii yake haitakidhi haja kwa sababu yoyote iwayo ni kumvunja moyo na ni jambo lisilofaa. Methali hii inaweza kupunguza jitihada za wanajamii kwa kuwa ikiwa juhudi zao hazitafua dafu basi hawana haja ya kufanya bidii.

*c) Mungu humpa alalaye na aliye kitako.*

Methali hii imeegemezwa katika imani ya majaaliwa. Hatuwezi kubaini kikamilifu mbinu anazotumia Mwenyezi Mungu kuwatunuku watu riziki maishani kwa kuwa jambo hili linahitaji uwezo wa kiungu. Hata hivyo, vitabu vitakatifu humnasihi mwanadamu kuwa asiwe mzembe bali afanye kazi. Biblia takatifu hata inadiriki kusema kuwa asiyefanya kazi asile (Wathesalonike 2 3:10). Kutokana na jambo hili, kudai kuwa Mungu humtunuku alalaye (asiyefanya kazi) na aliye kitako yaani anayetarazaki ni kumvunja moyo anayefanya kazi. Ana haja gani ya kufanya kazi na kuchoka ikiwa jaza yao kwa Mungu ni moja?

Kwa mujibu wa imani inayotokana na dini hasa ya Kiislamu, ambayo Waswahili ni waumini wake, methali hii inamaanisha kuwa Mungu humpa mtu atafutaye na asiyetafuta; Mungu humkidhia kila mtu haja zake. Maelezo haya hayana nia ya kuonyesha kuwa Mungu hana uwezo wowote au hamkidhii mwanadamu haja zake bali kuonyesha kuwa methali kama hii inaweza kuzua kasumba za kizembe na kuwafanya watu wasitie bidii maishani. Swala hapa ni je kuna haja gani ya kutoa jasho ikiwa aliye kitako pia atapata?

*d) Amechagua nazi akapata dafu.*

Aghalabu mwanadamu huchagua kwa lengo la kuhakikisha kuwa amejitwalia kilicho chema na kitakachomfaa kulingana na mahitaji yake. Ni kawaida kwa wanadamu kuchagua kila kitu katika maisha kwa kuwa uhalisi wa maisha ni kupata vyema vikiwa vimechanganyika na viovu au hata viovu vikiwa vimejitia sura ya vyema. Dafu ni tunda la mnazi linalokaribia kuwa nazi au ambalo halijakomaa na lililojaa maji ndani huku nazi ikiwa tunda la mnazi lililokomaa linalotokana na dafu. Katika jamii zilizo na utamaduni wa kutumia nazi katika mapishi, nazi ndio hutoa tui nzuri inayofaa kuungia mchuzi wala si dafu. Watu hasa wanawake wanaponunua nazi huitikisa kwanza kama njia ya kujua ikiwa imekomaa au ni dafu. Swala la kuchagua ni muhimu katika ununuzi na matumizi ya nazi katika mapishi. Kumdhihaki mtu kuwa juhudi zake za kuhakikisha kuwa amepata nazi zimeambulia kumpa dafu ni kumvunja moyo. Katika uwanda mzima wa maisha pia kumwambia mtu kuwa juhudi zake za kupata kilicho chema kiwe kazi, mume, mke, nguo, nyumba au kitu kingine chochote kile zimeambulia patupu kwa njia ya kumdhihaki ni kumkatisha tamaa. Kando na hilo, methali hii inawavunja moyo wanaonua kupenya

katika swala husika kuwa wasichague bali wajitwalie chochote kitakachojileta kwao. Mtazamo kama huu katika maisha ni hasi kwa kuwa vyema ni vichache maishani na uchaguzi wa kina unafaa kuhimizwa. Methali hii ina uhasi sawa na methali isemayo *Mchagua nazi hupata koroma.*

*e) Cha mwerevu huliwa na mjinga*

Kuwa na ujinga ni hali ya kutojua kitu fulani; ni sawa na kuwa mpumbavu. Kwa upande mwingine mwerevu ni mtu mwenye kutumia akili kwa makusudi ya kupata haja yake japo wakati mwingine werevu hudaiwa kutumia hila. Mwanadamu ni kiumbe mvumbuzi na anayependa kusaili mambo kwa lengo la kujitoa ujingani. Hakuna mwanadamu anayependa ujinga wa kutofahamu chochote maishani kwa kuwa kujua ndiko huleta maendeleo katika maisha ya kibinafsi na ya kijamii. Kwa kawaida mjinga huelekezwa na mwerevu katika kujua asichojua. Kwa hali ya ujinga na werevu kuwepo lazima mjinga awe amepungukiwa na ujuzi wa jambo fulani ambalo mwerevu analifahamu. Haiwezekani mjinga yuyo huyo kumpiku mwerevu na kumnyanganya chake. Ikiwa atafanya hivyo, hawezi kuitwa mjinga tena kwa kuwa lazima ametumia werevu wa aina fulani kujipatia kitu hicho. Kando na kukiuka mantiki, methali hii inahalalisha unyanganyi na ulaghai. Inataja kitendo cha mjinga kula mali ya mwerevu kama jambo la kawaida na la kujivunia.

*f) Jitihada haiondoi kudura*

Kwa mujibu wa Knappert (1979) kudura inaonekana kuwa motifu bia inayofumana na mithiolojia ya Waswahili pamoja na maisha yao kijumla yawe yanaegemea dini au kilimwengu. Wanaamini kuwa Mungu humpangia kila mtu kudura yake na anaweza

kuikatiza wakati wowote anaotaka. Maisha ya kila kiumbe hupangwa karne nyingi kabla ya kuzaliwa kwake na kila kitu katika maisha hayo kuwekwa wazi ikiwa ni pamoja na chakula chake cha kila siku na vitu vingine vidogo anavyohitaji mtu maishani ambavyo mtu huvipata kutegemea mapenzi ya Mwenyezi Mungu mwenyewe. Hakuna kinachosadifia maishani mwa mwanadamu bali kila kitu huwa kulingana na mpango wa Mungu. Hata kifo kinapotendeka vitani kwa mfano, Waswahili huamini kuwa risasi hiyo ilikuwa 'imeandikwa jina la marehemu.' Kwa kutaja methali hii kama inayovunja moyo hatukusudii kumaanisha kuwa hakuna Mungu wala Mungu hana uwezo wowote juu ya maisha ya mwanadamu bali lililo wazi ni kuwa kuweka imani zetu katika methali kama hizi kunaweza kutukatisha tamaa maishani na kupunguza juhudi zetu za kutafuta riziki. Kando na hilo, methali hizi zinaweza kuwa msingi wa kuhalalisha tabia zisizofaa katika jamii pamoja na uzembe kwa kudai kuwa hiyo ndiyo kudura yetu huku waliofanya juhudi na kufanikiwa maishani wakinyimwa sifa kwa kudaiwa kuwa si juhudi zao bali wamejaaliwa ufanisi.

Methali hizi zinamsawiri binadamu kama kiumbe hoi kabisa asiyeweza kuubadilisha mkondo wa maisha yake katu na anayefaa kukaa kitako na kungoja litakaloamuliwa mbinguni. Katika Bibilia Takatifu (Mhubiri 6: 10) Nabii Suleiman anadai "Kila kitu kimeamuliwa. Inajulikana tangu zamani kila mtu atakuwa na hatima gani. Kwa hivyo haina haja ya kumlalamikia Mungu kuhusu hatima yako." Mawazo yanayokaribiana na haya yanapatikana katika waumini wa dini ya Kiislamu kwa kuwa imeandikwa kwamba hakuna janga linaloweza kutokea katika dunia au roho za waja ikiwa halikuandikwa kabla ya kutendeka kwake; kwa kuwa jambo hili ni rahisi sana kwa Allah (Quran 57:22).

Ujumbe wa methali hizi umeibuliwa, kukuzwa na kuwekewa mizizi thabiti na maandiko haya na mengine hivyo kuwafanya waumini wengi kuuamini ujumbe huo na kuufuatilia. Hata hivyo, isidhaniwe kwamba utafiti huu unalenga kuupuuza maandiko ya kidini bali kutanabaisha kuwa kuweka imani katika methali kama hizi hurejesha nyuma juhudi za mwanadamu kutarazaki na kujiimarisha kimaisha. Ikumbukwe kuwa, hakuna mwanadamu anayejua majaaliwa yake kwa hivyo ni jukumu lake kujaribu mikondo tofauti ya maisha aone ikiwa majaaliwa yake yamewekwa upande huo. Japo dini hutuambia kuwa Mungu anajua ‘leo’ na ‘kesho’ yetu ni jukumu la mwanadamu kuisaka ‘kesho’ aliyojaaliwa kwa kutia bidii maishani. Methali zenye maana sawa na hii ni kama *Liandikwalo halifutiki, Liandikwalo lina mhuri, Liandikwalo ndilo liwalo, Liandikwalo kuwa halina uzio, Wino wa Mungu haufutiki na Ulitakalo hupati hupata hujaaliwalo.*

### **3.3.8 Methali zinazohimiza unyonge**

Kwa mujibu wa McLellan (1973) akirejelea mawazo ya Karl Marx, dini ni kama bangi kwa binadamu. Anasema kuwa dini imeibuka kutokana na tamaa ya mwanadamu kufidia maisha ya kutengwa. Dini inatumiwa kuwazuzua watu kwa kuwashawishi kuwa wote wako sawa mbele ya Mungu; maskini na tajiri. Wanaomiliki nyenzo za uzalishaji mali hutumia kanuni zinazoambatana na dini ili kuwafanya maskini wasilalamikie hali zao za umaskini (Wolf 2010:3). Zipo methali za Kiswahili zenye sifa hii. Methali hizo hujaribu kumwonyesha maskini kuwa mbele ya Mwenyezi Mungu hana tofauti na tajiri na wakati mwingine hata kumwonyesha kuwa yeye ni bora kumliko tajiri kwa kuwa hali yake ya umaskini itamzolea mahali pema peponi huku tajiri akisawiriwa kama aliyelaaniwa kwenda jahanamu. Matumaini haya ya pepo humfanya maskini kuvumilia dhuluma za

matajiri ambao humtumia kujitajirisha zaidi huku akijizuia kulalamika asije akawa na hatima moja na tajiri ambaye anamhurumia sana kwa kukubali kuwa na mali ya duniani na kukosa raha ya pepo. Katika hali yake ya kulewa imani na kasumba za dini, maskini huishi katika matarajio daima huku akijiambia kuwa kukosa mali duniani si neno kwa kuwa kunamhakikishia utamu wa raha ya peponi.

Methali hizi hutatua matatizo ya maskini kwa kuwahimiza kuegemea unyonge wao na kutojitetea. Zinawahimiza watosheke tu na umaskini kwa kuwa zinaonelea kuridhika huko ni kwema. Lengo la methali hizi hasa ni kuwapa maskini moyo katika matatizo wanayokumbana nayo ila zinafanya hivyo kwa njia ya kuwaletea udhaifu zaidi na kufungua njia za kuleta udhalilishaji zaidi kwa kuwa zinawahimiza kutojitetea au kuuchukulia ubaya waliotendewa kama wema ilhali wanajua fika kuwa si wema. Methali hizi zinaepuka ugumu wa maisha ambapo inabidi maskini ang'ang'ane ili atatue matatizo yake kwa kumwambia kirahisi kuwa ama aukubali uovu aliotendewa au amwache tu mwenye nguvu apate kilichokuwa haki yake (maskini) bila ya yeye kukipigania. Aidha, zinazichukulia shida za maskini kama majaaliwa na kuwahimiza kuzikubali hali zao duni kwa kuwa ndio majaaliwa yao. Ikiwa wanyonge watakuwa na mwelekeo kama huu katika maisha kila mtu atachukua nafasi hiyo kuwanyanyasa kwa kujua kuwa hawatajitetea. Methali hizo ni kama;

*a) Kila likuepukalo mwanadamu lina heri nawe*

Mtu anaposema kuwa kitu kimemwepuka inamaanisha kuwa amekuwa akikitafuta kitu hicho. Nia yake imekuwa kukipata kitu hicho wala si kuepukwa nacho. Haiwezekani hivyo, kuepukwa na kitu hicho kukawa heri katika misingi yoyote ile. Kukuita kuepukwa

nacho heri ni kutumia unafiki kuepuka uchungu. Methali hii inawafanya wanajamii kuishi maisha ya unafiki wa kujifanya kuwa hawajadhulumiwa ilhali ni wazi kuwa wamepitia dhuluma. Hii ni mbinu isiyoweza kuwasaidia wanyonge kujikomboa unyongeni ila kudidimia humo zaidi. Hivyo, dhima yake katika jamii ni hasi.

*b) Mtaka mbele mpishe*

Ikiwa anayeelekezewa methali hii anaambiwa ampishe anayetaka mbele, inamaanisha kuwa yeye yu mbele tayari na anashauriwa ampishe wa nyuma nafasi yake. Kuiacha nafasi yake ya mbele kunamaanisha kuwa mhusika atachukua nafasi ya nyuma. Kwa kawaida walio katika nafasi za mbele ndio hunufaika kwa urahisi kwa kuwa mazuri huwapata wao kwanza ndio sababu mhusika alikuwa ametangulia huko. Ikiwa mhusika aliye mbele alikuwa amejitahidi hadi akaangukia nafasi hiyo ina maana kuwa aliitaka na kumshauri kumwachia wa nyuma vivi hivi si haki. Kando na hili, methali hii inawahimiza watu kuzembea tu kwa kuwa watapishwa na wenzao. Aidha, ikiwa tunayeshauriwa kuachia nafasi ya mbele ni mwenye nguvu methali hii inahalalisha kitendo cha wenye nguvu kujinyakulia nafasi bora za wanyonge kimabavu jambo ambalo ni hasi.

*c) Aliyekunyoa shungi kakwepushia kuchana.*

Shungi ni nywele ndefu zinazoangukia katika kipaji cha uso. Ikiwa mmiliki wa shungi amezikuza nywele zake hadi kufikia kutengeneza shungi ina maana kuwa alikuwa na haja nazo na hakutaka kuzinyoa kwa kuwa angefanya hivyo kitambo. Vivyo hivyo, lazima amepitia shida nyingi katika juhudi za kuzikuza nywele hizo. Madai kuwa aliyemnyoa shungi lake amempunguzia mzigo wa kuchana ni unafiki unaonua kupunguza uchungu

wa kupoteza shungi lililokuwa linathaminiwa sana na mmiliki wake. Kwa upande mwingine, mwenye shungi hakuwa analalamikia urefu au uzito wa shungi lake kwa hivyo hajaonyesha haja ya kulitaka linyolewe. Hivyo, methali hii ina unafiki na inawapa wanyonge moyo kwa njia ya kufungua njia za wao kunyanyaswa zaidi kwa kuwaambia wasijitete.

*d) Aridhikaye na umaskini wake ni tajiri wa ajabu*

Umaskini ni hali ya kupungukiwa kiuchumi hivi kwamba mhusika hawezi kuyakimu mahitaji yake ya kila siku ipasavyo. Umaskini kwa kawaida si hali ambayo watu wanafaa kuridhika kwayo bali kutafuta mbinu za kujikwamua. Aidha, kudai kuwa maskini aridhikaye na umaskini wake ni tajiri tena wa ajabu ni mbinu tu ya kujipa moyo ila kwa njia hasi. Methali hii haimpi maskini changamoto ya kutaka kujipatia raslimali na mwishowe kujikomboa kutokana na umaskini. Inawahimiza wanajamii kuishi katika hali ya kujikana badala ya kukubali hali zao duni na kutia bidii kuzirekebisha. Isitoshe, methali hii inamwonyesha maskini kuwa anayeridhika na kichache alichojaaliwa na Mungu huishi vyema hata zaidi ya tajiri mwenye mali nyingi kwa kuwa utajiri si kitu ambacho hufanya mtu kuwa na wasaa maishani.

Hii ni methali iliyojengeka katika imani za kidini ambazo humsawiri maskini kama kiumbe aliye karibu sana na Mungu. Nabii Muhammad (SAW) aliomba na kusema “Mungu, nipe maisha marefu kama ya maskini; nifanye nife kama maskini na nikifufuka nijipate katika hadhara ya maskini.” Mke wake alipomuuliza kwa nini aliomba ombi hilo alisema “Kwa sababu maskini wataingia peponi kabla ya matajiri” (Al-Tirmidhi, Hadith 1376). Maskini wanaoamini methali na maandiko haya wameishi katika maliwazo kuwa

hawafai kutamani makubwa yanayowafanya watu kukosa ufalme wa Mungu au pepo hivyo wanaselelea katika umaskini zaidi. Methali sawa na hii ni *Ukikinai kichache Mungu atakupa kingi.*

e) *Kufa kikondoo ndiko kufa kiungwana*

Kufa ni kupoteza uhai. Kufa kikondoo katika maana ya juu hapa kunaashiria kufa bila kujitetea au kulalamika huku maana ya ndani ikimaanisha kupata shida au matatizo bila kulalamika. Aghalabu kondoo hafi tu bali huuawa na mwanadamu au mnyama mwingine kwa lengo la kula nyama yake. Tukielekeza falsafa hii katika maisha ya wanadamu, aghalabu mara nyingi mwanadamu hapati shida tu bali shida zake hutokana na mwanadamu mwenzake kwa lengo la kujitimizia hitaji fulani. Anayeteswa hivyo anapaswa kulalamika asikike na wanajamii wenzake ili waweze kumsaidia kukabiliana na shida zake au na mwenye nguvu anayemkandamiza. Kila mwanajamii akiyanyamazia matatizo yake kwa kutaka kufa kikondoo kwa kuwa ndiko kufa kiungwana dhana ya *Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu* itakufa kwa kuwa huwa inajitokeza sana mwanajamii mmoja anapopatwa na shida na wenzake wakamsaidia kuitatua. Isitoshe, kuna msemu wa Kiingereza unaosema kuwa *kusema shida ni nusu ya kuitatua.* Wanadamu hawafai kuzinyamazia shida zao kwa kuwa huko ni kujiumiza kisaikolojia bali wanafaa kuzisema wapate kujiondolea mizigo nyoyoni na kusema si kulalamika.

f) *Mkono usioweza kuukata ubusu.*

Methali hii inatokana na mfumo wa kitabaka uliokuwa katika jamii za Pwani hasa Waswahili ambapo jamii imegawika katika tabaka la wenye mali na waso mali. Mkono katika muktadha huu umetumiwa kurejelea watu wenye nguvu za kiuchumi, kielimu au

hata kimwili kuwashinda wenzao. Methali hii inatunasihi kuwa tusipigane nao bali tukubaliane nao. Ni vyema kufahamu kuwa, ikiwa mhusika alitaka kuukata mkono husika, ulikuwa kero kwake na ulikuwa unamfanyia yasiyofaa. Vivyo hivyo, ikifikia hali ambapo tunataka kupigana na wenye nguvu lazima wanatumiza kwa njia fulani. Kubusu nako hapa kuna maana ya kukubali. Methali hii inasema kuwa tukubali maonevu na dhuluma za wenye nguvu tukiona hatuwezi kupigana nao. Kitendo kama hiki ni cha kioga na hakifai kuambiwa wanajamii kwa kuwa hakileti suluhisho lolote kwa wenye shida bali kinawatia matatizoni zaidi kwa kurahisisha kazi ya unyanyasaji kwa mwenye nguvu. Mnyonge akiubusu mkono huu anatia sahihi kuwa yuko tayari kudhulumiwa bila kujitetea wala kulalamika hivyo mwenye nguvu anapata upenyu wa kumnyanyasa zaidi na zaidi.

### **3.3.9 Methali zenye ubaguzi wa kinasaba**

Nasaba ni uhusiano wa kizazi baina ya watu. Watu wa nasaba moja ni watu wanaohusiana kwa karibu sana kidamu kutokana na wao kutoka familia, mlango, au ukoo mmoja. Aghalabu watu wa nasaba moja husaidiana na kufaana kwa mengi na huwa watu wa kwanza kukimbilia mtu anapopatwa na janga. Hivyo, watu hawa hawawezi kuthubutu kukaribisha kutoelewana kati yao. Hata hivyo, methali zilizo katika kundi hili huwahimiza wanajamii wa nasaba moja kutoshirikiana wala kusaidiana na licha ya hilo kubaguana. Methali hizi ni kama;

a) *Baba wa kambo si baba.*

Ni kweli kuwa wazazi wengi wa kambo huwatesa wana wao wa kambo kwa njia tofauti tofauti. Hata hivyo, wapo baba wa kambo wazuri ambao huwalea wana wao wa kambo kama watoto wao wenyewe. Kwa watoto waliobahatika kuwa na baba wa kambo wa aina hii, methali hii ni chochezi kwa kuwa japo baba mzazi ndiye baba hawafai kwa lolote ila usaidizi wao unatoka kwa baba wa kambo. Pia, methali hii inapunguza upendo wa baba wa kambo kwa wanawe wa kambo kwa kujua kuwa hakuna analoweza kufanya akubalike kama baba bali watoto watamchukua kama adui yao daima. Kwa hivyo, methali hii inajenga kizuizi cha kiuhusiano kati ya mume mwoa mama na watoto wa mama husika ilhali methali nyingine husema *Mume wa mama ni baba au Aliyemwoa mama ndiye baba.* Methali sawa na *Baba wa kambo si baba ni Mama wa kambo si mama.*

b) *Kaburi la mke mwenza li kombo.*

Inasemekana kuwa methali hii ilitokana na hadith inayotaja kisa cha kweli kumhusu Aisha, mke wa pili wa Mtume Muhammad (SAW). Khadija ambaye alikuwa mke wa kwanza wa Muhammad (SAW) alipendwa sana na Mtume (SAW) mapenzi yaliyoendelea hata baada ya Khadija kufariki. Aisha alipoona hivyo alikasirika sana na kumwonea wivu Khadija japo hakuwahi kumwona kwa kuwa aliolewa baada ya kifo chake. Wivu huu uliendelea hadi siku moja Aisha alimuuliza Muhammad (SAW) kwa nini alimpenda sana mwanamke mkongwe aliyekufa zamani kana kwamba Allah hakumpa mwanamke mwingine mrembo na mzuri hata zaidi. Visa vingi ambavyo vimesimuliwa na Aisha mwenyewe vilitendeka na kudhihirisha wivu mkubwa wa Aisha kwa Khadija. Siku moja Aisha alipita na mwanamke shoga yake karibu na kaburi lililotengenezwa vizuri sana na

akalisifu sana kwa uzuri wake wa ajabu. Baada ya kulisifu mwanamke aliyeandamana naye alimfahamisha kuwa kaburi hilo lilikuwa la Khadija. Hapo ndipo Aisha alipodai kuwa kaburi hilo halikuwa nzuri kama alivyodhania awali bali lilikuwa kombo pembeni.

Aidha, kijumla methali hii imetokana na utesi na ugomvi ambao huwa kati ya wake wenza. Kila wake wenza wanapozozana ugomvi wao hutokana na mume wanayeshiriki kwa mmoja kumwona mwingine kama anayependwa au kupendelewa zaidi. Ikiwa mmoja wao ataaga dunia mwenzake anabaki na mume na hafai kuwa na kinyongo naye tena kwa kuwa hawezi kumnyanganya mume akiwa kaburini. Kuendeleza chuki hadi kufikia kukosoa hata kaburi kwa kusema li kombo ni hulka mbaya kupita kiasi. Inaonyesha kuwa kifo cha mke mwenzake hakimpigi mshipa wa moyo anayehusika na hana majonzi yoyote. Ni vyema kukumbuka kanuni kuu ya Grice kuwa tufanye mchango wetu katika uzungumzaji uwe kama unavyohitajika kuwa katika muktadha husika. Muktadha wa majonzi hivyo, unahitaji maneno ya kupoza wala si ya kuponda na kudharau. Methali hii hukaribiana kimaana na methali isemayo *Uke wenza una karaha*.

c) *Mjukuu si mwana akilia mpeleke kwao.*

Mjukuu ni mwana wa mwana wa mtu. Methali hii inatushauri kuwa tusijishughulishe na matatizo ya wajukuu ila wakipatwa na shida tuwapelekee wazazi wao. Ni vyema kufahamu kuwa mjukuu ni jamaa wa karibu sana ambaye tunafaa tuwajibike katika kumshughulikia na kutatua matatizo yake. Fauka ya hayo, wazee wana wajibu wa kuelekeza wajukuu na kuwafundisha maadili na utamaduni wa jamii kwa kuwa uhusiano wao huwa wa karibu na usiowekewa mipaka ya kuogopana kama ilivyo kati ya wazazi na wana. Kwa misingi hii, methali hii kuwashauri wazee kuwarejesha wajukuu nyumbani

pindi waliapo ni kuwashauri visivyo kwa kuwa mchango wao katika malezi ya wajukuu ni muhimu sana. Zaidi ya hilo, methali hii inajenga chuki kati ya wazee, wana wao na wajukuu.

*d) Mwana kidonda mjukuu kovu / Mwana na ndugu kirugu, mjukuu ni mtu mbali/mwanangwa*

Kama ambavyo mwana huzaa mjukuu, kidonda huibua kovu. Kidonda huuma na hushughulikiwa sana lakini kovu haliumi kwa hivyo halishughulikiwi. Kirugu (uvimbe kama upele mwilini) pia hushulikiwa kama kidonda kwa kuwa huwasha sana. Mwanangwa naye ni mwana wa watu; yaani mwana wa kwingine. Mwana na mjukuu wametokana na mtu mmoja ambaye ni baba na babu mtawalia. Isitoshe, babu hawezi kuonyesha mapenzi au kumshughulikia mwanawe na kumwacha mjukuu akiteseka kisha mwana akubali tu. Naye, atataka kumshughulikia mjukuu kwa kuwa ndiye mwana kwake na kwake yeye ni kidonda si kovu kama ilivyo kwa babu (baba yake). Kando na kuwa methali hii inahimiza ubaguzi wa kinasaba, inaruhusu kutowajibika na kujenga chuki kati ya babu/ nyanya na wajukuu wao.

*e) Mtaka nyingi nasaba hupata mwingi msiba.*

Lengo la jamii kudumisha mahusiano ya kinasaba ni kuweza kufaana na kusaidiana katika kutatua matatizo na kusherehekea ufanisi. Hili ndilo chimbuko la methali inayosema *Mkataa wengi ni mchawi*; yaani anayekataa ushirikiano huenda si mwema. Jinsi jamii ilivyo na watu wengi walio na ushirikiano wa karibu ndivyo inavyoweza kujiendeleza kwa kutatua matatizo yake kwa urahisi. Ni kuipotisha jamii, kuishauri kuwa

anayeleta watu wa nasaba yake pamoja atapatwa na majanga mengi. Methali hii ina lengo la kuivuruga na kuitenganisha jamii kando na kuuua uhusiano wa kinasaba na wa kijamii.

### 3.3.10 Methali zenye ubaguzi wa kiumri

Tangu kale vijana wamekuwa wakionekana kama watu ambao hawana mwelekeo na wasio na hekima ya kutosha kutokana na kukosa tajriba ya maisha. Kukosa tajriba huku hakutokani na lingine ila umri wao na dhana kuwa wazee wameishi kwa muda mrefu na wameona mengi. Tofauti hii ya kiumri mara nyingi imeishia kuwa chanzo cha vijana kubaguliwa kwa njia mbalimbali na methali zinazopatikana katika kundi hili ni mojawapo ya methali zinazowabagua wanajamii kutokana na umri wao. Methali hizo ni kama;

#### a) *Ngoma ya vijana/wana haikeshi.*

Katika miaka ya hivi karibuni jamii nyingi kote ulimwenguni zimekuwa na mwamko mpya kuwahusu vijana kwa kuwapa nafasi za kujiendeleza na kuwahimiza kuwa mstari wa mbele katika nyanja zote maishani zikiwemo siasa na uongozi. Kutokana na jambo hili, baadhi ya vijana wameweza kuibukia kuwa maarufu sana katika sekta tofauti za jamii na kufaulu kuziimarisha sana. Ngoma katika muktadha wa methali hii inamaanisha jambo au shughuli. Kutokana na yaliyoelezwa kuhusu vijana, kwa sasa methali hii haina mashiko kama ilivyokuwa miaka ya awali. Hata hivyo, ikiwa ina mashiko au la methali hii imebeba ujumbe wa ubaguzi kwa vijana na haiwafai kwa lolote ila kuwavunja moyo.

*b) Akosapo mkubwa mdogo huadhibiwa*

Japo methali hii inataja jambo ambalo ni la kweli katika jamii tunapozingatia ukubwa wa umri na pia mamlaka, dhima yake ni hasi. Uhasi wake unatokana na hali kuwa uonevu huu unaofanyiwa wanyonge au wadogo na wakubwa wao unatajwa kama jambo la kawaida tu ambalo labda jamii haina shida nalo ilhali si ukweli. Ni kawaida ya wenye nguvu ama kutokana na umri au mamlaka kuonekana kama viumbe wasiokosea hivyo lawama zote pamoja na adhabu zinazotokana na makosa yao kuwaendea wadogo wao. Ikiwa huu ndio ukweli wa hali, kuutaja bila kuushutumu kwa vyovyote kunawapa nguvu wadhaliilishaji dhidi ya wanyonge na kuwafanya kuwadhaliilisha na kuwakandamiza hata zaidi.

### **3.3.11 Methali zenye ubaguzi wa kiuana**

Baadhi ya methali katika kategoria hii huzua ulinganisho usiohalalika kati ya jinsia ya kike na kiume hasa kwa kutumia mizani ambayo inahakikisha kuwa jinsia ya kike imeshindwa. Zingine humsawiri mwanamume kama kiumbe huru anayeweza kufanya lolote alitakalo huku mwanamke akionyeshwa kuwa kiumbe duni aliye chini ya utawala wa mwanamume. Methali hizo ni kama;

*a) Kuku jike hawiki penye jogoo*

Kulinganisha kuku jike na dume kwa kutumia mizani ya 'kuwika' si haki kimaumbile kwa kuwa kwa vyovyote vile kuku jike hakupewa uwezo wa kuwika. Hii ni sawa na kumlinganisha kuku dume na jike kwa kutumia mizani ya 'kutaga' ambapo kuku dume hawezi kuwa mshindi. Kuku jike hapa anawakilisha jinsia ya kike huku kuku dume

akiwakilisha jinsia ya kiume. Methali hii ina maana potofu kuwa wanawake hawana usemi katika kundi la waume. Huu ni ubaguzi na uonevu na la kuudhi ni kuwa hautokei kwa sababu ya udhaifu wowote kwa wahusika bali tu kuwa ni wa jinsia ya kike. Katika karne ya ishirini na moja ambapo kila mwanajamii anapigania haki za kijinsia na nyanja zote za jamii zinajaribu kuondoa ishara zozote za ubaguzi wa kijinsia katika lugha, methali hii haiwezi kuwa na dhima chanya kwa jamii ila tu dhima hasi.

Swala la kimsingi lililoibuka katika maana ya methali hii ni kuwa, mwanamke ni mtu dhaifu akilinganishwa na mwanamume na hawezi kamwe kuwa juu ya mwanamume. Hata hivyo inapata mtetezi katika dini ya Kiislamu kwa kunukuu nasaha ya Mtume Muhammad (SAW) kwa wanawake kwamba *“lau ingeruhusiwa binadamu kumsujudu binadamu mwenzake, ningewaambia wanawake wawasujudie wanaume.”* Methali hii inashirikiana na dini kumkweza mwanamume na kumtweza mwanamke kwa upande mwingine hivi kwamba mmoja anaelekea kuwa Mungu wa mwenzake (Quran 4:34) kando na kujenga kasumba kwa wanawake kuwa majaaliwa yao ni kuwa chini ya wanaume daima. Kasumba hii kwa wanajamii inadhihirika vizuri zaidi katika utenzi wa ‘Mwanakupona’ (Ndungo, 1985). Katika utenzi huu inadhihirika kuwa mwanamume ndiye hata anayeamua ikiwa mwanamke ataenda peponi au jahanamu. Ushauri ufuatao unapatikana katika ubeti 24 hadi 26:

*Na ufapo wewe mbee  
Radhi yake izengee  
Wende uitukuzie  
Ndipo upatapo ndia*

*Siku ufufuliwao  
Nadhari ni ya mumeo  
Taulizwa atakao  
Ndilo takalotendewa*

*Kipenda wende peponi  
Utakwenda dalhani  
Kinena wende motoni  
Huna budi utatiwa*

Ujumbe huu kama ule upatikanao katika methali inayojadiliwa ni hasi na wenye dhalala kwa wanawake.

*b) Mume ni kazi mke ni tabia / Uzuri wa mke ni nguo, wa ng'ombe ni kulimiwa /  
kupamba mke ndiyo sifa ya mume*

Labda katika kipindi cha kuibuka kwake methali hii ilikuwa na uchanya wake kwa kuwa wakati huo hasa katika jamii ya Waswahili iliyotawaliwa zaidi na imani ya dini ya Kiislamu mwanamke alitarajiwa kukaa nyumbani (Quran 33:33) akijirembesha kwa ajili ya mumewe na kumtunzia mume nyumba, mali na watoto huku mume akitarazaki kutafuta chakula na mahitaji mengine ya kuikimu familia yake. Hata hivyo, mpito wa wakati, kubadilika kwa mifumo ya kiuchumi, elimu na matangamano ya Waswahili na watu wa janibu zingine yamewafanya wanawake pia kushiriki kikamilifu katika kazi takriban zote zifanywazo duniani. Kwa hivyo, maana ya methali hii kuwa mume ndiye mmiliki wa nyumba na mwenye kukidhi mahitaji ya nyumbani huku mke akiwa wa kujirembesha tu pamoja na dhima ya kuwahimiza waume wawe wakakamavu maishani ili wakidhi mahitaji ya mke na watoto zimepitwa na wakati.

Methali hii ikiangaliwa kijuujuu inaweza ikapata maelezo ya kuvutia sana kama yanayotolewa na King'ei na Ndalū (keshatajwa) wanaotoa maana yake kuwa '*Mume sio jina bali ni kujitolea kufanya kazi. Mke naye hupendeza akijipamba kwa nguo za kuvutia (Uk. 228)*. Hii ni dhana ambayo imepitwa na wakati katika ulimwengu wa sasa ambapo

wanawake kwa wanaume wamesoma sawa na kujihusisha sawa katika ujenzi wa mataifa yao. Wanawake katika karne hii wanapatikana katika kila taaluma hata zile zilizoachiwa wanaume kitambo kama urubani, uhandisi na ujenzi. Isitoshe, si haki kumshauri mwanamke ajipambe tu na kungojea mumewe kumfanyia kazi kwa kuwa jambo hili limebainika kama chanzo cha ukandamizaji na udhalilishaji kwao. Japo mume anafaa afanye kazi na mwanawake anafaa ajipambe, methali hii haina mchango wa kuifaa jamii ya sasa kutokana na ubaguzi wa kijinsia unaotokana nayo. Inamchora mwanamke kama kiumbe anayefaa kujishughulisha tu katika kujikwatua ili apendeze zaidi kwa mumewe au kwa wanaume bila kuchangia katika ujenzi wa uchumi wa nchi.

*c) Mume ni moto wa koko usipowaka utafuka.*

Mkoko ni mti unaomea baharini ambao kuni zake huwaka na kufuka moshi hata kuonekana na walio mbali. Methali hii imejaa taasubi za kiume na majigambo ya mwanamume na jinsia yake katika jamii. Ikiwa mwanamume anadai kuwa yeye ni moto wa koko basi asingefikia uamuzi huo bila kujilinganisha na mtu wa jinsia tofauti. Kutokana na jambo hili inalomaanisha methali hii moja kwa moja ni kuwa mwanamke ni mtu dhaifu akiwekwa katika mizani na mwanamume kwa kuwa mwanamume hangejilinganisha na kiumbe mwingine yeyote yule. Kando na kumkweza mwanamume kibaguzi, methali hii inamwonea, kumtweza na kumdhalilisha mwanamke na kwa sababu hiyo dhima yake ni hasi.

*d) Mwanamme ni mbono hualika kule.*

Mbono ni mti huzaao mbegu ambazo zikikauka hupasuka kwa nguvu na kutawanyika mbali sana; kualika mbali. Hii ni methali inayotishia asasi muhimu zaidi katika jamii

ambayo ni asasi ya familia. Inafanya hivyo kwa kuwaonyesha wanaume kuwa hulka yao ni kuwa na mahusiano kadha na kusambaza mbegu zao kote. Nasaha ya methali hii ikizingatiwa na wanaume asasi ya ndoa na familia ambazo ndizo msingi wa jamii pana zitaporomoka na kupelekea kuporomoka kwa jamii nzima. Isitoshe, ujumbe ulio katika methali hii ni tishio kubwa kwa afya ya jamii hasa inapokumbukwa kuwa kuna magonjwa mengi yanayosambazwa kupitia mahusiano ya kimapenzi UKIMWI ukiwemo. Isisahaulike pia kuwa swala hili la ugonjwa wa UKIMWI limekuwa donda sugu kwa jamii kwa kuleta matatizo ya kupoteza wataalamu wake, kuachwa kwa watoto mayatima baada ya wazazi kufa na gharama kubwa iliyoелеmezwa serikali ya kugharamia matibabu ya wanaougua. Kufuatia yote haya, methali hii inaielekeza jamii katika maangamizi. Methali sawa na hii na inayotumiwa sana na hasa wanawake wa Kiswahili kuhalalisha hali ya waume kuwa na mapenzi nje ya ndoa husema *Mtu halindi bahari, ipitayo kila chombo*.

Hata hivyo, japo hasi kwa kuonekana kuhalalisha wanaume kuwa na jicho la nje, methali hii hupata kutetewa na dini. La kushangaza ni kuwa wanawake wanaotarajiwa kupinga swala hili huiunga mkono pia katika misingi kuwa inasawiri ukweli wa maisha. Hii ni methali inayoendeleza taasubi za kiume kwa kuonyesha kuwa mwanamume ana uhuru wa kufanya lolote alitakalo katika mahusiano ya kimapenzi. Aidha, misemo kama vile *Mume ni mume japo gumegume ana sifa za Mtume* na *Hakuna mtume mwanamke* huitetea. Isitoshe, hali ya dini ya Kiislamu kukubali wanaume kuoja jumla ya wake wanne kwa pamoja (Qur'an 4: 3) na dini ya Kikristo katika agano la kale kukubali wanaume kuoja zaidi ya mke mmoja (Kutoka 21: 10) inaitia nguvu zaidi. Hoja hiyo ni kando na

manabii watajika kama Musa, Yakobo, Elkana, Daudi na Suleimani kuwa na zaidi ya mke mmoja.

*e) Mke ni nguo, mgomba hupaliliwa*

Mke ni mwanamke ambaye ameolewa na mwanamume fulani nao mgomba ni mmea uzaao ndizi. Uzuri wa mke katika methali hii unafananishwa na hali ya kunawiri kwa mgomba. Kama ambavyo mgomba unahitaji kupaliliwa na kutunzwa kwa mbolea na kadhalika ili utoe ndizi nzuri ndivyo mke anavyofaa kuvishwa mavazi mazuri yakiwemo nguo, vipuli, bangili, mikufu, vikuba na khanga. Kwa upande mwingine, anafaa kuletewa chakula kizuri ili asipoteze urembo aliotoka nao kwao.

Kawaida ya utamaduni wa Waswahili ni kuwa huku mume akitarazaki kupata mali na fedha za kuyakimu mahitaji ya familia mke hubaki ndani ya nyumba kufanya shughuli za ndani tu hasa kujirembesha kwa sababu ya mume na kupika kilicholetwa na mume. Methali hii ni mojawapo ya methali ambazo zikiangaliwa juu juu zinaonekana kuwa na dhima chanya huku dhima hasi ikiwa imefichika. Matteru (1998) anasema;

“Picha ya mgomba na nguo zinatumiwa kusimama sambamba na ile ya mke. Katika methali hii imani ya kuwa mwanamke ni kiumbe mnyonge na anahitaji kutunzwa ili awe na manufaa zaidi inajitokeza”

Japo Matteru anataja kuwa mke kwa muktadha wa methali hii anatunzwa ili awe na manufaa zaidi, ni vyema kutilia mkazo swala kuwa anatunzwa kwa imani kuwa yeye ni ‘dhaifu’. Swali la kujiuliza ni je wake kweli ni dhaifu? Dhana hii potovu imetumiwa na jamii nyingi kumdhaliisha mwanamke na kumtenga na maswala muhimu ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa kuwa anaachwa tu nyumbani na wala hajui linaloendelea nje ya kijiji chake au hata boma lake. Zaidi ya hayo, mke hapa amedunishwa na kutwezwa

chini ya kiwango cha binadamu mwenye akili na uamuzi wa kibinafsi na badala yake kuwa pambo dhaifu la mume lisiloweza kujitegemea pasipo usaidizi wa mume.

*f) Hakuna mkika muungwana*

Muungwana ni mtu mwenye adabu na desturi njema na anayekaa na binadamu wenzake kwa uzuri. Aidha, muungwana pia ni msamiati uliotumika sana Pwani hasa miongoni mwa Waswahili kwa maana ya mtu asiye mtumwa. Biashara ya watumwa ilinoga sana pwani hasa katika karne ya kumi na tisa na ishirini. Kwa mujibu wa Strobel (1979), japo baadhi ya wanawake walimiliki watumwa, kisheria na kwa mujibu wa falsafa ya jamii wao walimiliki nafasi sawa na watumwa. Methali hii inaonyesha kwamba wanawake sawa na watumwa hawangeweza kuwa waungwana. Vivyo hivyo, wanawake wawe wameolewa au la hawatarajiwi wala kuruhusiwa na sheria za kiislamu kukidhi mahitaji ya familia zao kiuchumi. Wao wanakuwa watumwa wa kiuchumi kwa wanaume na wahitaji wanaowategemea wanaume kwa mahitaji yao yote. Hivyo, ujumbe ulio katika methali hii na dhima yake ni hasi.

*g) Ikiwa hana kazi (mume) hajaliwi*

Heshima na wajibu wa mume huonekana zaidi katika uwezo wake wa kifedha kwa mujibu wa methali hii. Mume ambaye hawezi kuikidhia familia yake mahitaji ya kiuchumi huchukuliwa kama aliyefeli kimaisha. Hivyo, wasichana wa Kiswahili walihimizwa kuolewa na wanaume wenye uwezo wa kifedha. Tangu utotoni mtoto msichana hulelewa kwa lengo la kuwa mke na mama mzuri. Msichana hufundishwa jinsi ya kufanya kazi za nyumbani zikiwemo kupika, kufua na kunadhifisha nyumba ya mumewe pindi atakapolewa kando na kujikwatua kwa ajili ya kumfurahisha mumewe.

Wasichana Uswahili pia hawakurusiwa kutoka nje peke yao hasa mchana ila waliruhusiwa kutoka usiku tu kuwatembelea marafiki wakiandamana na mwanamke mwenza tena mtu mzima. Wanaume walipotembea, wasichana walitarajiwa kujificha katika vyumba vya ndani wasionekane na wangekaidi wangepokea adhabu kali. Isitoshe, Waswahili waliwatawisha wasichana punde wanapovunja ungo (miaka sita) ili kuhakikisha kuwa hawatangamani na wavulana na kushiriki nao mapenzi (Kindy, 1972). Kutawisha kulihusisha msichana kufungiwa ndani na kupeanwa kwa kungwi ambaye huwa kama mwalimu wake wa kumfundisha jinsi ya kujitunza, kupika kutengeneza vikapu na bidhaa zingine za nyumbani pamoja na jinsi ya kuishi na mume. Wasichana hawa walitoka tu kwa jambo la dharura huku wakiwa wamevaa buibui kimashrti. Elimu ambayo wasichana hawa walipata kwa kungwi ilijulikana kama unyago na lengo lake kuu hasa ni kumfurahisha mume. Wanawake wanatayarishwa kuingia katika ndoa kwa njia hii kwa kuwa wao wanatarajiwa kuzaa watoto na kuwalea kando na kumtunza mume tu wala hawatarajiwi kujihusisha na shughuli zozote za kiuchumi. Ujumbe unaopatikana katika methali hii basi umeegemezwa katika utamaduni wa jamii ambao ni hasi na wenye dhalala kwa wanawake. Methali zingine sawa na hii husema *Mpuuzi hana kazi na Mume ni kazi*.

*h) Ushaufu si sifa ya mwanamke*

Wanawake wamefundishwa kuridhika kwa kuwajibikia maswala ya kinyumbani ya kuwa mke na mama huku wanaume wakipewa motisha na shauku ya kutoka nje, kutangamana na kubobea katika nyanja zote za maisha. Ugawaji wa majukumu ya kiuana katika jamii humwekea mwanamke mipaka ya kufanyia majaribio talanta zake na uwezo wake wa

kiakili na kimwili hivyo kuuu uwezekano wake kupata ufanisi wa aina yoyote nje ya nyumbani kwake. Mwanamke mwadilifu ni yule mwenye mapenzi kwa bwana (Al-Tirmidhi 3272) na watoto, mwenye bidii na anayebakia nyumbani na kumngoja bwana kumkimia mahitaji yake. Aidha, mwanamke anatarajiwa kutia kila juhudi kumtunza bwana na kuwalea wanawe kwa uadilifu iwezekanavyo. Jamii kupitia methali kama hii inamwonya dhidi ya kukiuka lolote linalompasa mwanamke mzuri kwa kuwa kwa kufanya hivyo atafikwa na mawi yasimkinika. Methali nyingine inayomhimiza mke kujitolea kumtumikia mume hata kwa maswala yanayomuumiza husema *Mume ni jaha si raha*.

i) *Mwanamke hapendezi ila dafuni mwake.*

Methali hii inatokana msisistizo wa jamii hasa ya Waswahili kuwa majukumu yote ya mwanamke yanazungukia nyumbani kwake wala hatarajiwi kutanga na njia. Mwanamke hana jukumu lolote katika uwanja wa kiuchumi kwa kuwa jukumu lake ni la kinyumbani tu. Mahitaji yake yote ya kifedha, kijamii na kidini yanakidhiwa na mumewe. Kwa sababu hii, mwanamke naye anatarajiwa kujitolea kwa mume kwa mahitaji yake yote ya kijamii na kimapenzi. Jambo hili linadhihirika wazi katika utenzi wa Mwana Kupona (1860) ambapo mama anamwasa bintiye kuhusu jinsi ya kuishi na mume kwa kumwambia:

*Keti naye kwa adabu  
Usimtie ghadhabu  
Akinena simjibu  
Itahidi kunyamaa*

*Kilala siikuse  
Mwegeme umpapase*

*Na upepo usikose  
Mtu wa kumpepea*

*Chamka siimuhuli  
Mwandikie maakuli  
Na kumtunda mwili  
Kumsinga na kumwoa*

Majukumu yote anayotajiwa mwanamke katika beti hizi tatu yanaweza kutekelezwa tu nyumbani na hilo ndilo lililotarajiwa kwa mwanamke yeyote yule. Hivyo, methali hii inatumiwa na jamii iliyojaa taasubi za kiume kumwekea mwanamke mipaka ya kiutangamano, kiuchumi na kifikra hivi kwamba hawezi na hatarajiwi kujihusisha na lolote linalopita au za nyumbani kwake.

*j) Jogoo halei mwana*

Methali hii inauweka wazi ugawaji wa majukumu ya kijamii kitamaduni ambapo mke amepewa jukumu la kuwalea wana. Inamkumbusha na kumfanya mwanamke kuamini kuwa jukumu la kuwatunza watoto ni lake kikamilifu wala si la mume asilani. Jukumu kubwa la mume kwa upande mwingine, ni kuikidhia familia yake mahitaji yote ya kiuchumi. Kutokana na jukumu hili la mke lawama nyingi zinazohusiana na tabia za wana huwalenga wanawake hata kama hawana mchango katika kuzikuza tabia hizo. Baadhi ya lawama hizo huwa ndani ya methali kama; *Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu* ambayo huchukulia kuwa mtoto yeyote mwenye tabia zisizofaa katika jamii alikosa kuelekezwa na mamake. Aidha, methali *Mama kwa mwanawe, mtoto kwa mamaye* inayoonyesha uhusiano wa karibu kati ya mama na mwana.

### 3.3.12 Methali zinazohimiza ukabila

Kwa mujibu wa Osaghae (1994) kabila ni kundi la watu wanaojinasibisha na jadi moja kijamii, kiutamaduni na kitajriba hasa tajriba za kitaifa. Mambo mengine yanayotambulisha taifa ni pamoja na itikadi, historia, urithi, lugha, falsafa, dini, maumbile, mavazi, chakula na makazi ya kiasili. Obioha, (1999) anatambua kuwa tatizo la ukabila mara nyingi hutokana kimsingi na hali ya mtu kujitambulisha na kabila fulani kwa kuwa utambuzi huo huambatana na mvuto wa kinafsi na kijamii. Hata hivyo, utambuzi huo huwa vigumu kutambulika kwa kuwa umefichika akilini mwa mhusika hadi unapojitokeza katika hali ya kutoelewana kati ya kabila husika na lingine. Baadhi ya methali zinazoendeleza dhana za kikabila ni;

*a) Mtu hauzi kabila lake.*

Kuuza katika methali hii kuna maana ya kusaliti. Ni dhahiri kuwa nchi nyingi hasa za Kiafrika ziko katika hali mbaya ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kwa sababu ya ukabila; kwa sababu ya watu ambao hawako tayari kuyasaliti makabila yao katika hali yoyote ile. Kila lifanywalo na wanakabila lao ni nzuri si kwa kuwa mwanakabila hakosi bali kwa kuwa hasalitiwi. Kati ya mawi mengi yaliyozuka kutokana na kasumba hii ni vita vya kikabila, mauaji ya jinai, uharibifu wa mali, ubakaji, utekaji nyara, uibukaji wa makundi ya waasi, mapinduzi ya kiserikali na wananchi kuishi uhamishoni miongoni mwa mengine mengi. Katika hali kama hii ambapo ukabila umeyaumiza mataifa mengi na ambapo wanadiplomasia na viongozi wema katika jamii wanajaribu kuwahimiza watu kuweka mataifa yao mbele ya makabila methali hii haitufai kwa lolote kwa kusema kuwa tusiyasaliti makabila yetu bila kufafanua muktadha. Maelezo haya hata hivyo

hayalitupili mbali kabila kama asasi isiyo na umuhimu wowote katika jamii bali yanaonyesha kuwa upendeleo mwingi wa kikabila umesababisha mabaya mengi na haufai kuhimizwa.

*b) Mgala mwwue na haki umpe.*

Waswahili wa kaskazini ya pwani wamepakana na Wagalla na wamekuwa maadui wakipigana mara kwa mara hasa kutokana na asasi zao za kiuchumi zisizolingana. Waswahili ni wakulima huku Wagalla wakiwa wafugaji wa kuhamahama. Methali hii inachochea maonevu kwa kabila la Wagalla kutoka kwa Waswahili japo kuna sehemu inayotaja upewaji wa haki. Haki katika muktadha huu haina umuhimu wowote kwa kuwa inafika baada ya maafa kutokea. Kwa kawaida Mgalla angepewa haki kabla ya kuuawa ili akipata haki ya kuishi aepuke kifo. Kinyume cha jambo hili, methali hii inapendekeza adhabu ya kifo kwa Mgalla kabla ya swala la haki yake kufikiriwa. Hivyo, ni unafiki uliokithiri kudai uungwana wa kumpa mtu haki ilhali adhabu yake imepitishwa bila nafasi ya kujitetea. Ikiwa Mgalla atauawa haki yake ataipataje? Au ikiwa atatendewa ubaya kabla ya kutendewa wema atauhisi wema huo?

### **3.3.13 Methali zenye ubaguzi wa kidini**

Kubagua kidini ni hali ya kutoa vitu, huduma au kuhusiana na wanajamii wengine kwa upendeleo wenye misingi ya dini. Methali zenye upendeleo wa kidini hueneza dhana kuwa watu wa dini moja wanafaa kuwa ndugu na kufaana wao kwa wao na uhusiano wao na watu wa dini nyingine haufai ila tu inapobidi. Aidha, baadhi ya methali hizi pia

hutumia dini kuleta ubaguzi wa kitabaka kwa kuhusisha imani ya dini na hali za watu za kiuchumi. Mifano ya methali hizi ni kama;

a) *Kafiri akufaaye si Islamu asiyekufaa*

Methali hii ikiangaliwa kijuujuu inaweza kuonekana kama yenye dhima chanya na inayoonyesha uhusiano mwema kati ya kafiri na Islamu. Kafiri hutumiwa kwa kawaida kwa maana ya mtu asiyeamini dini ya Uislamu na hutumiwa na Waislamu kuonyesha dharau. Kijelezi hiki kina maana kuwa watu wote ambao si Waislamu ni kafiri hata kama ni waumini wa dini zao hivyo dharau la neno 'kafiri' linawaangukia wote. Isitoshe, methali hii inaonyesha kuwa ukawaida au utaratibu mwafaka wa mambo ni Mwislamu kumfaa Mwislamu mwenzake na ni jambo lisilo la kawaida kwa kafiri kumfaa Islamu lakini haidhuru tu ikiwa atamfaa. Kando na hilo methali hii inawataja wasio waislamu kwa neno la dharau "kafiri" kama njia ya kuonyesha chuki na kutojali hisia zao kwa kuwa ni watu wa kundi hasimu. Huu ni ubaguzi wa kidini na unaleta chuki na utengano unaoegemea dini.

b) *Maskini hana imani*

Methali hii hurejelea uwiano uliopo kati ya dini na utabaka katika jamii. Inasawiri kuwa dini pia ilitumiwa na bado hutumiwa hadi leo kuendeleza dhuluma katika jamii na kuwagawa watu kutegemea hali zao za kiuchumi. Dini inatumiwa na tajiri kumtenga maskini na hata kumdhaliisha kwa singizio kuwa hana imani kutokana na umaskini wake. Ni vyema kutaja hapa kuwa, dini si swala la kiuchumi kwa vyovyote vile bali swala la kiroho na kiimani. Hali ya mtu ya kiuchumi haichangii kwa vyovyote vile imani

yake kwa Mungu au kwa dini yake. Methali hii ni kinyume cha methali *Kukosa (mali), si ila na Kumcha Mungu, si kilemba cheupe*.

### 3.4 KIISHILIO

Sura hii imeeleza aina za uhasi katika methali za Kiswahili pamoja na maelezo ya kina ya jinsi uhasi huo unavyojitokeza pamoja na unavyohusiana na utamaduni wa jamii. Aina za uhasi zilizozingatiwa ni kuchochea vita, kudharau wanyonge, kuvunja moyo, kudhihaki ulemavu, kutabiri maangamizi pamoja na kuendeleza ubaguzi wa kikabila, kijinsia, kidini na kiumri. Aidha, imebainika kuwa uhasi huu unaambatana na maovu mengine kama vile kutozingatia uhalisia, kukwepa majukumu na matumizi mabaya ya utamaduni. Zaidi ya methali zilizochanganuliwa hata hivyo, lugha ya Kiswahili ina methali nyingi sana ambazo zimekusanywa na kuandikwa vitabuni na baadhi ambazo hazijaandikwa. Utafiti huu umechunguza asilimia ndogo sana ya methali zote za Kiswahili. Hivyo, Kiswahili kina methali nyingi zenye dhima chanya wala haifai kuchukuliwa kuwa methali zote za Kiswahili zina dhima hasi. Kando na hilo, methali zizi hizi zilizopewa dhima hasi katika sura hii zinaweza kuwa na dhima chanya zinapohusishwa na miktadha tofauti kama ilivyofanyika katika sura ifuatayo (sura ya nne).

## SURA YA NNE

### MANUFAA YA METHALI ZA KISWAHILI ZENYE DHIMA HASI KWA JAMII

#### 4.0 UTANGULIZI

Sura ya tatu imeziainisha na kuzichanganua methali za Kiswahili zenye dhima hasi kwa kuonyesha uhasi wake na jinsi zisivyoifaa ama jamii nzima au kundi lengwa katika jamii. Uchanganuzi huo umefanyika kwa kusisitiza kuwa uhasi husika unategemea muktadha na katika muktadha tofauti methali zinaweza kuzua dhima chanya au kuwa na manufaa kwa jamii. Sura hii itashughulikia dhima chanya ya methali za Kiswahili zilizochanganuliwa katika sura ya tatu kwa mtazamo hasi. Ni vyema kufahamu kuwa, kwa mujibu wa nadharia ya Udenguzi ambayo ndiyo imeongoza utafiti huu hakuna maana itokanayo na lugha ambayo inadumu na hakuna kauli ya lugha inayoweza kutajwa kama yenye maana moja mahsusi kwa kuwa lugha yenyewe haina kitovu kimoja cha maana bali maana huhamahama. Mara nyingi, lugha haiwezi kubainisha wazi inachomaanisha kwa kuwa maana yake inaweza kufasiriwa kwa njia tofauti kutegemea kigezo cha hasa muktadha, mfasiri na tajriba yake, nia ya mfasiri, utamaduni wa jamii, mpito wa wakati n.k.

Uhasi na uchanya wa methali za Kiswahili kwa mujibu wa nadharia ya Udenguzi hivyo, ni kama pande mbili za shilingi ambapo zote zinamilikiwa na shilingi moja. Hata hivyo, haiwezekani kwa pande hizo kuangaliwa kwa wakati mmoja bali mtu anaweza tu kuuangalia upande mmoja kwanza ndipo aungeukie upande wa pili. Vivyo hivyo, methali za Kiswahili zinaweza kuwa na dhima mbili: moja hasi na nyingine chanya ila dhima

hizo mbili haziwezi kujitokeza katika muktadha mmoja bali kila moja hujitokeza katika muktadha wake.

#### **4.1 UCHANYA WA METHALI HASI**

Ni sharti umuhimu wa methali katika lugha utangulizwe kwa kufahamu kuwa methali huathiriwa na utamaduni wa jamii husika. Muriel (1982) akiendeleza mawazo ya watangulizi wake kama Parker (1970) na Msuya (1977) anasema kuwa lugha na utamaduni ni kama ndugu. Methali hutokana na utamaduni wa jamii. Aidha, methali za Kiswahili hazitokani na ombwe tupu bali hutokana na utamaduni wa jamii ya Waswahili. Kwa mujibu wa Kinge'i (1982) methali zote hujihusisha na mambo ya maisha ya kila siku ambayo ni pamoja na vitendo, maneno na fikra za watu katika maingiliano yao ya kawaida, matumaini yao, imani zao, kazi zao, dini yao, sherehe, ada na kadhalika. Hivyo, methali hutumiwa kama kifaa cha jamii cha kutatulia shida zao zinazowakumba kila siku na kumaliza migogoro ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ama kati ya wanajamii wa jamii husika au kati ya jamii hiyo na nyingine. Kupitia kwa methali, watumiaji huweza kupata mwelekeo wa kutathmini na kuepukana na misukosuko mbalimbali ya kimaisha kwa kuwa methali zina nguvu ya kuibua usemezano wa nafsi, mtu na mtu, mtu na watu au watu na watu (Maitaria, 2012). Akichangia swala kuwa umaarufu wa methali za Kiswahili umetokana na matumizi mapana ya lugha ya Kiswahili Afrika Mashariki na Kati, Maitaria (2013) anaongeza ufafanuzi kuwa, methali huwasilisha maarifa lukuki katika kukabiliana na matatizo yaliyopo kwa manufaa ya jamii za Afrika Mashariki na kwengineko ambapo lugha hii hutumiwa kama chombo cha mawasiliano.

Methali vile vile, hutumika kama akiba ya tajriba ya jamii katika mazingira maalumu. Sababu mojawapo ya kufanya hivyo inatokana na ukweli kwamba methali hutoa ufafanuzi wa falsafa katika jamii fulani kuhusu maisha yao ya zamani na tajriba zao za miaka na mikaka. Aidha, methali na falsafa havitengani kwa kuwa vyote hugusia kanuni za maadili ya ustaarabu maishani (Nsookwa, 2011). Methali imeundwa na kutolewa kulingana na mawazo kadhaa na nia maalumu kwa faida ya jamii. Mawazo yaliyomo ndani ya methali yanashikamana na tamaduni, desturi na hadhi ya jamii hiyo husika. Kwa mfano, baadhi ya methali zilizochanganuliwa katika sura ya tatu zinadhihirisha dhima chanya kama ifuatavyo:

#### **4.1.1 Kusawiri ukweli wa maisha ya mwanadamu**

Methali zilizo katika kundi hili husawiri uhalisia wa matukio ambayo humkumba mwanadamu katika maisha yake moja kwa moja. Zinataja matukio mbalimbali yanayomkabili mwanadamu yawe ya kupendeza ua la kwa lengo la kumwonyesha ukawaida wa hali anayopitia (hususan inayoumiza) hivyo kumpa moyo. Methali hizi ni kama;

##### *a) Bahati humwacha wa mbele na kumfuata wa nyuma*

Japo methali hii inaweza kutumiwa kwa njia hasi katika muktadha uliotajwa katika sura iliyopita, muktadha tofauti unaisawiri kama methali chanya na yenye mafao makubwa kwa jamii. Methali hii inatanabaisha kuwa japo bidii ni muhimu mja pia huweza kufanikiwa kupitia bahati na bahati ya mja haiwezi kumwepuka. Ingawa hatuwezi kuitegemea bahati katika kutafuta riziki, ukweli ni kuwa baadhi ya watu katika jamii hufanikiwa kwa kuangukiwa tu na nyota ya jaha. Methali hii inaweza kutumika kuwatia

moyo watu ambao wamekosa kitu baada ya kutia bidii huku wenzao wakifanikiwa katika jambo lilo hilo. Inawausia kuwa wasife moyo kwa kuwa siku yao ya kufanikiwa itafika. Methali hii ina maana sawa na “*Bahati ya mwenzio usiilalie mlango wazi.*”

*b) Mahaba ya wanadamu si mambo ya dawamu / Mahaba hayana dawamu*

Methali hii kwa upande mmoja ambao ndio wazi zaidi ina uhasi. Hata hivyo, inaweza kutumiwa kwa upande mwingine kupeana nasaha kuhusu mapenzi hasa kwa vijana ambao wanaweza kuwa wamejaa mshawasha wa mapenzi bila kujali hatima yake. Inawausia kuwa binadamu ni kiumbe dhaifu na udhaifu wake hauwezi kumruhusu kupenda dawamu bila pingamizi zozote au masharti yoyote kwa kuwa hayo ndiyo maumbile yake. Kutokana na udhaifu wake kwa mfano akikosewa mapenzi yake yanaweza kupungua au kuisha. Isitoshe, inawatia moyo watu walioachwa na wapenzi wao kwa kuwafahamisha kuwa jambo lililowapata ni la kawaida kabisa na wanafaa kulikubali na kuendelea na maisha.

*c) Kiingiacho mdomoni si haramu / kiingiacho mjini si haramu*

Japo methali hii inatoa dhima hasi moja kwa moja kwa kuhalalisha kila kinachoringia mdomoni na mjini kiwe kizuri au kibaya inaweza kutumika kwa njia chanya pia. Hali ya kuingia mdomoni/ mjini inaweza kuwa na maana ya kitu kinachoweza kumsaidia mtu anapokuwa katika hali mbaya sana. Japo kitu hicho kwa kawaida kinaweza kuonekana kibaya, katika muktadha huo si haramu kwa kuwa aghalabu kina uwezo wa kumsaidia. Kwa mfano waumini wa dini ya Kiislamu hawaruhusiwi kula nyama ya nguruwe katika muktadha wa kawaida lakini wanaruhusiwa tu katika muktadha ambapo nyama hiyo tu ndiyo inayoweza kuyaokoa maisha ya mtu (Quran, Al-Baqara 2: 173).

d) *Mgala muue na haki yake umpe*

Kwa kutaja kifo kabla ya haki, uhasi wa methali hii uko wazi. Hata hivyo, kwa upande mwingine methali hii ina uchanya wake kwa kufundisha kuwa hakuna mbaya anayekosa hata chembe ya uzuri. Katika mtazamo huu, methali hii inatetea haki kuwa mtu mwovu japo ametenda maovu akitenda wema anahitaji sifa kwa wema huo bali haufai kumezwa na maovu yake. Katika mtazamo huu methali hii ina maana sawa na '*Baniani mbaya kiatu chake dawa*' na '*Shomvi mbaya kiatu chake dawa.*'

e) *Mtu hauzi kabila lake*

Japo ukabila unaweza kukuzwa kwa methali hii, inaweza pia kutumika kwa uchanya. Kwa kusema kuwa mtu hauzi kabila lake, methali hii inaweza kumaanisha kuwa mtu hafai kuisaliti jamii yake bali anafaa kuwa mzalendo na kuisaidia. Ukweli ni kwamba mtu hutokana na jamii fulani ya watu inayoweza kuwa kabila, kijiji, mji au nchi. Methali hii inamkumbusha kila mwanajamii kuwa ameibukia katika jamii fulani ya watu ambayo ndiyo imemlea na hafai kuidharau jamii hiyo aushini mwake.

#### 4.1.2 Kutahadhari

Japo kwa mtazamo wa juu methali za kategoria hii zinaweza kuchukiwa kwa kutoa vitisho na kutumia lugha ya ukali kupita kiasi au hata kutoa utabiri wa maangamizi kwa mlengwa, lengo lake haswa ni kutoa tahadhari kwa wanajamii katika hali zinazoonekana kuwa hatari kwao na kwa wenzao. Methali zote katika kundi hili zinafuata nasaha ya methali *Tahadhari kabla ya athari* na zinafanya hivyo kwa kutochelea kumkasirisha

mwanajamii ikiwa kwa kufanya hivyo mwanajamii huyo atarekebishika. Methali hizi ni kama;

a) *Bendera ipepeayo sana mwishowe hupasuka*

Kwa kawaida bendera inapopepea huwa mlingotini. Hivyo, beramu hiyo huonekana na watu wote; wanaotaka kuiona na wasiotaka. Kutokana na kuwa juu mlingotini dhoruba nyingi huikumba ikiwa ni pamoja na upepo mkali. Bendera hapa imetumika kama jazanda ya mwanajamii yeyote msifika ama kutokana na uongozi au sifa nyingine yoyote inayomletea umaarufu miongoni mwa wanajamii wengine. Inawatahadharisha watu kama hawa kwa kuwaambia kuwa watahadhari kabla ya athari kwa kuwa jinsi jina lao linavyotukuka ndivyo wanavyopata maadui. Methali hii inaweza kuungwa mkono na methali isemayo '*mti hupigwao ni ule wenye matunda.*' Aidha, methali hii inaweza kutumika kwa viongozi katili wanaotumia mamlaka yao kupita kiasi kwa kuwafahamisha kuwa japo wanatisha sasa hawawezi kutisha milele bali iko siku watachanika.

b) *Mtenda wema kinyuki jazaye hulipwa moto*

Methali hii inatumia jazanda inayotokana na matumizi ya neno 'kinyuki'. Nyuki hutenda wema kwa kutengeneza asali ambayo hurinwa na mwanadamu baada ya kumchoma nyuki kwa moto. Hata hivyo, nyuki huendelea kutengeneza asali nyingine pale pale mzingani akisubiri mwanadamu aje tena amchome kwa moto na kumwibia asali yake. Jambo hili hujirudia mara kadha lakini nyuki hajifunzi kutokana na mabaya yaliyotumiwa na mwanadamu kumlipa wema wake. Kwa hivyo, kutenda wema kinyuki kumetumiwa kama mfano wa 'kutenda wema kijinga'. Hii ndio sababu methali hii haikusema *Mtenda wema jazaye hulipwa moto* bali *Mtenda wema kinyuki jazaye hulipwa*

*moto*. Methali hii inawaonya wanadamu kuwa wasifanye wema kijinga bali wajifunze na mambo yaliyowadhuru awali japo mema kwa kuwa ni hulka ya baadhi ya wanadamu kutendewa hisani wakalipa kwa hiana.

c) *Kilichomla baba na mwana kitamla*

Methali hii ina maana sawa na methali *Kilichompata ngwena na mamba vivyo hivyo* na *Mchoma janga hula na wa kwao*. Inachomaanisha ni kuwa kilichomdhuru baba kitamdhuru na mtoto pia. Japo methali hii haimtendei haki mwana, inaweza kutumika kwa njia chanya kuwanasihii wazazi. Inawaonya kuwa wanapofanya mabaya na kuchuma majanga huku na kule wakumbuke kuwa majanga hayo hayatawaathiri wao tu bali yatakuwa donda ndugu kwa vizazi vyao vitakavyofuata pia kwa hivyo watie tahadhari.

d) *Akipenda chongo huita kengeza*

Katika mtazamo chanya methali hii inatoa onyo. Inawaonya watu wanaong'ang'ania kitu kinachoonekana wazi kitawaletea madhara kwa kuwanasihii wakichunguze kwa makini ili waone kasoro yake. Isitoshe, inaweza kutumika kufafanua hali ya mtu ambaye anafanya jambo linaloonekana na watu wengine kama ambalo halitamletea mafao yoyote. Watu hawa wanakumbushwa kuwa kila mtu hutia thamani katika vitu tofauti maishani na hatufai kuwahukumu sana wenzetu kwa kufanya maamuzi fulani ya kibinafsi.

e) *Asazacho mwizi na mganga atwae*

Methali hii inaweza kutumika kuleta dhima chanya tu katika kumtahadharisha mtu ambaye amekumbwa na janga fulani. Inafahamika kuwa mara nyingi watu wengi wanapokumbwa na janga hutumia njia nyingi, wakati mwingine bila makini yoyote,

kujaribu kulikabili. Methali hii inawakumbusha watu kama hao kuwa wanaweza kupoteza hata kidogo ambacho shida iliyowakumba iliwaachia ikiwa hawatatia makini. Tahadhari inayonuiwa kwa watu hao inaweza kutolewa vizuri zaidi katika kauli ya kibalagha kama “unataka asazacho mwizi na mganga atwae?” Ujumbe wa methali hii unaweza kusesitizwa zaidi na methali ‘*Apatikanaye na mkasa hupatikana na visa.*’

*f) Fadhila ni utumwa*

Methali hii inamhusia mfadhiliwa na kumpa changamoto kuwa ajihadhari na kupenda sana vya bwerere akasahau kutarazaki mwenyewe kwa kuwa vya bwerere vinaweza kumtumbukia nyongo kwa kufanywa kama mtumwa.

*g) Samaki mmoja akioza huoza wote / Pono mmoja akioza huoza shazile*

Methali hizi huungwa mkono na methali isemayo ‘*Chombo hakizami tezi omo kikaowea.*’ Kama ilivyotajwa awali japo samaki mmoja anaweza kuwaambukiza wenzake uozo kama alivyo mtu mwenye tabia mbaya kundini, madai kuwa wote watapatwa na uozo huo si haki kwa kuwa hilo ni jambo lililotiliwa chuku na kujitenga na ukweli. Isitoshe, kumpa samaki mmoja aliyeoza uwezo wa kuwaozesha samaki wengine wote ni kumtukuza samaki huyo na hivyo kuufanya uozo wake (tabia mbaya) kuwa maarufu na kuigwa na wengine. Licha ya yote haya, methali hizi zinatoa tahadhari kwa wanajamii kuwa si vyema kumpuuza mwanajamii mmoja mwenye tabia zisizopendeza kwa kuwa matokeo ya tabia hiyo yanaweza kuiathiri jamii nzima.

#### 4.1.3 Kutoa mawaidha

Wazee katika jamii za Kiafrika, ambao ndio wanaoaminika kuwa waliibua methali, ndio waliokuwa na jukumu la kuwanasihi wanajamii kuhusu maswala mbalimbali. Wazee hasa waliwashauri watu kuhusu maswala ya kisiasa, kidini, kiuchumi na kijamii. Mawaidha haya wakati mwingine yalitolewa katika kusuluhisha migogoro katika jamii au kuhimiza sheria kwenye mahakama ndogo za kienyeji (Nzookwa, 2011). Kutokana na miktadha isiyo ya kupendeza ambayo baadhi ya methali hizi huibuka na kutumika hivyo, lugha yake huwa kavu na isiokuwa na hata chembe ya kubembeleza hivyo kuonekana hasi japo manufaa yake kwa jamii ni makubwa. Baadhi ya methali hizi ni;

*a) Mtaka nyingi nasaba hupata mwingi msiba*

Japo nasaba ni uhusiano wa kizazi baina ya watu, neno nasaba katika methali hii limetumiwa kumaanisha 'shughuli za maisha'. Methali hii ina maana kuwa anayetaka kujihusisha na shughuli nyingi za maisha zinazozidi hata uwezo wake atapatwa na shida nyingi maishani. Kivumishi cha idadi "nyingi" kimetumika kusisitiza umuhimu wa kiwango katika mambo ambayo mwanadamu anajihusisha nayo. Hii ni methali inayonasihia kuwa watu wajihusishe na kufuata mikondo michache ya maisha inayowafaa kwa kuwa haiwezekani kwa mtu mmoja kuwa na ujuzi wa kila kitu maishani. Aidha, inawanasihia wasiparamie mambo mengi maishani kwa sababu hawawezi kuutanganya ulimwengu wote.

*b) Angeenda juu kipungu halifikii mbingu*

Kipungu anayerejelewa hapa ni aina ya samaki anayejulikana na Waswahili wa visiwani kama "papa kipungu". Samaki huyu huwa na tabia ya kuruka juu kutoka baharini na

kisha kutumbukia majini tena kwa kuwa japo yeye hung'ang'ana kuruka hawezi kulifikia mbingu wala kubakia hewani kwa muda mrefu. Kipungu ametumika kama jazanda ya mwanadamu anayejaribu kujipatia uwezo mkubwa wa kiuchumi au kiutawala hivi kwamba anaonekana kama anayeshindania nafasi na Mwenyezi Mungu. Mwanadamu kama huyu huambiwa methali hii kuonyesha kuwa mwanadamu ana kiwango cha uwezo na wala hawezi kupata mamlaka kama aliyo nayo Mungu. Methali hii huwatanabaisha watu na kuwawekea mipaka ya uchu wao wa kutaka hadhi na mamlaka duniani huku ikiwakumbusha kuwa hata wakipata mamlaka kiasi gani hawawezi kupata uwezo unaomzidi Mwenyezi Mungu. Baadhi ya Waswahili husema "usilete ujabari kuvaa joho la Mungu kwa kuwa joho la Mwenyezi Mungu mja halimfai kitu." Vile vile, inadhibitisha ukweli wa kauli ya Wafula na Njogu (2007: 33) kuwa *Kiburi cha madaraka huzaa beberu.*

c) *Mke kipofu ni mwaminifu*

Mke kipofu katika methali hii ni jazanda ya mke ambaye anamwona mumewe pekee katika maswala ya mapenzi. Upofu wake si upofu wa kutoona kabisa au upofu wa kutoona kwa macho ya kawaida bali macho ya kidhahania ya mahaba. Mke huyu anamwona mumewe pekee katika muktadha wa mapenzi na kutowaona wanaume wengine wote; hivyo kuwa kipofu kwao. Inatumiwa kuwasia wanawake kuwa na uaminifu mkamilifu kwa waume wao na kupoteza hamu ya mahusiano na wanaume wengine kabisa kama ambavyo kipofu hupoteza uwezo wake wa kuona. Methali hii hutumiwa pia na wanajamii kumtakia mwanaume anayetafuta mke, mke mzuri. Mwanamume kama huyo huambiwa "ninakutakia upatane na mke kipofu."

d) *Cha mwerevu huliwa na mjinga*

Uerevu na ujinga unaorejewa katika methali hii haujawekewa mipaka ya uwezo mkamilifu wa kufahamu jambo fulani na ukosefu wa uwezo huo mtawalia, bali viwango vya ufahamu wa jambo hilo. Methali hii huelekezewa anayejifanya kuwa anafahamu kila kitu katika uwanja fulani wa maisha (mwerevu) kwa kuwaringia anaodhani kuwa hawafahamu chochote au hawana ufahamu wa kutosha. 'Mwerevu' anausiwa kuwa japo 'mjinga' hajui chochote kuna uwezekano kuwa ana jambo analoweza kumpiku kwalo. Nasaha kwa 'mwerevu' hivyo ni kuwa hafai kujifanya anajua kila kitu bali anafaa kuwaachia wengine nao wafanye mengine kwa kuwa labda wanaweza kuyafanya bora zaidi.

e) *Ukila pamwe na namiri igiza zake tabia*

Ugeni ni hali ambayo huwatatiza wengi kwa kushindwa jinsi ya kuhusiana na watu ambao hawajazoeana nao na kutojua hulka zinazoenziwa na wenyeji. Methali hii imetumia jazanda ya namiri kumaanisha wageni na hali nzima ya ugenini. Inanasihi kuwa mtu akienda ugenini anafaa achunguze kwa kuiga tabia za mahali hapo kwanza kabla ya kuonyesha hulka za kwao. Hii ni kwa sababu wakati mwingine ukubalifu wa mambo hutegemea muktadha na wahusika katika muktadha wenyewe. Jambo hili linaweza kuepusha aibu inayopatikana katika methali kama '*Maskini hajui kula na mkwasi, akianza kula samaki huanzia kichwani.*'

*f) Kafiri akufaaye si Islamu asiyekufaa*

Kafiri ni mtu asiyeamini dini ya Uislamu na hutumiwa na Waislamu kuonyesha dharau kwa watu wa dini zingine maana ambayo imesambaa miongoni mwa waumini na kutumika kila siku. Hata hivyo, kwa mujibu wa waumini wa dini ya Kiislamu, Quran haiwaorodheshi Wakristo na Wayahudi miongoni mwa kafiri bali kafiri inafaa kuwa na maana ya 'mtu asiyekuwa na dini yoyote au anayeabudu miungu ya kishirikina.' Quran inawarejelea watu wote ambao si Waislamu lakini wanamwabudu Mungu mmoja (Mungu wa Ibrahimu) kama 'Ahl al-kitab' yaani 'watu wa kitabu.' Hivyo, japo inaonyesha mapendeleo ya kidini, inanasih pia kuwa mtu anayetoa msaada wa aina fulani japo mbaya ni bora kuliko mzuri asiyeweza kusaidia kwa lolote. Inawanasih watu wasiwadharau wenzao na kuwabagua kwa misingi ya kidini na kikabila kwa kuwa labda hao ndio wanaweza kuwafaa zaidi ya wale wa karibu nao.

*g) Utajiri ni raha ya leo, mateso ya kesho ahera*

Methali hii inaweza kutumiwa kuwanasih watu kuwa wajihadhari na utajiri na wautumie kwa njia zifaazo kwa kuwa utajiri una anasa nyingi zinazoweza kumpotosha mtu na kumletea adhabu ya kesho ahera.

Kijumla, ni vyema kufafanua kuwa, dhima chanya ya methali za Kiswahili ndicho kiungo muhimu zaidi cha methali na ndicho kinachofaa kuangaziwa zaidi kwa kuwa manufaa yake kwa jamii ni ya moja kwa moja. Hata methali zinazoonekana kuwa na dhima hasi kama zilizochanganuliwa katika sura ya tatu husheheni dhima chanya katika muktadha fulani maalum ambao ndiyo wenye umuhimu kwa jamii. Methali zinazoonekana kukemea, kukejeli, kudhihaki na kukashifu hufanya hivyo katika juhudi za kuwakosoa na

kuwaadilisha wanajamii. Methali zenye ukali wa maneno zina uwezekano wa kuwa zilizuka katika mkutadha wa kuwarekebisha wanajamii ambao ni wagumu wa kutii au kuzingatia mawaidha. Kwa mfano, methali *Mtoto akililia wembe mpe* haionyeshi kutojali kwa mzazi au ukosefu wa mapenzi kwa mwanawe bali inatolewa katika juhudi za kumkosoa mwana mtundu. Jamii inalazimika kutumia mbinu zisizokuwa za kawaida kuwaongoa wanajamii ambao wana tabia zisizo za kawaida. Aidha, methali hii inafuata kanuni na falsafa ya jamii iliyo katika methali kama *Mchelea mwana kulia, mwisho hulia yeye na Zinguo la mtukutu ni ufito*.

Methali nyingi za Kiswahili huwaonya waja dhidi ya hulka na vitendo vinavyoweza kuwazulia balaa maishani kama vile *Bila silaha usiingie vitani na Jaza ya hisani ni hisani*. Matumaini na maliwazo katika hali ngumu za kimaisha pia hupatikana katika methali kama *Yaliyopita si ndwele tugange yajayo* huku methali kama *Mgema akisifiwa tembo hulitia maji, Mgaagaa na upwa hali wali mkavu na Mke ni nguo mgomba ni kupalilia* zikisawiri na kuhifadhi utamaduni wa Waswahili wa vinywaji na chakula mtawalia. Changamoto moja kubwa zaidi kwa lahaja za Kiswahili na lugha zingine za Kiafrika kwa sasa ni kufa kwake huku baadhi kama Kihadimu zikiwa zimeshakufa. Hivyo, methali za Kiswahili kama *Kazi mbi si mchezo mwema* na *Mui huwa mwema* hutekeleza jukumu muhimu katika kuhifadhi msamiati na vikale katika lugha hiyo ambavyo viko katika hatari ya kudidimia kutokana na kukosa kutumika au kutumika kwa nadra sana. Methali zingine huwapa wanajamii ushauri unaoweza kuwafaa zaidi maishani kwa kuwaelekeza kufanya mambo yatakayowaletea natija. Mifano ya methali hizi ni kama *Ndaulia haitoshi heri ni kuona mwenyewe, Udongo upatimize ungali maji, Samaki mkunje angali mbichi, Mchelea mwana kulia mwisho hulia yeye na Zinguo la mtukutu ni*



*ufito*. Mwisho, baadhi ya methali huwa na jukumu la kuiburudisha jamii kwa kusheheni lugha tamu na yenye mnato na mguso unaovutia usomaji na usikilizaji. Mfano wa methali inayotekeleza jukumu hili ni kama *Pemba peremba, ukija na winda utarudi na kilemba*.

## 4.2 KIISHILIO

Sura hii imebainisha kuwa methali za Kiswahili zinaweza kuwa na ufasiri tofauti kutegemea mambo mbalimbali ambayo ni pamoja na muktadha wa matumizi, dhamira au lengo la mfasiri, dini, mlengwa, jinsia n.k. Baadhi ya methali zilizotolewa maelezo ya kuwa na dhima hasi katika sura ya tatu zilichanganuliwa upya na kupewa dhima chanya hivyo kudhibitisha ukweli wa nadharia ya Udenguzi iliyotawala utafiti huu kuwa matini inaweza kufasiriwa kwa zaidi ya njia moja na kutoa maana tofauti katika kila ufasiri, na kuwa wahakiki wanaruhusiwa kutoa fasiri tofauti za matini moja, hata zinazokinzana, mradi wana ushahidi wa kutosha.

Imebainika pia kuwa, nyingi za methali hasi hupata uhasi kwa kutilia maswala zinazorejelea chuku. Hata hivyo, jambo hilo halitendeki kwa kutaka kuleta uhasi bali kwa ama kutaka jamii ione uzito wa jambo husika ili iogope na hivyo kuepukana na hatari au kulirahisisha jambo linaloumiza mioyo na hisia za wanajamii ili wapumbazike, kuliwazika na mwishowe kuusahau uchungu unaoletwa na jambo husika. Katika kuitekeleza dhima hiyo, methali hizi huishia kuzitoa hali husika katika uhalisia na kuzielekeza katika udhahania ambao huibua utata wa kimaana na kidhima huku dhima hasi ikipata nafasi yake pia. Hivyo, katika sura hii methali hizo zimechanganuliwa kwa kuhusishwa na miktadha tofauti na kupatikana kuwa zina dhima chanya kwa jamii pia.

Sura inayofuata itakamilisha utafiti kwa kutoa matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo kwa utafiti zaidi.

## **SURA YA TANO**

### **HITIMISHO, MATOKEO NA MAPENDEKEZO**

#### **5.0 UTANGULIZI**

Sura hii inayotukamilishia utafiti huu imebeba muhtasari wa mambo yote yaliyozingatiwa katika utafiti. Matokeo ya utafiti ambayo yamebainishwa kwa kuzingatia maswali na malengo ya utafiti yamefafanuliwa. Isitoshe, sura hii imetoa mapendekezo yanayoweza kuwachochea watafiti wa baadaye kufanya utafiti zaidi kwa kuwa methali ni kiungo muhimu cha lugha na fasihi ya takriban kila jamii na zina historia ndefu ya matumizi.

#### **5.1 HITIMISHO NA MATOKEO YA UTAFITI**

Utafiti huu ulimulika kwa undani dhima ya methali za Kiswahili na kuonyesha kuwa methali ni kiungo muhimu sana cha lugha ya Kiswahili. Kando na dhima chanya hata hivyo, baadhi ya methali hizo hubeba dhima hasi ambayo ama huwa ya kipekee katika methali husika au huwa mojawapo wa dhima nyingine chanya, zote zikijitokeza katika miktadha tofauti. Malengo ya utafiti huu yalikuwa kutambua miktadha ya matumizi ya methali za Kiswahili, kuziainisha methali za Kiswahili zenye dhima hasi kutegemea uhasi wake na kutambua manufaa ya methali za Kiswahili zenye dhima hasi kwa jamii.

Utekelezaji wa malengo haya ulifanyika kwa kuzichanganua methali teule kwa mujibu wa mihimili teule ya nadharia ya Udenguzi. Nadharia hiyo ilitumiwa kufafanua maana na dhima mbalimbali zinazopatikana katika methali za Kiswahili kwa kusisitiza dhima hasi

kwa kuwa tayari methali za Kiswahili zimetolewa maelezo mengi yanayozipa dhima chanya. Nadharia hii iliusaidia utafiti huu katika kuziumbua methali za Kiswahili na kuonyesha sura zake zilizofichika ambazo ni hasi. Lengo kuu la utafiti lilikuwa kuonyesha kuwa kando na dhima chanya methali za Kiswahili huwa na dhima hasi japo methali moja inaweza kubeba dhima zote mbili na dhima hizo kujitokeza kutegemea muktadha wa matumizi.

Methali zilizochanganuliwa katika utafiti huu ni zile zinazopatikana katika kamusi mbalimbali za methali zilizochapishwa nchini Kenya na watafiti mbalimbali kuanzia miaka ya 1980 hadi sasa. Sababu ya kuchagua sampuli hii ni kuwa mtafiti alikusudia kuchunguza methali za Kiswahili zinazotumika nchini Kenya na hasa zinazotokana wa Waswahili wa pwani ya Kenya. Katika kipindi kilichotajwa watafiti wamelizamia swala hili la methali kwa lengo la kukusanya methali zaidi na zaidi na kwa sasa wamefaulu kukusanya methali takriban elfu tatu. Ifahamike kuwa japo utafiti huu umezijasidili methali za Kiswahili kwa kuonyesha dhima hasi katika baadhi yake, idadi hii ni ndogo sana ikilinganishwa na idadi kubwa ya methali zote za Kiswahili. Kwa hivyo, utafiti huu haukuwa na nia ya kuonyesha jinsi methali za Kiswahili zisivyo na dhima yoyote chanya bali kuwa methali moja ina uwezo wa kuwa na zaidi ya dhima moja na kuwa katika baadhi ya methali dhima hiyo huwa hasi.

Sura ya kwanza imebainisha maswali ya utafiti na malengo yake pamoja na kudhihirisha mbinu zilizotumiwa kuufanikisha utafiti. Sura ya pili imefafanua mambo muhimu kuhusu miktadha ya matumizi ya methali kijumla na sifa za methali za Kiswahili. Kimsingi ilibainika kuwa jamii ya Waswahili imejengwa katika mwamba wa utamaduni mkongwe

wenye mizizi yake kote Afrika Mashariki, Mashariki ya kati na Mashariki ya Mbali kuanzia karne nyingi nyuma. Methali zake hivyo zimebeba mchanganyiko wa dhana; baadhi zinazowakilisha falsafa ya kijumla ya maisha ya watu kutoka sehemu mbalimbali na baadhi maoni ya wanajamii fulani waliowahi kuishi Uswahilini. Kwa sababu hii, methali za Kiswahili hasa zinazohusu maisha ya jadi zinafaa kuchujwa kwa misingi ya dhima yake katika miktadha tofauti ya kijamii kwa kuangalia zinampendelea mwanajamii yupi katika miktadha mbalimbali na kwa misingi hiyo zina uwezekano wa kuwa zilibuliwa na nani.

Kuna umuhimu wa kuangalia pia ikiwa methali husika zina uwezo wa kubadilika ili kukimu mahitaji ya jamii ya kiharakati ikiwa ni pamoja na kutetea haki za usawa wa kijinsia na kukomesha ukabila, utabaka, taasubi za kiume na kike, ufasadi na chuki za kidini miongoni mwa mengine ikitiliwa maanani kwamba hali ya maisha ya wakati wa kubuniwa kwake ilikuwa tofauti kabisa na hali ya sasa. Aidha, ilibainika kwamba methali za Kiswahili zimetokana na mazingira ya Uswahili, utamaduni na dini ya Kiislamu.

Uchanganuzi wa methali teule katika sura ya tatu ulibainisha kuwa baadhi ya methali za Kiswahili huwa na dhima hasi; iliyo wazi au iliyofichika ambayo ni pamoja na kuchochea vita, kudharau wanyonge, kuvunja moyo, kudhihaki ulemavu na kuleta ubaguzi wa kikabila, kijinsia, kidini na kiumri miongoni mwa wanajamii. Ikikumbukukwa kuwa methali zizo hizo zimetolewa maelezo chanya katika kamusi mbalimbali za methali na pia katika sura ya nne, utafiti huu ulibainisha ukweli wa nadharia ya Udenguzi iliyotumika kuwa matini moja inaweza kufasiriwa kwa njia tofauti na kuishia kutoa maana nyingi tofauti mradi mfasiri ana ushahidi wa kutosha. Aidha,

ukweli kuwa methali hazikuibuka katika ombwe tupu bali ni zao la tajriba, utamaduni, imani na historia ya jamii pia lilidhibitika kutokana na baadhi baadhi ya methali kuzihusisha na tukio mahsusi la kijamii au kidini lililowahi kutendeka au linaloaminika kuwa lilitendeka.

Sura ya nne ilidhibitisha kuwa methali ni mojawapo wa kauli muhimu zaidi na zinazotumika sana miongoni mwa wanajamii katika matumizi yao ya lugha. Ilibainika kuwa japo baadhi ya methali za Kiswahili zina dhima hasi na zinafaa kuchujwa, kuchujwa huko kunafaa kutendeka kwa njia ya kuifafanua dhima hiyo hasi ili ijulikane na watumiaji lugha ili kuweza kuepukwa huku dhima yoyote chanya inayoweza kujitokeza katika methali iyo hiyo katika muktadha tofauti ikitiliwa mkazo zaidi. Methali hizo hazifai kutupiliwa mbali kabisa kwa sababu zina umuhimu katika fasihi na lugha ya jamii.

Kwanza, baadhi zina ukweli wa hali halisi ya kimaisha hususan ya unyanyasaji, dhuluma na unyonyaji unaotendewa maskini na wanyonge wa aina mbalimbali katika jamii pamoja na uroho na umeru wa 'wenye nacho' katika jamii wanaofanya kila juhudi kumdidimiza na kumzamisha maskini katika umaskini zaidi. Vile vile, baadhi zinaonyesha kasumba za kijamii na kidini zinazowapotosha watu maishani na kuwafanya kuishi maisha yaliyokosa matumaini hasa kwa kutegemea kudura. Ni kwa kufahamu methali hizi na uhasi wake tu ambapo watu wanaweza kuhamasishwa na kufundishwa jinsi ya kushinda kasumba maishani na kuishi maisha chanya.

Pia, zipo baadhi ya methali hizo ambazo zimebeba historia ya jamii kwa kutaja hali za kale za kimaisha na maeneo ya kale yasiyofahamika sasa kama vile *Mkele* pamoja na visa

vingine vilivyowahi kuikumba jamii ya kale kama vile vita kati ya Wamvita na Wapate na ugomvi kati ya Waswahili na Wagalla.

Isitoshe, methali hizi zinaweza kutufundisha mfumo wa lugha ya kale hasa msamiati. Kupitia kwake tunaweza kutathmini mabadiliko ambayo lugha ya Kiswahili imepitia kihistoria na tofauti zake kilahaja kwa kuwa methali mbalimbali zimetokana na watu wa lahaja mbalimbali na hata lugha zingine za kibantu zinazopakana na Waswahili.

Ikumbukwe kuwa, maana na dhima ya methali hutegemea muktadha na mfasiri au mhakiki, na labda haikosi muktadha ambao methali hizo zinaweza kutumika kwa njia chanya; aghalabu kusisitiza hoja au kuipamba kazi ya fasihi na kusisitiza hoja zake.

## **5.2 MAPENDEKEZO**

Utafiti huu umeongozwa na misingi ya nadharia ya Udenguzi inayozingatia kuwa lugha haina maana inayodumu na hatuwezi kubainisha wazi tunachomaanisha. Matini haiwezi kumpa msemaji maana moja kwa kuwa lugha yenyewe huwa na utata. Kwa mantiki hii, maana hubadilika kutegemea miktadha, hali za wahusika, mazingira na kadhalika. Vile vile, Udenguzi hutambua kuwa jukumu la mdenguzi ni kuchunguza ni kwa njia gani maana moja inapendelewa katika matini au mjadala. Maana moja inaweza kupendelewa kwa kuchukuliwa kuwa ya kipekee, iliyojitenga, yenye ukweli, yenye thamani, yenye umuhimu au yenye ujumla zaidi ya vinyume vyake. Kutokana na haya, ipo haja ya watumiaji wa methali za lugha ya Kiswahili na hasa wataalamu wa lugha hiyo ambao ni pamoja na waandishi wa vitabu, wanahabari na walimu kufahamu kuwa methali za Kiswahili hubeba dhima hasi japo haijapendelewa na jamii kwa kuonekana kuwa haina

thamani. Utafiti huu unapendekeza mtazamo kuwa methali kama zilivyo matini zingine zinaweza kuwa na zaidi ya kinyume kimoja na maana nyingi za methali zinaweza kupendelewa kwa wakati mmoja kutegemea muktadha wa matumizi. Ni kwa kufahamu jambo hili ambapo pia itafahamika methali zisizofaa kutumika katika miktadha fulani kutokana na uhasi wake katika miktadha husika.

Ni vyema kufahamu kuwa methali huundwa kutokana na msamiati unaochotwa katika hazina ya jamii husika pamoja na tajriba zake. Itamwia mtumiaji asiyetoka maeneo ya Uswahilini vigumu kufahamu maana na dhima za baadhi ya methali bila kuwa na uelewa wa msamiati husika kama unavyofahamika katika jamii zalishi. Jambo hili linadhibitisha ukweli kuwa kusambaa kwa methali katika maeneo ya mbali na Uswahilini pamoja na mabadiliko ya jamii yamechangia baadhi ya methali kupoteza maana na dhima zake za awali au kupata maana na dhima nyingine juu ya ile ya awali. Tatizo hili pia linawakumba Waswahili wa sasa ikifahamika kuwa jamii hiyo imebadilika sana katika itikadi zake, mifumo ya kiuchumi, kazi, mifumo ya elimu na kadhalika na baadhi ya maswala yanayoenziwa katika methali (ambayo bila shaka yalienenziwa na jamii ya kale) yamepoteza umuhimu wake na kuonekana kama yaliyopitwa na wakati au hata kukashifiwa kuwa uvunjaji wa haki za binadamu. Utafiti huu unapendekeza kuwa mabadiliko haya yaliyoikumba jamii na yaliyobadilisha mwonoulimwengu wa jamii katika takriban kila kitu, methali zikiwemo, yanafaa kutiliwa maanani na hasa waandishi wa kamusi za methali pamoja na waandishi wa kazi zingine za kifasihi ili kupewa nafasi ya kuchangia uamuzi wa ufaafu wa matumizi ya baadhi ya methali za Kiswahili katika miktadha fulani ya jamii.

Hali ya watafiti na hasa waandishi wa kamusi za methali kuzitetea methali na kujaribu bila kufua dafu kuonyesha uchanya wa baadhi ya methali teule inadhihirisha kuwa wanajamii hawajaribu kufikiria kuwa tamathali za usemi ziliundwa na wanajamii kama wao ambao baadhi wangeibua kauli hasi zinazotekeleza maslahi yao wenyewe wala ukweli kuwa hali ya jamii imebadilika tangu kuundwa kwa methali hizo na kilichokubalika wakati huo kinaweza kuwa hakikubaliki kwa sasa. Kwa kuwa waandishi hawa waliandika kamusi zao baada ya kufanya utafiti kwa wanajamii hasa wa jamii za Pwani, ni dhahiri kuwa wanajamii hao pia wanashikilia mtazamo huo. Kwa hivyo, watumiaji wa methali wanafaa kufahamu kuwa kiini asilia cha mtunzi wa matini hakiathiri maana za mtumiaji wala mhakiki kwa vyovyote bali kilicho muhimu tokea hapo ni mhakiki na matini, pamoja na fasiri anazozipata kutokana na mantiki itokanayo na muktadha wa jamii na uelewa wao. Pia, ni muhimu hata zaidi ifahamike kuwa, kazi inayohakikiwa ina maana yenyewe na kuna uwezekano wa fasiri nyingi kutolewa kwa kazi moja kutegemea wasomaji na wahakiki wa kazi hiyo wala haina haja ya mtu yeyote kuisemea isichosema kwa lengo la kuipa dhima fulani.

Isitoshe, itawafaa wanaokusanya methali za Kiswahili na kuandika kamusi zake kufafanua maana tofauti za methali husika pamoja na dhima zake mbalimbali zinapotumika katika mazingira tofauti badala ya kuangazia dhima chanya pekee. Ubadilikaji wa maana na dhima ya methali kutegemea mabadiliko ya kijamii unafaa kutiliwa maanani na waandishi wa kamusi katika toleo jipya za kamusi za methali za Kiswahili kwa kuwa jamii haibakiii mahali pamoja bali inabadilika, na hivyo kuzilamisha tamathali zake kupoteza maana na dhima za awali. Utafiti huu unapendekeza kuwa utafiti

zaidi unaweza kuendelezwa ili kushughulikia maswala ambayo hayakuangaziwa katika tasnifu hii.

Kwa mfano, watafiti wa baadaye wanaweza kutafiti matumizi ya methali zenye dhima hasi katika kazi za fasihi andishi. Uchunguzi huu utatuwezesha kufahamu miktadha ambayo waandishi wa riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi hutumia methali zenye dhima hasi na kuhakiki uhasi na chanya wa miktadha hiyo. Aidha, utafiti zaidi unaweza kufanywa kuzidahili methali za Kiswahili zenye dhima hasi kama tamathali za usemi zinazokuza maudhui hasi katika fasihi andishi ya Kiswahili.

Pia, utafiti zaidi unaweza kuangazia wingi-dhima katika tamathali zingine za usemi za lugha ya Kiswahili kama vile nahau au kuchanganua methali za lugha zingine za Afrika Mashariki kidenguzi ili kufahamu ikiwa baadhi yazo zina dhima hasi, pamoja na kuchanganua miktadha ya matumizi ya methali hizo.

Mwisho, utafiti zaidi unaweza kufanywa kubaini methali kama chombo kinachohifadhi tamaduni, itikadi, kasumba na imani za jamii zilizopitwa na wakati.

## MAREJELEO

- Abdullah, S. A. S. (1969) *Quran Takatifu*. Nairobi: Nairobi Islamic foundation
- Abudu, M. na A. Baruwa, (1981) *Methali za Kiswahili: Maana na Matumizi*. Nairobi: Shungwaya Publishers
- Achebe, C. (1962) *Things Fall Apart*. London: Heinemann
- Amory, D. (1985) "Kanga Cloth and Swahili Society: Mke ni Nguo" Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Yale (hajjachapishwa)
- Andambi, A. na E. Murono, (2005) *Muundo Mpya wa Methali za Kiswahili*. Nairobi: Mvule Afrika Publishers.
- Anozie, S. (1981) *Structural Models and African Poetics*. London: Routledge and Kegan Paul
- Arewa, O. na A. Dundes, (1964) 'Proverbs and the Ethnography of Speaking Folklore'. In: 'American Anthropologist'.
- Balkin, J. M. (1990). "Tradition, Betrayal, and the Politics of Deconstruction,". Faculty Scholarship Series. Paper 283
- Bambara, T. C. (1998) *African American Literature; Voices in Tradition*. New York: Harcourt Brace and Company
- Barthes, R. (1977) 'The death of the Author'. *Image Music -Text.* Tafsiri ya Stephen Health. London: Fontana Pg. 142-148
- Belsey, C. (2004) 'Literature, History, Politics' In: Donald Keesey (3<sup>rd</sup> Ed), *Contexts for Criticism*. London: Mayfield publishing company
- Bible Society of Kenya, (1995) *Biblia Takatifu; Habari Njema kwa Watu Wote*. Nairobi
- Biersteker A. na I. N. Shariff, (1995) *Mashairi Ya Vita Vya Kuduhu*. Ann Arbor: Michigan State University Press
- Chacha, N. C. (1980). "Ushairi wa Abdallatif Abdalla." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Nairobi (Hajjachapishwa)
- Chesaina, C. (1997) *Oral Literature of the Embu and Mbeere*. Nairobi: EAEP
- Cuddon, A. (1991) *Dictionary of Literary Terms and Literary Theory*. Third ed. London: Blackwell

- Culler, J. (1975) "*Defining Narrative Units.*" In: *Style and Structure in Literature.* Ed. R. Fowler. Ithaca: Cornell University Press
- Davison, B. na wenzake (1967) *The Growth of African Civilization East and Central Africa to the 9<sup>th</sup> Century.* Nairobi: Longman
- Derrida, J. (1976) *Of Grammatology.* Translated By Gayatri Chakravorty Spivak. Baltimore: John Hopkins University Press
- Dolozel, L. (1973) *Narrative Modes in Czech Literature.* Toronto: University of Toronto.
- Durkheim, E. (1933) *Division of Labor in Society.* Illinois: The Free Press of Glencoe
- Eagleton, T. (1983) *Literary Theory; An Introduction.* London: Blackwell
- Evans-Pritchard, E.E. (1956) "Sanza a characteristic feature of Zande language and thought." *The Bulletin of the School of Oriental and African Studies.* Vol. 18
- Evans-Pritchard, E.E. (1963) "Meaning in Zande proverbs." *Royal Anthropological Institute of Great Britain and Ireland Journal* Vol. 63 pp. 4-7
- Finnegan, R. (1970) *Oral Literature In Africa.* Oxford: Clarendon Press
- Gellner, E. (1973) *Cause and Meaning in the Social Sciences.* Boston: Routledge Kegan Paul
- Genette, G. (1980) *Narrative Discourse: An essay in Method.* Ithaca: Cornell University Press.
- Gibson, J. (1979) *The Ecological Approach to Visual Perception.* Boston: Houghton-Mufflin
- Goring P. na wenzake (2001) *Studying Literature: The Essential Companion.* London: Anold
- Grice, H. P. (1975). "Logic and Conversation." In: Cole, P. & Morgan, J. (Eds.), *Syntax and Semantics* (pp. 41-58). New York: Academic Press.
- Jakobson, R. (1988) *Language in Literature.* Ed. Krystyna P. and Stephen R. : Belknap Press.
- Kabira, W.M. na K. Mutahi, (1988) *Gikuyu Oral Literature.* Nairobi: Heinemann Kenya
- Kanu, I. A. (2014) "Igbo Proverbs as Embodiments of Igbo-African Philosoph." *International Journal of Humanities and Social Science* Vol. 4 No. 1; pg 164-168
- King'ei, K. na A. Ndal, (2008) *Kamusi ya Methali; Toleo Jipya.* Nairobi: EAEP

- Kinoti, T. (2008) *Fasihi Simulizi na Utamaduni; Kitabu cha Walimu na Wanafunzi (Shule na Vyuo)*. Nairobi: Jomo Kenyatta foundation
- Knappert, J. (1979) *Myths and Legends of the Swahili*. Nairobi: Heinemann Kenya
- Knappert, J. (1979) *Four Centuries of Swahili Verse: A Literary History and Anthology*. London: Heinemann
- Kropáček, L. (1997) "Some Remarks on Swahili Proverbs." *Archiv Orientální*
- Leech, G. (1983) *Principles of Pragmatics*. London: Longman
- Ligami, P. na S. Barasa, (2006): "Tahakiki ya Methali za Kiswahili", katika Njogu, K., Momanyi, C. na Mathooko, M. (Wah.) *Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Nairobi: Twaweza Communications.
- Lioba, M. (2006) "The Globalized World Languages: The Case of Kiswahili." Katika Olaoba, F. A. na Michael, A. P. (Wah.) *Selected Proceedings of the 36th Annual Conference on African Linguistics*. Somerville, MA: Cascadilla Proceedings Project. [www.lingref.com](http://www.lingref.com), document #1421. Pg. 166-175
- Madumulla, J.S. (1995) *Proverbs and Sayings, Theory and Practice*. Dar es Salaam: Dar es Salaam institute of Kiswahili studies
- Maitaria, J. N. (1991) "Methali za Kiswahili kama Chombo cha Mawasiliano: Mtazamo wa Kiisimu Jamii." *Tasnifu ya uzamili. Chuo kikuu cha Kenyatta.*(Haijachapishwa)
- Marie, B.R. (2001b). 'Ambiguous Signs: The Role of the Kanga as a Medium of Communication.' *Swahili Forum, Vol. 8* pg. 157–169; <http://www.ifeas.uni-mainz.de/SwaFo/Volume8.html>
- Matteru, M.L.B. (1983) "Fasihi simulizi na Uandishi wa Kiswahili" katika: *Fasihi*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mazrui, A.M. na B. K. Syambo, (1992) *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: EAEP
- Mbaabu, I. (1985) *Utamaduni wa Waswahili*. Nairobi: KLB.
- Mbaabu, I. (1996) *Language Policy in East Africa*. Nairobi: Educational research and publications.
- Mey, J. L. (2001) *Pragmatics: An Introduction*. London: Blackwell
- Mieder, W. (2004) *Proverbs - A Handbook*. Westport, CT: Greenwood Press.
- Miruka, O. (1994) *Encounter with Oral Literature*. Nairobi: EAEP

- Msokile, M. (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: EAEP
- Mung'athia, R. (2011) "Ufumbuaji wa Mashairi ya Kiswahili: Mfano wa Malenga wa Mvita na Malenga wa Vumba." Tasnifu. Chuo Kikuu cha Kenyatta (haijachapishwa)
- Muriel, S. (1982) *The ethnography of communication: an introduction*. Oxford: Basil Blackwell.
- Mwamzandi, I. (2013) 'Riwaya Teule za Karne ya Ishirini na Moja na Udurusu wa Nadharia za Fasihi' Katika: Swahili Forum 20: 48-66
- Mwikali, K. na P. Coughlin, (1990) *Barking, You'll be eaten! The wisdom of Kamba Oral Literature*. Nairobi: Afropress Ltd
- Nandwa, J. na A. Bukenya, (1983) *African Literature for Schools*. Nairobi: Longhorn publishers
- Ndungo, C. (1998) "Images of women in African Oral Literature: A Case of Gikuyu and Swahili Proverbs." Tasnifu. Chuo Kikuu cha Kenyatta (haijachapishwa)
- Ng'etich, D.K. (2011) "Dini kama Chombo cha Kuwadhulumu Waumini: Mifano Kutoka Fasihi katika Kiswahili." Tasnifu. Chuo Kikuu cha Kenyatta (haijachapishwa)
- Ngugi, P. na P. Musau, (1999) *Kunga za Kiswahili*. Nairobi: Didaxis
- Ngure, A. (2003) *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari*. Nairobi: Phoenix publishers
- Njogu, K. na R. Chimerah, (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta foundation
- Norick, N. R. (1985) *How Proverbs Mean*. New York: Mouton Publishers
- Nsookwa, J. C. 2011). "Dokezo za Sitiari katika Methali za Kiswahili na Kiganda" Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu. Chuo Kikuu Cha Makerere (haijachapishwa)
- Nyembezi, C. (1954) *Zulu Proverbs*. Johannesburg: Witwatersrand University Press
- Odaga, A. (1984) *Yesterday's Today: The Study of Oral Literature*. Kisumu: Lake Publishers and Enterprises.
- Odaga, B.A. na K. S. Akivaga, (1982) *Oral Literature, A School Certificate Course*. Nairobi: EAEP
- Okpewho, I. (1992) *African Oral Literature*. New York: Indiana university press.
- Polome, E.C. (1967) *Swahili Language Handbook*. Washington D.C.: Center For Applied Linguistics

- Propp, V. (1968) *Morphology of The Forktale*. Austin: University of Texas Press
- Schipper, M. (1991) *Source of All Evil: African Proverbs and Sayings On Women*. Nairobi: Phoenix publishers.
- Seitel, P. (1972). "Proverbs and the Structure of the Metaphor among the Haya of Tanzania." *Tasnifu ya Uzamifu*. Chuo Kikuu cha Pennsylvania, USA (haijachapishwa)
- Senkoro, F .E. M. (1988) *Ushairi: Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press
- Sperber, D. (1995) "How do we Communicate." In: Brockman, J. & Matson, K. (Eds.), *How Things Are: A Science Toolkit to the Mind* (pp. 191–99). Morrow.
- Strobel, M. (1979) *Muslim Women in Mombasa 1890-1975*. London: Yale university press
- Tylor, A. (1962) *The Proverb and Index to the the Proverb*. Copenhagen: Rosenkilde and Bagger.
- Vansina, J. (1985) *Oral Tradition as History*. Nairobi: EAEP
- Wafula, R.M. na K. Njogu, (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Waihiga, G. na F. Kagwa, (2007) *Kamusi Changanuzi ya Methali*. Nairobi: Macmillan
- Wamitila, K.W. (2001) *Kamusi ya methali*. Nairobi: Longhorn Publishers
- Wamitila, K.W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers
- Wamitila, K.W. (2003) *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books
- Wamitila, K.W. (2003) *Kichocheo Cha Fasihi*. Nairobi: Focus books
- Yankah, K. (1989) *The Proverb in the Context of Akan Rhetoric*. New york: Peter Lang Publishing

## **KIAMBATISHO A**

### **METHALI TEULE**

1. Adhaniaye amesimama aangalie asianguke.
2. Adui ukimtahadhari mara moja rafiki utamtahadhari mara mia.
3. Ajali haina kinga/ Ajali haikingiki
4. Akipenda chongo huita kengeza
5. Akosapo mkubwa mdogo huadhibiwa
6. Akusameheaye deni amekunyima mkopo.
7. Akutendaye mtende, usimche akutendaye
8. Akutendaye mtende, usimche akutendaye.
9. Alalaye usimwamshe, ukimwamsha utalala wewe.
10. Aliye juu mngoje chini
11. Aliye na nguvu hula dhaifu hulipa.
12. Aliyekunyoa shungi kakwepushia kuchana.
13. Aliyeshiba hamkumbuki mwenye njaa.
14. Amani haiji ila kwa ncha ya upanga/ Suluhu haiji ila kwa ncha ya upanga.
15. Amechagua nazi akapata dafu.
16. Anayenyolewa kwa chupa hasahau
17. Anayepandisha wengine hupigwa teke menoni.
18. Aridhikaye na umaskini wake ni tajiri wa ajabu
19. Asiye mali hasidi wa mwenye mali
20. Asiye na mwana aeleke jiwe
21. Asiyejua maana haambiwi maana.

22. Asiyekuwapo machoni na moyoni hayupo
23. Asiyekuwapo na lake halipo
24. Baba wa kambo si baba.
25. Bahati humwacha wa mbele na kumfuata wa nyuma.
26. Bendera ipepeayo sana mwishowe huchanika.
27. Bibi mzuri hakosi kilema
28. Bibi wa ovyo hupata mume mzuri.
29. Bidii ya mja haikidhi haja.
30. Cha kuzama hakina rubani / Cha kuzama hakina usukani
31. Cha mfupi huliwa kichwani
32. Cha mfupi huliwa na mrefu
33. Cha mwerevu huliwa na mjinga
34. Chema hakidumu / hakikai/ hakina maisha
35. Dau la mnyonge haliendi joshi, likienda ni Mwenyezi Mungu kupenda
36. Dua la kuku halimpati mwewe
37. Fadhila ni utumwa.
38. Funika kombe mwanaharamu apite.
39. Hakuna mchele usiokuwa na ndume
40. Hakuna mkika muungwana
41. Ikiwa hana kazi (mume) hajaliwi
42. Ivumayo haidumu
43. Jahazi la mkata haliendi joshi
44. Jicho la mkata halioni, likiona haliongozi

45. Jitihada haiondoi kudura
46. Jogoo halei mwana
47. Kaburi la mke mwenza li kombo.
48. Kafiri akufaaye si Islamu asiyekufaa
49. Kiingiacho mjini si haramu
50. Kila likuepukalo mwanadamu lina heri nawe
51. Kila mwamba ngoma huvuta kwake.
52. Kilichomla baba na mwana kitamla
53. Kizuri hakikosi ila.
54. Kufa kikondoo ndiko kufa kwema / kiungwana.
55. Kufa kwa wengi ni harusi
56. Kuku akemea mnyakuzi anyakua
57. Kuku jike hawiki penye jogoo
58. Kuku wa mkata hatagi na akitaga hufa
59. Kuku wa mkata hatagi, akitaga haangui na akiangua vifaranga hutwaliwa na  
mwewe
60. La mnyonge haliendi joshi, likienda litazama
61. La mnyonge halina mashiko
62. Liandikwalo halifutiki
63. Liandikwalo kuwa halina uzio
64. Liandikwalo lina mhuri
65. Liandikwalo ndilo liwalo
66. Mahaba ya wanadamu si mambo ya dawamu.

67. Mapenzi ya maskini hayaonekani
68. Mashua ya mnyonge huzama mtoni
69. Maskini haokoti, akiokota kaiba
70. Mgala mwuue na haki umpe.
71. Mjukuu si mwana akilia mpeleke kwao.
72. Mkata hampendi mwana
73. Mkata hendi Mkele, angenda Mkele na kujaza mtele jahazi tele hurudi na upele
74. Mke kipofu ni mwaminifu.
75. Mkono usioweza kuukata ubusu.
76. Mnyonge kupata haki ni mwenye nguvu kupenda
77. Mnyonge msonge
78. Mtaka mbele mpishe
79. Mtaka nyingi nasaba hupata mwingi msiba.
80. Mtashi hana haya au kinyongo
81. Mtenda mema kinyuki jazaye hulipwa moto.
82. Mtoto wa nyoka ni nyoka.
83. Mtu hauzi kabila lake.
84. Mtumbwi wa maskini huzama
85. Mume ni kazi mke ni nguo.
86. Mume ni moto wa koko usipowaka utafuka.
87. Mungu humpa alalaye na aliye kitako.
88. Mwana kidonda mjukuu kovu

89. Mwana mtukutu hali ugali mtupu.
90. Mwana na ndugu kirugu, mjukuu ni mtu mbali / mwanangwa
91. Mwanamke hapendezi ila dafuni mwake
92. Mwanamme ni mbono hualika kule.
93. Mwenda Pate harudi kirudicho kilio
94. Ng'ombe wa maskini hazai pacha
95. Ngoma ya vijana/wana haikeshi.
96. Nisimbulie unipe mnyonge hana kinyongo.
97. Pono mmoja akioza huoza shazile
98. Samaki mmoja akioza huoza wote
99. Ukikinai kichache Mungu atakupa kingi
100. Ukila pamwe na namiri igiza zake desturi
101. Ulitakalo hupati hupata hujaliwalo.
102. Ushaufu si sifa ya mwanamke
103. Utajiri ni raha ya leo mateso ya kesho ahera.
104. Uungwana haufai bora ni ndarama.
105. Wakimbia kufiwako wenda kuliwako nyama.
106. Waovu wana maisha marefu.
107. Wino wa Mungu haufutiki
108. Ya mkiwa haita na ikita hupapata.
109. Ya mkiwa haizai nyike / jike.